

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA MANISPAA – MPANDA**



**MKUTANO WA NNE WA BARAZA LA MADIWANI KWA MWAKA  
2017/2018 KITAKACHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA TAREHE 25/07/2018  
KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

**TAARIFA ZA KATA**

**Imetayarishwa na:**  
OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA,  
S.L.P. 216,  
**MPANDA**  
SIMU NA 025-252957128,  
FAX NA 025-252957129,  
[Email: md@mpandamc.go.tz](mailto:md@mpandamc.go.tz)

**JULAI 2018**

MUHTASARI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 25/04/2018.....	3
YATOKANAYO NA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE 25.04.2018.....	8
KATA YA ILEMBO .....	9
KATA YA KAKESE .....	19
KATA YA KASHAULILI.....	26
KATA YA KASOKOLA.....	35
KATA YA KAWAJENSE.....	42
KATA YA KAZIMA .....	49
KATA YA MAGAMBA.....	56
KATA YA MAKANYAGIO .....	64
KATA YA MAJENGO .....	70
KATA YA MISUNKUMILO.....	78
KATA YA MPANDA HOTEL.....	82
KATA YA MWAMKULU.....	87
KATA YA NSEMULWA.....	92
KATA YA SHANWE.....	104
KATA YA UWANJA WA NDEGE.....	109

AGENDA ZA MKUTANO WA NNE WA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE 25.07.2018

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA  
MADIWANI
4. KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MKUTANO WA TATU WA  
BARAZA LA MADIWANI
5. TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KUTOKA KWENYE KATA
6. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI
7. KUFUNGA MKUTANO

**MUHTASARI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA  
KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA  
MPANDA TAREHE 25/04/2018**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1.	MHE.WILLIAM P. MBOGO	DIWANI KATA YA MAJENGO	MWENYEKITI
2.	NDG.MICHAEL F. NZYUNGU	MKURUGENZI WA MANISPAA	KATIBU
3.	MHE.KANONI LUCAS	DIWANI KATA YA SHANWE	MJUMBE
4.	MHE.MATONDO KANYEPO	DIWANI KATA YA MISUNKUMILO	"
5.	MHE.BAKARI KAPONA	DIWANI KATA YA NSEMULWA	"
6.	MHE.PHILIP J. KALYALYA	DIWANI KATA YA MAGAMBA	"
7.	MHE.CARITAS MANGWANGWA	DIWANI VITI MAALUM	"
8.	MHE.TOSIGWEGE MWAKYUSA	DIWANI KATA YA ILEMBO	"
9.	MHE.NURU A. MKANA	DIWANI VITI MAALUM	"
10	MHE.CHRISANT MWANAWIMA	DIWANI KATA YA KASOKOLA	"
11	MHE.EDILTRUDA M. KAMINDA	DIWANI VITI MAALUM	"
12	MHE.ELIAS MWANISAWA	DIWANI KATA YA KAZIMA	"
13	MHE.PIUS M. BUZUMALE	DIWANI KATA YA KAWAJENSE	"
14	MHE.STEPHANO A MWAKABAFU	DIWANI KATA YA UWANJA WA NDEGE	"
15	MHE.WILLIAM LIWALI	DIWANI KATA YA MPANDA HOTEL	"
16	MHE.ROSE J. KOMBA	DIWANI VITI MAALUM	"
17	MHE.GEOGINA S. KISALALA	DIWANI VITI MAALUM	"
18	MHE.KALIPI KATANI	DIWANI KATA YA MWAMKULU	"
19	MHE.RHODA MWAKALENGE	DIWANI VITI MAALUMU	"
20	MHE.HAIDARY SUMMRY	DIWANI KATA YA MAKANYAGIO	"

**WASIOHUDHURIA**

1.	MHE.SEBASTIAN KAPUFI	MBUNGE WA JIMBO LA MPANDA MJINI
2.	MHE.RHODA KUNCHELA	MBUNGE VITI MAALUM
3.	MHE.JOHN MATONGO	DIWANI KATA YA KASHAULILI

**WATAALAM WALIOKUWEPO**

1.	NDG.DEODATUS C. KANGU	MKUU WA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA
2.	NDG. SAID MANDUA	AFISA MAZINGIRA
3.	NDG .PASCHAL KWEYA	AFISA AFYA
4.	NDG. JOSHUA SANKALA	MRATIBU WA TASAF

5. NDG .ASUBISYE MWAG'ONDA	KAIMU MKUU WA IDARA KILIMO NA USHIRIKA
6. NDG .LUCAS NDOMBELE	MKUU WA IDARA YA FEDHA NA BIASHARA
7. NDG .OSWALD RWEZAULA	KAIMU MKUU WA KITENGO CHA UCHAGUZI
8. ENG.MOHAMED ULENGA	KAIMU MKUU WA IDARA YA UJENZI
9. NDG .RESPISTER KARUGENDO	MRATIBU WA TIKA
10. NDG .MARIETHA MLOZI	MKUU WA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII
11. NDG .MAGDALENA MKELEMI	MKUU WA IDARA YA MAJI
12. NDG .GEOFREY T. SIWEZI	KAIMU MKUU WA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI
13. NDG .GISBERT MSEMWA	KAIMU MKUU WA IDARA YA MIPANGO MIJI,ARDHI NA MALIASILI
14. NDG .PULKERIA J. MAKUNGU	AFISA USAFIRISHAJI
15. NDG .LUNYILIJIA KILINGA	KAIMU MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA
16. NDG .MARY A KANUMBA	MCHUMI
17. NDG .PHILIPO KAROL	MKUU KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI
18. NDG .MARY F. LUHULULA	MKUU WA IDARA YA MIPANGO ,SERA NA UFUATILIAJI
19. NDG .JOSEPHINE CHILLONGOZI	KAIMU MKUU WA KITENGO CHA SHERIA
20. NDG HOBOKELA MWAKAGAMBA	KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MANUNUZI
21. NDG .NOELI NKANA	AFISA BIASHARA
22. NDG .ALEX SEMWALI	MKUU WA USAFISHAJI NA MAZINGIRA
23. DR.OBED MAHENGE	MKUU WA IDARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII
24. NDG. JANE LUTEGO	KAIMU MKUU WA IDARA YA ELIMU MSINGI
25. NDG.BENSON NG'AMILO	KATIBU TSC
26. NDG.PIUS DONALD	AFISA HABARI
27. NDG.GILBERT BAYAGA	KAIMU KATIBU TAWALA WILAYA
28. NDG.EZEKIA BICHURO	AFISA TARAFI YA KASHAULILI

### **WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

1. NDG.ABELI KIMAZI	MWENYEKITI WA CCM WILAYA YA MPANDA
2. A/INSP. GEORGE	KAIMU MKUU WA POLISI WILAYA
3. A/INSP.ISRAEL KUTIKA	MKUU WA KIKOSI CHA ZIMA MOTO NA UOKOAJI WILAYA
4. A/INSP. OSWALD LUNGUYA	KAIMU MKUU WA MAGEREZA WILAYA
5. IC GODLISTEN PETER	KAIMU MKUU WA IDARA YA UHAMIAJI WILAYA
6. NDG.JOHN D. SALANGA	MTENDAJI KATA YA MAJENGO
7. NDG.MARY T. NGOMALUFU	MTENDAJI KATA YA KASHAULILI
8. NDG.DONALD KUSEKWA	MTENDAJI KATA YA MPANDA HOTEL
9. NDG. EMIL KATENDELE	MTENDAJI KATA YA ILEMBO
10.NDG. DEODATUS MASHAURI	MTENDAJI KATA YA KASOKOLA
11.NDG.JOHARI A. JUMA	MTENDAJI KATA YA MAGAMBA
12.NDG.ANNA G. KAPONDO	MTENDAJI KATA YA UWANJA WA NDEGE
13.NDG.REUBEN. W. KASOMO	MTENDAJI KATA YA KAKESE

14. NDG.MUSA KITEKA	KAIMU MTENDAJI KATA YA MAKANYAGIO
15. NDG.GEORGE ILESHA	MTENDAJI KATA YA MWAMKULU
16. NDG.RASHID MSYETE	KAIMU MTENDAJI KATA YA KAZIMA
17. NDG.REVOCATUS NGOMENI	MTENDAJI KATA YA NSEMULWA
18. NDG.ANGELO KATWANA	KAIMU MTENDAJI KATA YA KAWAJENSE
19. JANUARY KAYUNGILO	MTENDAJI KATA YA MISUNKUMILO
20. NDG.EMIL KATENDELE	MTENDAJI WA KATA YA ILEMBO
21. NDG.FULGENCE MKULILA	MTENDAJI WA KATA YA SHANWE
22. NDG.ARAM NDIMUBENYA	MWENYEKITI WA CHAMA CHA CUF WILAYA
23. NDG. CYRILVIVIANUS MSHYOTA	KATIBU WA ACT WAZALENDU WILAYA
24. NDG. RAFAEL B. SANGU	KATIBU WA CHAMA TLP
25. NDG. SAID R. KASHINDYE	MWENYEKITI WA CHAMA CHA UDP
26. NDG.ABRAHAM MAPUNDA	MWENYEKITI WA CHAMA CHA CHADEMA
27. NDG. ABDUL S. SIGERA	MWENYEKITI WA CHAMA CHA NCCR-MAGEUZI WILAYA
28. NDG.ADABUU JUMA	KATIBU WILAYA WA CHAMA CHA ADC
29. NDG.LINUS SIWEZI	KATIBU WA WILAYA WA CHAMA CHA UMD
30. NDG.FAUSTINE MWANAKATWE	KATIBU WA MBUNGE WA JIMBO LA MPANDA MJINI
31. NDG.ADOLPH MBATA	MWANDISHI WA HABARI –TBC
32. NDG.WINIFRIDA FIDELIS	MWANDISHI WA HABARI-PAMOJA FM
33. NDG.FATUMA AMASI	MWANDISHI WA HABARI- REDIO FREE AFRICA

### **SEKRETARIATI**

NDG.GALUS MAEMBE- KATIBU WA KAMATI

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:01: KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti, Katibu alitoa maelezo kuwa Mkutano ulikuwa wa **tatu** kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pia akidi ya wajumbe waliokuwa wanahitajika katika Mkutano huo ilikuwa inatosha kutoa maamuzi.

Baada ya utangulizi huo alimkaribisha Mwenyekiti ambaye kabla ya kufungua kikao alianza kwa kutoa shukurani kwa Madiwani, Wataalam na Wananchi wote kwa kuhudhuria kwenye Mkutano huo.

Mwenyekiti alifungua mkutano mnamo saa 4.32 Asubuhi.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:02: KURIDHIA AGENDA ZA MKUTANO**

Katibu alizisoma agenda zifuatazo;

- 1) KUFUNGUA KIKAO
- 2) KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO
- 3) KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA MADIWANI
- 4) KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA MADIWANI
- 5) TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KUTOKA KWENYE KATA
- 6) MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI
- 7) KUFUNGA MKUTANO

Baada ya kusomwa agenda hizo, mkutano uliridhia ziadiliwe.

**MUHT:MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:03: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA NNE WA BARAZA LA MADIWANI**

Muhtasari wa Mkutano wa pili wa baraza la madiwani ulisomwa na kuridhiwa na hivyo kutiwa saina kuwa kumbukumbu sahihi ya mkutano huo.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:04: KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MKUTANO ULIOPIITA**

Mkutano uliridhia utekelezaji wa maagizo ya mkutano uliopita.

**MUHT:MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:5:TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUTOKA KWENYE KATA.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wenyeviti wa vikao vya Maendeleo ya kata (WDC) kuwasilisha taarifa za kata ambapo kata ziliwasilisha taarifa za utekelezaji kama ifuatavyo;

Kasokola ,Kakese, Kazima, Majengo, Makanyagio, Shanwe, Uwanja wa Ndege, Nsemulwa, Kawajense,Kashaulili, Mwamkulu, Magamba, Ilembo, Misunkumilo na Mpanda Hotel.

Baada ya taarifa zote kujadiliwa, kikao kiazimia yafuatayo:-

**Azimio** :Gari la taka lipewe alama ya utambulisho

**Azimio:**Mkurugenzi aandike barua kwa Mkuu wa Wilaya ya kumshukuru/kutambua mchango wake katika kuhamasisha wadau wa Elimu.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:06: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Mwenyekiti aliagiza watendaji wa kata kuwasilisha taarifa mapema ili waandaji waweze kukamilisha makablasha kwa wakati.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:7: KUFUNGA MKUTANO**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika Mkutano. Alimkaribisha Mwenyekiti ambaye kabla ya kufunga Mkutano walizishukuru na kuzipongeza Kata ambazo ziliandaa taarifa vizuri.

Baada ya maelezo hayo aliwashukuru wajumbe na wananchi wote waliohudhuria Mkutano. Alifunga mkutano mnamo saa 7.48 Mchana.

**Umethibitishwa na kusainiwa na:-**

.....

.....

**KATIBU**

**MWENYEKITI**

**Jina.....**

**Jina.....**

**Tarehe.....**



**YATOKANAYO NA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE  
25.04.2018**

<b>AGENDA</b>	<b>AGIZO</b>	<b>MTEKELEZAJI</b>	<b>UTEKELEZAJI</b>
<b>MUHT:MMC/BARAZA/ 03/2017/2018:Agd:5</b>	Gari la taka lipewe alama ya Utambulisho	Mkurugenzi	Agizo limetekelezwa Gari la taka limeandikwa ubavuni
<b>MUHT:MMC/BARAZA/ 03/2017/2018:Agd:5</b>	Mkurugenzi aandike barua kwa Mkuu wa Wilaya ya kumshukuru/kutambua mchango wake katika kuhamasisha wadau wa elimu.	Mkurugenzi	Agizo limezingatiwa Barua ya kumshukuru Mhe.Mkuu wa Wilaya imeandikwa tarehe 23.07.2018 yenye KUMB.NA.KTV/MM C/E.30/8/15.

## KATA YA ILEMBO

### 1. A. UTANGULIZI

Kata ya Ilembo ni miongoni mwa Kata **15** zilizomo katika Halmashauri ya Manispaa Mpanda, katika Wilaya ya Mpanda Mkoani Katavi.

### B. MIPAKA YA KATA

Kata ya Ilembo imepakana na Kata zifuatazo:-

- i. Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Magamba
- ii. Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Misunkumilo
- iii. Upande wa Kaskazini imepakana na Kata ya Mpandahotel
- iv. Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Kapalala.

### C. MAENEO YA UTAWALA

Kata ya Ilembo ina mitaa **3**

(i) Mtaa wa Mapinduzi (ii) Mtaa wa Kasimba (iii) Mtaa wa Ilembo

### D. IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa sensa ya watu na maendeleo ya makazi ya mwaka **2012** kata ya Ilembo inajumla ya Kaya zenye Idadi ya watu kwa mchanganuo ufuatao:-

MITAA	KAY A	IDADI YA WATU			WENYE UWEZO			WASIO NA UWEZO			WALEMAVU		
		ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML
MAPINDUZI	<b>204</b>	522	540	<b>1062</b>	363	439	<b>802</b>	256	266	<b>522</b>	2	3	<b>5</b>
KASIMBA	<b>338</b>	519	604	<b>1123</b>	368	396	<b>764</b>	176	183	<b>359</b>	1	2	<b>3</b>
ILEMBO	<b>374</b>	548	612	<b>1160</b>	358	437	<b>795</b>	175	192	<b>367</b>	3	1	<b>4</b>
JUMLA	<b>916</b>	1607	1738	<b>3345</b>	1089	1272	<b>2361</b>	1249	641	<b>1248</b>	6	6	<b>12</b>

### E. SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Wananchi wakazi wa Kata hii wanafanya shughuli zifuatazo:-

- i. Wafanya biashara na wajasiriamali
- ii. Wakulima wadogo na wafugaji
- iii. Watumishi wa Serikali na wafanya kazi wa mashirika.
- iv. Wachimbaji wadogo wa madini mbalimbali.

### F. HUDUMA ZA KIJAMII

Kata ya Ilembo ina huduma za Kijamii kama zifuatazo:-

- (a) Shule za Msingi (i) S/M Mapinduzi (ii) S/M Ilembo
- (b) Shule za Sekondari (i) Kasimba Sekondari (ii) Sun Sekondari
- (c) Shule za Awali (i) Motherland (ii) Sumbilo
- (d) Ushauri na tiba (i) Kituo cha Afya Kasimba.

### G. HALI YA UONGOZI

Kata ya Ilembo ina viongozi wafuatao kwa nyazifa zao:-

- (i) Diwani wa Kata (ii) Afisa Mtendaji Kata (iii) Wenyeviti wa Mitaa
- (iv) Afisa Mtendaji Mtaa (v) Wataalam wa kada mbalimbali.

### H. IDADI YA WATUMISHI KILA IDARA

IKAMA	UTAWALA	SEKONDARI	MSINGI	KILIMO	AFYA	JAMII
MAHITAJI	4	35	30	2	2	1
WALIOPO	2	29	27	1	-	1
PUNGUFU	2	6	3	1	2	1

## **2.A. MPANGO SHIRIKISHI WA JAMII**

Ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo lazima kuwepo na malengo ya mpango shirikishi utakaoiongoza jamii kwa mchanganuo huu:-

- Kukusanya takwimu za mazingira, kitaalam, nyakati, kijamii na kiuchumi.
- Kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama; kupiga kura, vipaumbele kwa utashi na mlinganisho jozi.
- Kuweka malengo shabaha na kubuni mikakati ya ufumbuzi katika utekelezaji.
- Kupitisha na kuthibitisha rasmu ya mpango wa maendeleo katika utekelezaji.
- Kuweka taratibu za utekelezaji wa mpango kabambe ulio azimiwa na wananchi.
- Kufuatilia na kufanya tathimini ya mpango ulio kuwa umeandaliwa kwa maendeleo.
- Kuwepo na bajeti itakayoongoza utekelezaji wa mpango huu maalum.
- Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya utekelezaji wa mpango.

## **B. LENGU LA USHIRIKISHWAJI WA JAMII**

Lengu ni kuwataka wananchi waweze kutambua matatizo yanayowakabili na jinsi gani ya kutafuta umbuzi wake kwa kuhusisha makundi yote ya vikongwe, wazee, vijana na watoto ambapo makundi maalum kama yatima, walemavu, wajane, wagane na wanaoishi katika mazingira hatarishi watapewa kipaumbele kwanza.

## **C. UTAWALA BORA NA DEMOKRASIA**

Malengo ya utawala bora wananchi ndio chimbuko la mamlaka na madaraka ya Serikali **(i)** Katiba kushika hatamu **(ii)** utawala wa sheria **(iii)** usawa wa haki mbele ya sheria **(iv)** mgawanyo wa madaraka na majukumu **(v)** heshima kwa haki za binadamu na kuthamini utu wa mtu **(vi)** uwajibikaji wa wananchi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo **(vii)** ushiriki wa wananchi katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao **(viii)** maendeleo ya watu na kuondoa umasikini, ujinga na maradhi.

## **D. MISINGI YA UTAWALA BORA**

Mambo mhimu ya kuzingatia katika utawala bora

**(i)** Utawala wa kidemokrasia **(ii)** utawala wa kuzingatia sheria **(iii)** ushirikishwaji wa umma/Jamii **(iv)** haki na usawa wa watu wote **(v)** uwajibikaji katika utendaji wa kazi **(vi)** uwazi katika uendeshaji katika shughuli za maendeleo **(vii)** kuwepo uaminifu na maadili ya kazi **(viii)** kukidhi matakwa ya wananchi katika huduma.

## **E. UTOAJI WA HUDUMA BORA**

- Uimarishaji wa huduma za elimu, maji, afya na usafi wa mazingira.
- Ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya mawasiliano na uchukuzi.
- Ushauri wa kitaalam kwa wakulima, wafugaji, mafundi na wafanya biashara wadogo.
- Kurahisha utaratibu wa upatikanaji wa viwanja na hati za kumiliki ardhi.
- Kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao katika maeneo yote.

## **3A. MISINGI YA DEMOKRASIA**

- Ushirikishaji wa wananchi katika kupanga mipango ya maendeleo.
- Kujikomboa kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa maendeleo.
- Madaraka kwa umma na uhuru binafsi wa kuchangia mawazo.
- Uchaguzi huru na haki kwa kuzingatia haki za binadamu.
- Kukubali kujikosoa, kusoana, kukosolewa na kushauriwa bila upendeleo.
- Mgawanyo wa madaraka na majukumu ya utendaji kazi.
- Upendo, amani, utulivu na mshikamano wa Taifa letu.
- Kutumia nguvu za hoja na siyo hoja za nguvu katika majadiliano.
- Uvumilivu na staha kwa mitazamo na maoni tofauti ya kisiasa

- Kuheshimu, kusikiliza na kukubali mawazo ya walio wengi katika maazimio.

## **B. SIASA NA UONGOZI**

Katika utekelezaji wa kazi au shughuli mbalimbali za maendeleo ili ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa tunahitaji yafuatayo:-

- (i)** Siasa safi **(ii)** uongozi bora **(iii)** rasilimali ardhi  
**(iv)** rasilimali watu **(v)** rasilimali pesa

## **C. UHURU BINAFSI**

Uhuru binafsi ni pamoja na kila mtu katika Jamii kuzingatia yafuatayo:-

- (i)** Uhuru wa kwenda mahali popote **(ii)** uhuru wa kuchangia mawazo mbalimbali  
**(iii)** Uhuru wa kuishi mahali popote kisheria **(iv)** uhuru wa kuamini dini utakayopenda  
**(v)** uhuru wa kushirikiana na watu wengine **(vi)** uhuru wa kushiriki katika shughuli za maendeleo

## **4 A. VIASHIRIA VYA UMASIKINI**

- (i)** Kutokujua kusoma, kuhesabu na kuandika **(ii)** uhaba wa kupata chakula, mavazi na marazi  
**(iii)** Huduma duni za afya kinga na tiba **(iv)** vifo vingi vya wananchi kutokea  
**(v)** kuwepo na mda mfupi wa kuishi **(vi)** utapia mlo kwa watoto na watu wazima **(vii)** uchakavu wa mazingira yanayotuzunguka **(viii)** ukosefu wa ajira na kipato duni katika kaya **(ix)** kutofahamu maswala muhimu ya kijamii.

## **B. KUPUNGUZA UMASIKINI**

- Kuanzisha na kuimarisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji mali na biashara
- Kuhamasisha wananchi kujenga uwezo wa utamaduni wa kujiwekea akiba.
- Kuratibu, kujenga na kuboresha uwezo wa ufundi, maarifa na stadi za kazi ili kuongeza tija.
- Kuwaelimisha wananchi kutambua fursa zilizopo na kuwajengea uwezo wa kuzitumia.

## **C. MALENGO YA MILLENIA**

- (i)** Kuondoa umasikini ulio kithiri na njaa **(ii)** kutoa elimu ya msingi kwa wote  
**(iii)** kuendeleza usawa wa kijinsia (wanawake) **(iv)** kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5 **(v)** kuboresha afya ya uzazi salama (wajawazito) **(vi)** kupambana na VVU/ UKIMWI, Malaria na mengine **(vii)** kuboresha mazingira endelevu kwa vizazi vijavyo **(viii)** kuendeleza ushirikiano kwa maendeleo ya kimataifa.

## **5. VIKAO NA MIKUTANO**

Kwa kipindi cha miezi **3** April – Juni 2018 Kata hii imeendesha vikao vya kamati ya maendeleo **2** tarehe **5/4/2018** kikao maalum, tarehe **27/6/2018** ambapo mikutano ya hadhara ilifanyika tarehe **23/5/2018** Mtaa Ilembo, tarehe **24/6/2018** Mtaa Kasimba (Kawalyowa) na tarehe **29/6/2018** Mtaa Mapinduzi kuwahamasisha wananchi katika utekelezaji wa kazi za maendeleo.

- a. Ukarabati wa jengo la utawala katika shule ya Sekondari Kasimba.
- b. Ujenzi wa matundu **20** ya vyoo katika shule ya Msingi Ilembo.
- c. Ujenzi wa maabara katika kituo cha Afya Kasimba Mtaa wa Kasimba

- d. Ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- e. Ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- f. Ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- g. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- h. Ujenzi wa vyumba **2** vya madarasa katika shule ya Msingi Mapinduzi
- i. Utengenezaji wa madawati **78** katika shule ya Sekondari Kasimba.
- j. Kuwahamasisha wananchi kufanya usafi wa mazingira makazi na biashara.
- k. Kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi na kujenga uwezo wa kutekeleza majukumu.
- l. Kusoma taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya nne.

## **6. ILANI YA UCHAGUZI CCM YA MWAKA 2015**

- a. Kusimamia na kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- b. Kudumisha amani, Upendo, Utulivu na Mshikamano kwa maendeleo
- c. Kuendelea kuwahamasisha wananchi juu ya uwekezaji ili kukuza uchumi.
- d. Kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na maisha bora na mazuri.
- e. Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa unaohimili ushirika.
- f. Kuboresha sekta ya uzalishaji mali na huduma za kijamii.
- g. Kuimarisha miundombinu na huduma za kiuchumi.
- h. Kuendeleza Sera ya uwezeshaji wananchi kuinua kipato.
- i. Kuendelea kuboresha huduma za Elimu, Afya na Maji.
- j. Kusimamia utawala bora wa Sheria katika sekta zote.

## **7. HALI NA MWELEKEO WA KATA**

- a. Kuondoa migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji ili kudumisha amani.
- b. Kuimarisha ulinzi shirikishi wa jamii kwa maendeleo ya wananchi.
- c. Kukaguwa usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na Biashara.
- d. Kuendelea kuwabaini wageni wanaoingia na kutoka katika mitaani.
- e. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi.
- f. Kusimamia uundaji wa vikundi vya kiuchumi kati ya vijana / wanawake.
- g. Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya rushwa na madawa kulevya.
- h. Kuendesha vikao na mikutano ili kutatua matatizo yanayo wakabili wananchi.
- i. Kusimamia na kufuatilia utoaji wa chanjo zote zinazotolewa na wananchi.
- j. Kuhimiza matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na mifugo.
- k. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo na sheria mama
- l. Kudumisha Amani, utulivu, upendo na mshikamano.

### 8. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO JANUARI 2018 – MACHI 2018

Kwa Kipindi Cha Miezi 3 Kuanzia Mwezi April 2018 – Juni 2018 Kata ya Ilembo ilikusanya fedha na kupokea fedha

**Tshs. 61,536,260/=** kutoka michango ya wananchi. Nakutumia fedha **Tshs. 40,586,260** sawa **85%** Makadirio ya **72,585,000/=**

MTAA	AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			UTEKELEZAJI	MAELEZO
			TOLEWA	TUMIKA	BAKI		
KASIMBA	Ujenzi wa maabara katika kituo cha Afya	Halmashauri, wananchi	20,000,000/= 1,000,000/=	-	20,000,000/= 1,000,000/=	Ujenzi bado kuanza	Fedha za ujenzi zimetolewa
MAPINDUZI	Ujenzi wa madarasa 2. S/M Mapinduzi	"	500,000/= 400,000/=	500,000/= 400,000/=	-	Tofari 600 Mchanga 3 Mawe 3	Halmashauri itoe fedha ujenzi
ILEMBO	Ukarabati wa jengo la utawala Kasimba	"	15,000,000/=	15,000,000/=	-	Ukarabati umesimama	Tunasubili fedha ya kumaliza kazi
KASIMBA	Ujenzi wa kivuko cha mto kawalyowa	Mbunge wa jimbo	1,000,000/=	500,000/=	500,000/=	Kazi imesimama	Gari hafiki eneo la kivuko
ILEMBO	Ujenzi wa choo 20 S/M Ilembo	Mfuko wa jimbo Wananchi	4,000,000/= 1,000,000/=	4,000,000/= 1,000,000/=	-	Kazi inaendelea	Fedha ziongezwe
MAPINDUZI KASIMBA SEK. ILEMBO	Capitation	Ruzuku	212,340.78 6,244,542.00 2,313,558.00	212,340.78 6,244,542.00 2,313,558.00	- - -	Fedha zimetumika	Fedha haitosherezi mahitaji
MAPINDUZI ILEMBO KASIMBA	TASAF	Ruzuku	8,077,300/= (CCT&PWP)	8,077,300/= (CCT&PWP)	28,000/=	Walengwa walishalipwa	Mpango huu uendeleo
<b>JUMLA</b>			<b>61,536,260/=</b>	<b>40,586,260/=</b>	<b>21,000,000/=</b>	-	-

## 9. SEKTA YA AFYA KINGA

Kwa kuzingatia kanuni za Afya bora kila mtu ameelekezwa yafuatayo:-

- Kuwaelimisha wananchi juu ya ujenzi wa vyoo bora vinavyotumia maji.
- Kuwahamasisha wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao.
- Kuendelea kuwaelimisha wananchi kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF.
- Kuwahamasisha walengwa wa TASAF kujiunga na Tika katika matibabu
- Kuwaelimisha mama lishe kufuata kanuni na sheria za Afya katika shughuli zao.

## 10. SEKTA YA AFYA TIBA

Kata ya Ilembo ina kituo cha Afya Kasimba kinachoendelea kutoa huduma kwa wananchi wa Kata hii. Japokuwa kina kabiliwa na upungufu wa wataalam, vitendea kazi, majengo na samani.

## 11. SEKTA YA MAJI

Kata hii inakabiliwa na tatizo la Maji kwa kiasi kikubwa kwa kuwa maji toka Ikolongo yanapatikana mara **3** kwa wiki katika Mtaa wa Ilembo ambapo Mtaa wa Mapinduzi hakuna maji kabisa. Aidha visima **2** kilichopo S/M Mapinduzi na S/M Ilembo vyote vilishaharibika. Hivyo tunaomba mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira watengeneze visima ili viweze kutoa hudumma kwa wananchi.

## 12. SEKTA YA UTAWALA

- kusimamia na kuimarisha ulinzi shirikishi jamii wa raia na mali zao.
- Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo
- Kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa wataalamu wote
- Kusimamia utawala bora kwa kuzingatia sheria zilizopo
- Kusimamia n kushiriki katika zoezi la usafi wa mazingira
- Kusimamia na kudhibiti utoro na mimba kwa wanafunzi shuleni
- Kusimamia utendeshaji wa vikao vya ndani na mikutano ya hadhara
- Kusuluhisha na kutatua migogoro mbalimbali inayojitokeza.

## 13. SEKTA YA UJENZI WA NYUMBA BORA

Wananchi wameshauriwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kuwepo vyumba vikubwa vyenye nafasi ya kutosha
- Kuwepo ramani ya mchoro wa nyumba
- Kuwepo kibali cha kujenga nyumba
- Kuwepo matofari ya kuchomwa na kuezeka bati
- Kuwepo choo cha kudumu na maji safi kinachotumika
- Kuwepo madirisha makubwa ya kuingiza mwanga na hewa.

## 14. SEKTA YA ELIMU S/M NA SEKONDARI

(i) **Kata hii ina shule 3 ambapo 2 S/M na 1 Shule ya Sekondari.**

SHULE	AWALI			WALIMU			WANAFUNZI		
	MH	WP	PF	MH	WP	PF	MH	WP	PF
Ilembo	274	140	134	22	17	5	874	778	96
Mapinduzi	61	32	29	13	10	3	268	237	31
Sek-Kasimba	-	-	-	32	26	6	804	722	82
<b>Jumla</b>	<b>335</b>	<b>172</b>	<b>163</b>	<b>67</b>	<b>53</b>	<b>14</b>	<b>1946</b>	<b>1737</b>	<b>209</b>

**(ii) Takwimu halisi ya miundombinu ya shule S/M & Seki**

SHULE	MADARASA			NYUMBA			VYOO		
	HT	YP	PF	HT	YP	PF	HT	YP	PF
Mapinduzi	10	5	5	10	1	9	14	8	6
Ilembo S/M	19	7	12	17	1	16	36	18	18
Kasimba Sek	20	12	8	26	3	23	39	18	21
<b>Jumla</b>	<b>49</b>	<b>24</b>	<b>25</b>	<b>53</b>	<b>5</b>	<b>48</b>	<b>89</b>	<b>44</b>	<b>45</b>

**(iii) Matokeo ya wanafunzi Kasimba Sekondari walifanya mtihani kidato II-2017**

SHULE	WALIOSAJILIWA			WALIOTAHINIWA			WASIOFANYA			WALIOFAULU			WALIOFELI		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML
Kasimba Sek	<b>90</b>	<b>113</b>	<b>203</b>	<b>85</b>	<b>107</b>	<b>192</b>	<b>5</b>	<b>6</b>	<b>11</b>	<b>80</b>	<b>84</b>	<b>164</b>	<b>9</b>	<b>19</b>	<b>28</b>

**(iv) Matokeo ya wanafunzi waliofanya mtihani kidato IV Kasimba 2017**

SHULE	WALIOSAJILIWA			WALIOTAHINIWA A			WASIOFANYA			WALIOFAULU			WALIOFELI		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML
<b>Kasimba Sek</b>	<b>39</b>	<b>30</b>	<b>69</b>	<b>39</b>	<b>29</b>	<b>68</b>	<b>0</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>30</b>	<b>23</b>	<b>53</b>	<b>9</b>	<b>6</b>	<b>15</b>



## 15. SEKTA YA MAENDELEO JAMII

Kata hii ina vikundi vya wajasiria mali **8** kama:-

(i) Morning Star (ii) Twikalane Group (iii) Jionee group (iv) Muungano (v) Development Front line (vi) Alfa Group (vii) Vijana group (viii) Change Revolution ambao bado wanadaiwa kurejesha mkopo. Aidha shughuli zilizofanyika katika idara hii ni pamoja na :-

- a. Kuendelea kuwahamasisha wananchi kuunda vikundi na kusajili.
- b. Kuratibu na kutoa elimu juu ya uendeshaji wa miradi.
- c. Kusimamia uibuaji wa miradi ya kilimo na mifugo.
- d. Kuendelea kutoa elimu juu ya kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.
- e. Kutoa Elimu ya kudhibiti mimba za utotoni kwa wanafunzi.
- f. Kufuatilia urejeshaji wa mikopo ya fedha kwa vikundi.
- g. Kutembelea vikundi na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo.
- h. Kusimamia ugawaji wa malipo wa kaya masikini TASAF.
- i. Kushiriki katika mafunzo ya mradi wa kizazi kipya.
- j. Kushiriki vikao vya kamati na kuhudhuria mikutano ya hadhara.

## 16. SEKTA YA UTUNZAJI MAZINGIRA

Kwa kipindi hiki kazi zilizofanyika ni pamoja na

- a. Kuwahamasisha wananchi kutunza vyanzo vya maji.
- b. Kuendelea kutoa elimu juu ya ufugaji wa kutumia zizi.
- c. Kuwashauri wafugaji kuupunguza idadi ya mifugo yao.
- d. Kutoa elimu juu ya wafugaji kudhibiti uzurulaji wa mifugo.
- e. Kufanya maandalizi ya vitalu vya miti na kupanda baadaye.
- f. Wafyatuaji wa matofari kupata vibali na kuchangia tofari.
- g. Kutunza mapori yasichomwe moto wala kuharibiwa.

## 17A. SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO

Katika sekta kilimo, mifugo na ushirika kazi zilizofanyika ni pamoja na

- a. Kutoa elimu kwa wafugaji wa kuku jinsi ya kudhibiti magonjwa
- b. Kuwahamasisha wakulima juu ya kulima mazao ya kinga ya njaa viazi na mhogo.
- c. Kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mahindi kutoka gunia 15 hadi 20 kwa ekari
- d. Shamba darasa na shamba la mfano kwa kuwafundisha wakulima
- e. Kutoa chanjo ya kichaa cha mbwa kwa idadi ya mbwa 8
- f. Kuwatembelea wakulima wa zao la korosho na kutoa maelekezo juu ya kilimo hicho.
- g. Kuwaandaa wananchi kuwa tayari kuanza maandalizi ya kulima mashamba.
- h. Wakulima **76** na wafugaji **13** wamepata elimu ya kilimo bora na ufugaji bora.
- i. Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa vikundi vya wakulima na wafugaji
- j. Kuwahamasisha wafugaji wa mbwa kuwapeleka mbwa wao kupata chanjo.
- k. Kuwasisitiza wananchi kuzingatia kanuni za kilimo bora na kujali muda wa kazi.
- l. Kutoa maelekezo juu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na mifugo.
- m. Kuwepo shamba darasa linalotumika kuwafundisha wananchi wakulima
- n. Kupiga chapa ng'ombe **704** za wafugaji **18**.

## B. IDADI YA MIFUGO KATIKA KATA

AINA YA MIFUGO	ASILI	KISASA	JUMLA
Ng'ombe	1220	8	<b>1228</b>
Mbuzi	378	0	<b>378</b>
Kondoo	44	0	<b>44</b>

Nguruwe	216	0	<b>216</b>
Mbwa	104	0	<b>104</b>
Kuku	14,087	183	<b>14,270</b>
Punda	1	0	<b>1</b>
Bata	276	0	<b>276</b>
Njiwa	101	0	<b>101</b>
Kanga	13	0	<b>13</b>
Sungura	4	0	<b>4</b>
Paka	6	0	<b>6</b>
<b>JUMLA</b>	<b>16,464</b>	<b>191</b>	<b>16,655</b>

## 18. DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2015 – 2025

- Kuimarisha mshikamano, amani na utulivu kwa maendeleo
- Kuimarisha uchumi imara unaohimili ushindani
- Kuondoa umaskini uliokithiri katika maisha ya kila siku
- Kuwa jamii iliyoelimika na inayohitaji kujifunza zaidi
- Kupunguza tofauti ya kipato kati ya walionacho na wasiokuwanacho
- Kuwa na maisha bora na mazuri yenye Afya kwa nguvu kazi
- Kuimarisha utawala bora wa sheria katika jamii kwa kuzingatia
  - Usawa kwa raia
  - ii) Uwazi na uwajibikaji
  - iii) Ugatuuji wa madaraka
  - iv) Haki stahiki ya ushiriki

## 19. SEKTA YA KATIBA NA SHERIA

Kwa mujibu wa sheria **Na 7/1985** ya uundwaji wa baraza la kata nchini Tanzania baraza la Kata la Ilembo kwa kipindi cha miezi 3 April – Juni 2018 baraza limepokea idadi ya kesi zifuatazo:-

- 6/4/2018 baraza lilipokea mgogoro wa kuuza kiwanja bila makubaliano
- 27/4/2018 baraza la Kata lilipokea kesi ya madai ya pesa
- 13/5/2018 baraza la Kata lilipokea kesi ya kutoa lugha chafu ya matusi
- 22/6/2018 baraza la Kata lilipokea mgogoro wa ndoa kati ya mume na mke
- 23/6/2018 baraza la Kata lilipokea kesi ya madai ya mbao za ujenzi
- 25/6/2018 baraza la Kata lilipokea kesi ya mgogoro wa kifamilia (Ukoo)

Aidha kesi nne zilishatolewa uamuzi na kesi mbili bado zinaendelea baraza la Kata.

## 20. SEKTA YA ULINZI NA USALAMA

Katika kutekeleza suala la ulinzi na usalama wa raia na mali zao Kata ya Ilembo tumefanya vikao **2** vya kamati ya ulinzi na usalama na kuendesha mikutano ya hadhara **3** kuwahamasisha wananchi kushiriki ulinzi shirikishi Jamii kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Kuwepo daftari la mahudhurio kazini na kusaini wakati wa kuanza ulinzi usiku.
- Kuwepo na vitendea kazi filimbi, tochi, virungu na vitambulisho vya kazi.
- Kutoa taarifa za siri kulingana na mazingira yanayopelekea uharifu mitaani.
- Kupanga eneo la kufanyia kazi kwa kila siku kwa kuzingatia ratiba ya kazi
- Kutoa taarifa za matukio yanayojitokeza wakati wote usiku na mchana.
- Kuwepo na sehemu maalum ya kukutana ili kuanza kazi ya ulinzi.
- Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa ndiye msimamizi mkuu wa kikundi cha ulinzi.

## 21. SEKTA YA UKIMWI

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 kazi zilizofanyika katika sekta hii ni pamoja na

- Kuendesha vikao vya ndani na nje katika kuwahamasisha wananchi kupima afya.
- CBHS Kuwatembelea wagonjwa majumbani kujua afya zao zinavyoendelea.
- Kutoa elimu juu ya kuingia familia zao zilizoko katika mazingira hatari.
- Kuhamasisha na kutoa elimu juu ya upimaji wa hiari katika kituo cha Afya.
- Kufuatilia walengwa (WAVIU) walioacha dawa na kuwarudisha CTC.

## **22A. PONGEZI ZA DHATI**

Uongozi wa Kata ya Ilembo unatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya awamu ya 5 kwa kutoa fedha za ujenzi wa miradi ya maendeleo kiasi cha **Tshs. 720,000,000/=** (Milioni mia saba ishirini) ambapo **Tshs. 320,000,000/=** kwa ajili ya kununua vifaa tiba na **Tshs. 400,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa miradi katika kituo cha Afya Kasimba kilichopo Kata ya Ilembo kama ifuatavyo:-

- a. Ujenzi wa maabara katika kituo cha Afya Kasimba Mtaa wa Kasimba
- b. Ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- c. Ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- d. Ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)
- e. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi kituo cha Afya Kasimba (Ilembo)

### **B. CHANGAMOTO**

- a. Upungufu wa madawati **78** katika Shule ya Sekondari Kasimba
- b. Upungufu wa watumishi wa idara ya Afya na utawala
- c. Upungufu wa vyumba vya madarasa katika S/M na Sekondari
- d. Kushamili kwa vibaka na wezi mitaani kunatokana na mapagala na viwanja kutoendelez ujenzi.

### **C. MAPENDEKEZO**

- Halmashauri ya Manispaa Mpanda iwanyang'anye wamiliki wa mapagala na viwanja ambao hawataki kuendeleza majengo yao.

### **Naomba kuwasilisha**

MHE. TOSIGWEGE MWAKYUSA  
**DIWANI WA KATA YA ILEMBO**

## **KATA YA KAKESE**

### **TAARIFA YA KAZI KWA KATA YA KAKESE KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (4) 2017/2018**

#### **UTANGULIZI.**

Kata ya Kakese ni miongoni mwa Kta 15 zinazounda Halmashauri ya Manispaa Mpanda, Tarafa ya Misunkumilo, Wilaya ya Mpanda.

Kata ya kakese inajumla ya vijiji (4) ambavyo ni

1. Kijiji cha Mbugani
2. Kijiji cha Kakese
3. kijiji cha Kawanzige
4. Kijiji cha Kamakuka

Pia kata ya kakese ina vitongoji kumi na nane (18) tu.

ambavyo ni:-

❖ Kijiji cha Mbugani -

1. Kitongoji cha Mbugani "A" Mashariki
2. Kitongoji cha Mbugani "B" Mashariki
3. Kitongoji cha Mbugani "B" Magharibi
4. Kitongoji cha Mwangoye
5. Kitongoji cha Maluja

❖ Kijiji cha Kakese

1. Kitongoji cha Mkwajuni
2. Kitongoji cha Makanisani
3. Kitongoji cha Kalofesi "B"
4. - Kitongoji cha Kakese "A"

❖ Kijiji cha Kawanzige

1. Kitongoji cha kawanzige "A"
2. Kitongoji cha Bulima
3. Kitongoji cha Mabanini
4. Kitongoji cha Jitegemee
5. Kitongoji cha Mwembeni

❖ Kijiji cha Kamakuka

1. Kitongoji cha Kamakuka "A"
2. Kitongoji cha Kamakuka "B"
3. Kitongoji cha Ipwaga
4. Kitongoji cha Isengule

#### **WATU NA MAKAZI**

Kata ya Kakese inajumla ya kaya 2577 na watu wapatao **14083, ke 7087** na **me 6988**; Takwimu hii ni ya sensa ya Taifa ya watu na makazi ya 2012

#### **SHUGHULI ZA WAKAZI WA KATA YA KAKESE NI**

- (a) Kilimo
- (b) Ufugaji
- (c) Biashara na ujasiliamali

(d) Uchimbaji mdogo wa madini

### **UONGOZI /UTAWALA/SIASA**

Kata ya kakese ina viongozi wa kuchaguliwa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Diwani wa kata mmoja (1)
2. Wenyeviti wa vijiji wanne (4)
3. Wenyeviti wa vitongoji (18) kumi na nane
4. Wajumbe wa Halmashauri ya kijiji (78) sabini na nane.

Viongozi hao kwa pamoja wanatokana na vyama vya siasa viwili CCM na CHADEMA.

### **WATAALAMU**

Kata ya kakese kwa sasa ina wataalamu wafuatao wanaotekeleza majukumu yao ya kiserikali.

<b>NO</b>	<b>CHEO/NAFASI</b>	<b>NGAZI</b>	<b>NO.</b>	<b>IDARA</b>	<b>ENEO LA KAZI</b>
	MTENDAJI KATA - KAKESE	KATA	1	UTAWALA	KAKESE
1.	AFISA AFYA	KATA	1	AFYA	KAKESE
2.	AFISA MAENDELEO	KATA	1	MAENDELEO JAMII	KAKESE
3.	AFISA UMWAGILIAJI	KATA	1	UMWAGILIAJI	KAKESE
4.	AFISA KILIMO	KATA	1	KILIMO	KAKESE
5.	AFISA MIFUGO	KATA	1	MIFUGO/UVUVI	KAKESE
6.	AFISA ZANA ZA KILIMO	KATA	1	KILIMO	KAKESE
7.	MRATIBU KATA	KATA	1	ELIMU	KAKESE
8.	ASKARI KATA	KATA	1	POLISI	KAKESE
9.	AFISA KILIMO	KIJIJI	1	KILIMO	KAKESE
10.	WATENDAJI	VIJJI	3	UTAWALA	KAKESE
11.	WALIMU SHULE ZA MSINGI	VIJJI	68	ELIMU	KAKESE

### **VIKAO NA MIKUTANO**

Ili kutekeleza shughuli za serikali kwa kipindi cha April hadi June 2017/2018 kata imekaa vikao kama ifuatavyo:-

<b>NO</b>	<b>VIKAO VYA KATA</b>	<b>KIKAO CHA KAWAIDA</b>	<b>KIKAO CHA DHARULA</b>	<b>TAREHE YA KIKAO</b>
1.	KAMATI YA ULINZI NA USALAMA	1	2	24/5/2018
2.	KAMATI YA VVU	1	1	03/07/2018
3.	KAMATI YA MALALAMIKO	1	2	27/06/2018
4.	KAMATI YA UJENZI/MAZINGIRA	1	3	03/07/2018
5.	KIKAO CHA MAENDELEO CHA KATA	1	2	05/07/2018
6.	MIKUTANO YA HADHARA	1	0	13/06/2018

## UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Kwa kipindi cha miezi mitatu ya robo ya nne (4) ya mwaka wa fedha 2017/2018 shughuli mbalimbali za maendeleo zimetokelezwa kama ifuatavyo:-

### KILIMO

Kufanya vikao viwili (2) kati ya chama cha Wakulima (kambui) na wataalamu toka shirika la SNV na wataalamu wa bonde la Ziwa Rukwa ili kujadili shughuli za kilimo na umwagiliaji kata ya Kakese na kata ya Itenka. Kutoa Elimu kwa wakulima dhidi ya kuandaa mavuno na kuifadhi mazao yao kwa chakula na biashara katika maghara kama vile Karanga, Mahindi, Mpunga, Mihogo na Viazi. pia kuendelea kutoa Elimu kwa wakulima wa zao la korosho kutunza vizuri zao hilo kwa msimu huu wa kiangazi, ambapo jumla ya wakulima 13 wamejitokeza kulima zao hilo sawa na hekta 14.

Kuhamasisha wananchi kwa njia ya vikao na mikutano ya hadhara kulima kilimo bora cha Mpunga badala ya kulima kilimo holela na cha mazowea.

Mfano:- katika kata yetu mtaalamu wa umwagiliaji aliunda kikundi na kuanzisha shamba la mfano baada yawakulima hao kwenda kupata Elimu Mkoani Morogoro kwa ufadhili wa shirika la SNV

Kupitia Elimu ya shamba hilo la mfano makisio ya mavuno katika shamba hilo ilikuwa kuvuna Gunia 35/40 kwa ekali moja, mavuno halali yamekuwa gunia 31 kwa ekali tofauti na mashamba ya kawaida ya wakulima yametoa Gunia 8 hadi 20 kwa mavuno ya juu zaidi.

Kwa msimu huu wa mavuno upatikanaji wa mavuno ni wa wastani. Hii inatokana na changamoto iliyojitokeza ya kuwa na mvua nyingi zilizopelekea mafuriko kwenye mashamba na kuoza mazao.

### MIFUGO

Ili kuimalisha secta ya kilimo na mifugo na kuwa na takwimu sahihi kwa kipindi hiki wataalamu wamefanya sensa ya mifugo kama ifuatavyo:-

NO	JINA LA KIJIKI	NG'OMBE	MBUZI	KONDOO	NGURUWE	KUKU	BATA	MBWA	PUNDA
1.	MBUGANI	4012	1068	128	45	4660	1398	267	20
2.	KAWANZIGE	1495	677	167	85	5850	850	180	2
3.	KAMAKUKA	198	212	40	7	1120	65	75	-
4.	KAKESE	1209	758	15	59	3420	203	102	-
	<b>JUMLA</b>	6914	2715	350	196	15050	2516	624	22

Jumla ya mifugo iliyochinjwa katika machinjio ya kata na kusimamiwa na Afisa Mifugo wa Kata ya Kakese.

AINA YA MFUGO	IDADI YA ILIYOCHINJWA	BEI KWA KILO	USHURU
NG'OMBE	117	Tsh. 5,000/=	0
MBUZI	98	Tsh. 7,000/=	0
NGURUWE	15	Tsh. 6,000/=	0
KUKU	6561	Tsh. 10,000/=	0

Mifugo tajwa hapo juu pia hutoa mazao yafuatayo endapo yatatumika ipasavyo:-

ZAO	MATUMIZI	MAONI
-----	----------	-------

NGOZI YA NG'OMBE	VIWANDA	Ngozi zote zinatupwa kukosa soko
NGOZI YA MBUZI	VIWANDA	Ngozi zinatupwa kukosa soko
MAZIWA	CHAKULA	Yanauzwa kwa matumizi nyumbani
MBOLEA	MBOLEA	Kutumika kiasi shambani

### Changamoto katika mifugo na kilimo

1. Secta ya mifugo paoja na kuwa na kundi kubwa la wau wanaotegemea kwa kipato, kuna tatiyo la mlipuko wa magonjwa hasa kwa:-

Kuku, mbwa, na ng'ombe, Nguruwe, mbuzi

↓	↓	↓	↓	↓
New			Warm	Warm
Castec		-Trypanosemiasis		
Castec		-Gast cost		
Fouct cholera		-fever		
		-veicular		
		Stomastitis		
		-Anaplasimols		

2. Eneo la malisho pia ni changamoto kwa mifugo katika eneo lefu na zaidi Gombe
3. Soko la kuuza mazao ya mifugo mfano ngozi, kwato, pembe na maziwa.
4. Ukosefu wa machinjio nzuri na JOSHO
5. wataalamu hawana vifaa vya kutolea huduma katika karatibu na kufundishia kwa mifugo na mazao.
6. Soko la kuuza mpunga na mchele bado ni tatizo kwani wakulima wanapouza wanunuzi wanawafuata katika kaya zao, hivyo kutoleta ushindani wa bei
7. Upatikanaji wa dawa za mifugo na mazao ya mashambani bado ni tatizo na kupelekea watu wengi kuuziwa dawa bandia na zisizotibu magonjwa husika

### **MAJI.**

Kwa kipindi cha robo hii ya nne 2017/2018 huduma ya maji safi na salama imekuwa ya wastani katika kaya na makazi.

1. Serikali kupitia mamalaka ya maji safi na maji taka mpanda-imechimba kisima kimoja kutoka kitongoji cha kakese' A' Sekondari na hatua iliyobaki ni kufunga pampu. Tunaomba pampu hiyo ifungwe ili huduma ianze kupatikana
2. Huduma hiyo inategemewa pia katika kijiji cha kamakuka na kawanzige ambapo wataalamu walishindwa kuchimba visima hivyo kwa sababu ya barabara ya kufika maeneo hayo kuwa mbaya.
3. Maeneo mengine yenye uhitaji ni eneo la mabanini, Kalofesi B, mahuja na mbugani magharibi
4. Wananchi wanahimizwa kuendelea kutunza vyanzo vya maji, moto, mabonde na mabwawa yanayochimbwa na mradi wa Tasafu.

### **AFYA.**

1. Kwa kipindi hicho, serikali za vijiji na kata tumeendelea kushirikiana kuhamasisha jamii kutunza mazingira, kufanya usafi katika kaya, maeneo ya biashara, maeneo ya wazi na katika Taasisi
2. Serikali imeendelea kutoa chanjo za watoto chini ya miaka 5 zahanati na mashuleni chanjo ya kichocho na minyoo
3. Serikali imeendelea kuratibu maduka ya dawa za binadamu kwa kuwatambua wamiliki na kuhakikisha wanavibali na kuuza dawa stahili.

4. Serikali imesimamia na kuzuia milipuko ya magonjwa ya kuambukiza kwa kusimamia usafi,na kutoa Elimu ya mbinu za kujikinga na kuzuwia mazaria ya vimelea vya magonjwa hayo.
5. Ukimwi na magonjwa sugu vimeendelea kuratibiwa na serikali kupitia kamati ya maendeleo ya kata,vijiji,mikutano na kuunda mikakati ya kuwatembelea makundi yaliyo katika mazingira hatarishi ili kutoa Elimu ya kujikinga na walioathirika watumie dawa za ARV katika vituo vya Afya na zahanati,hii ni pamoja na Elimu kwa magonjwa sugu.

#### **ELIMU NA UFUNDI**

#### **KATIKA SECTOR HII,SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NI KAMA IFUATAVYO:-**

1. Kusimamia ujenzi na ukamilishaji wa jengo la S/m kawanzige madarasa mawili na ofisi moja  
NB.Tunaishikuru halmashauri kwa kutoa fedha ya ukamilishaji huo kupitia P4R tsh 17,500,000/= ujenzi umekemilika na jengo linatumika.
2. Kuanzisha ujenzi wa madarasa mapya mawili ya shule ya msingi kawanzige kwa nguvu za wananchi ambapo mradi upo hatua ya msingi kwa sasa.
3. Kuanzisha mradi na ujenzi wa madarasa mapya mawili shule ya sekondari kakese kwa nguvu za wananchi.kwa sasa mradi upo hatua ya kukamilisha msingi.
4. Kusimamia kuundwa kwa kamati mpya za shule za msingi kwa kata ya kakese baada ya zilizokuwepo kumaliza muda wake.
5. Kusimamia na kuratibu shughuli za ufundishaji malezi kwa wanafunzi na kuzuia utoro sugu na wa lejaleja kwa shule zote za msingi kupitia kamati za shule na serikali za vijiji.

#### **ARDHI MAZINGIRA NA NYUMBA:-**

Katika kuboresha na kuhifadhi mazingira kwa robo ya nne(4)ya 2017/2018,shughuli zifuatazo zimetetelezwa.

1. Kuhamasisha jamii kupitia mikutano na vikao vya kamati kuifadhi mazingira ya vyanzo vya maji, misitu na mito.
2. Kutunza mashamba ya miti iliyopandwa kupitia mradi wa Tasafu kwa kaya maskini pamoja na kuhifadhi mabwawa.
3. Kuhimiza ujenzi na nyumba bora na ufyatuaaji tofali kwa kuendelea kuhifadhi mazingira
4. Kuratibu na kusimaia migogoro ya mashamba,mipaka na maeneo ya malisho na njia za mifuko kwa wakulima na wafugaji.

#### **UJENZI,MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

Kwa robo ya nne(4) ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa zifuatazo zimetetelezwa.

1. Kuhimiza wananchi kushiriki katika ujenzi na uhifadhi na ulinzi wa miundombinu ya barabara,madaraja,vivuko,mitandao,njia za mifugo na ujenzi maeneo yaliyo salama.
2. Pamoja na ushiriki huo safar hii imekuwa na changamoto kubwa zifuatazo:-
  - a. Tatizo la kuchakaa,na kuharibika kwa miundombinu ya barabara na karavati kwa maeneo yote ya kata kufuatia mvua kubwa zilizonyesha kwa msimu huu Hali hiyo imechangia kuwepo kwa ajali za mara kwa mara,bidha kupanda bei,nauli kupanda mara kwa mara na bei ya mazo kuwa chini zaidi.



- b. Kumekuwa na tatizo kubwa la wizi kwa njia ya mtandao na mawasiliano; ambapo baadhi ya watu wanatumia mawasiliano yasimu kuwadanganya wananchi kuwa wameshinda promesheni flani, bahati nasibu, zawadi kutoa dawa za biashara, uzazi, mapenzi, wanafunzi kupata ajali au magonjwa ya ghafla hasa waliopo masomoni, kutoa kazi na kufanya miamara ya fedha au biashara na vitisho.

NB. Tunaomba serikal kuingilia kati tatizo hili ili kuwasaidia wannachi wanaohangaika na janga hili kwa kuzuwia wizi huo.

### **KAZI ,AJIRA,VIJANA NA WALEMAVU**

- Kwa kipindi hiki cha robo ya nne(4) ya 2017/2018 kwa eneo letu, ni msimu wa mavuno na biashara. Hivyo wananchi wengi kutoka mikoa mbalimbali wamekuwepo na kuajiliwa kwa kazi za muda mfupi za mavuno ya mashamba hususani katika mashamba ya mpunga na kuongeza kipato kwa wananchi.

### **VIWANDA,BIASHARA NA MASOKO**

kwa robo hii ya nne (4) kata na vijiji, tumeendelea kuratibu shughuli za viwanda ,biashara na masoko kwa kutekeleza yafuatayo:-

1. Kufanya sensa na kutengeneza daftari la mchanganuo na biashara, viwanda na masoko yaliyopo katika maeneo yetu. ili kuwatambua na kuwasaidia.
2. Kufanya vikao na mikutano na wafanyabiashara ili kubaini fursa kero na changamoo wanazokumbana nazo na kuwa fursa au vikwazo kwa kazi zao.

**NB:** Katika kikao cha tar 09/07/2018 cha wafanyabiashara wote wa kata ya kakese wameomba kushughulikiwa yafuatayo.

1. Kutatuliwa changamoto ya tatizo la barabara
2. Kuboresha mnada wa kakee na soko la kakese mbugani kwa kufungua barabara ya kakese, itenka na kakese mwamkulu ili kuongeza mapato.
3. Wameomba kikao cha pamoja kati ya maafisa biashara maafisa mapato na T.R.A ili waweze kutambua majukumu ya sector hizo tatu na kuboresha biashara zao kwa kulipa mapato.

### **KERO NA MALALAMIKO:**

1. Kwa robo ya nne(4) ya 2017/2018 kata imeendelea kuratibu migogoro na mahusiano mema ya wananchi kwa kupokea kero za wananchi na kuzitatua kupita vikao na mikutano ambapo Jumla ya kero 7 zimepokelewa na kutatuliwa
  2. Jumla ya migogoro (3) mitatu imepokelewa na kutatuliwa
  3. Kamati ya kero na malalamiko imeborehswa kwa kuunda kamati mpya baada ya iliyokuwepo kumaliza muda wake
- Ambapo kamati ina wajumbe watano
    1. M/kiti –Reuben kasomo-WE0
    2. Katibu-MICHAELI SHABANI –CDO
    3. Khadija mlimbaji –mjumbe
    4. Asumani midule- mjumbe
    5. Joseph kalyalya –mjumbe

### **MAPATO NA MATUMIZI**

Taarifa ya mapato na matumizi kata ya kakese kwa kipindi cha robo ya nne (4)2017/2018

### **Utangulizi:**

Kata ya Kakese inajumla ya vijiji vine (4) na vitongoji kumi na nane. kata ina jumla ya kaya 2577 na wakazi wapatao 14083 ambapo Me=6988 na Ke=7095.

**Malengo:**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, kata ilikisia kukusanya, kupokea na kutumia kiasi cha Tsh. 56288,522.6 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ya kata

**Mapato:**

Kwa kipindi cha April hadi June kata imekusanya na imepokea kiasi cha 44,746,200/= toka serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake za maendeleo na malipo kwa kaya maskini.

**Matumizi:**

Kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2017 kata imetumia kiasi cha 48,746,200/= kutoka kutekeleza miradi ya maendeleo ndani ya kata

**SALIO:**

Kwa kipindi hicho kata imebaki na salio la ts 3,000,000/= million tatu

Naomba kuwasilisha

**Mh, Magaga Salagada**  
**DIWANI KATA YA KAKESE**

## KATA YA KASHAULILI

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA APRIL HADI JUNI 2018 KATA YA KASHAULILI.

### UTANGULIZI.

Kata ya Kashaulili ni miongoni nwa Kata tisa (9) zilizomo Tarafa ya Kashaulili Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi.

Kata ya Kashaulili inajumla ya wakazi wapatao **8546** wakiwemo wanaume **3858** na wanawake **4688** kaya **1016**.

KATA	IDADI YA WATU WOTE			WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI			WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI			WALEMAVU			WATOTO WANA OISHI MAZINGIRA HATARISHI		
	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	M	K	JM	M	K	JM
1016	388	468	854	228	275	503	159	172	332	32	31	63	61	64	125
	5	8	6	2	1	3	7	8	5						

### MIPAKA YA KATA

Kata ya Kashaulili imepakana na Kata za:-

1. Upane wa Mashariki imepakana na Kata ya Nsemulwa.
2. Upane wa Kaskazini imepakana na Kata ya kawajense.
3. Upane wa Magharibi imepakana na Kata ya Makanyagio.
4. Upane wa Kusini imepakana na Kata ya Majengo.

### SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Wananchi wa Kata hii ya Kashaulili wanajishughulisha na shughuli za biasharaya kubwa na wajasiliamali wadogo wakulima kwa kulimia nje ya Kata hii wanafanya shughuli zao za kilimo kwa Kata za Kakese, Mwamnkulu, Magamba n.k. Pia ni wachimbaji wa madini kwa kutumia Kata zenye madini. Watumishi mafundi wa fani mbalimbali.

### IDADI YA WATUMISHI KWENYE KATA

IDARA	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU	MAELEZO
UTAWALA	4	3	1	Tunahitaji mtendaji wa Mtaa 1
ELIMU	24	34	57	Walimu hawatoshi kulingana na idadi
AFYA	1	1	-	Kata moja na anafanya kazi vizuri
KILIMO	1	1	-	Anaudumia Kata Nne (4)
MAENDELEO YA JAMII	1	1	-	Anaudumia Kata mbili (2)
UVUVI	1	1	-	Anaudumia Kata mbili (2)

**VIONGOZI WALIOPO KATIKA KATA**

<b>VIONGOZI WA KUCHAGULIWA</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>WALIOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>	<b>MAELEZO</b>
WAH. MADIWANI	2	2	-	Wa Kata 1 viti maalumu 1
WENYEVITI WA MITAA	3	3	-	Wote wametoka chama tawala CCM
WAJUMBE SERIKALI ZA MTAA	15	13	2	Wamehama

**HUDUMA ZA JAMII ZILIZOPO**

Kata ya Kashaulili ina huduma za jamii kama ifuatavyo:-

**1. SHULE ZA MSINGI TATU, AMBAZO NI**

- (i) Shule ya msingi Kashaulili
- (ii) Shule ya msingi Mwangaza
- (iii) Shule ya msingi Uhuru

**2. MASOKO.**

- (i) Soko la Kuu
- (ii) Soko la Buzogwe

**3. KITUO KIDOGO CHA MABASI****4. HUDUMA ZA KIBENK.**

- (i) **NMB, POSTA N.K**

**3. IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE.**

<b>SHULE</b>	<b>WALIMU</b>			<b>WANAFUNZI</b>			<b>MADARASA</b>			<b>MADARAJA</b>			<b>VYOO</b>		
	<b>ME</b>	<b>KE</b>	<b>JML</b>	<b>ME</b>	<b>KE</b>	<b>JML</b>	<b>HIT</b>	<b>TAP</b>	<b>PUNG</b>	<b>HIT</b>	<b>TAP</b>	<b>PUN G</b>	<b>HIT</b>	<b>TAP</b>	<b>PUNG</b>
Kashaulili	6	15	21	552	615	1167	27	8	21	365	365	-	44	10	34
Mwangaza	-	-	-	614	608	1222	27	10	17	357	357	-	42	16	26
Uhuru	8	10	18	528	516	1039	16	3	13	316	276	40	37	10	27
<b>JUMLA</b>	<b>23</b>	<b>34</b>	<b>57</b>	<b>1508</b>	<b>1099</b>	<b>3137</b>	<b>70</b>	<b>21</b>	<b>51</b>	<b>1038</b>	<b>998</b>	<b>40</b>	<b>123</b>	<b>36</b>	<b>87</b>

**TAARIFA ZA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU ZA SHULE ZA MSINGI KATIKA ROBO YA NNE YA MWAKA APRIL HADI JUNI 2018.**

<b>SHULE</b>	<b>APRIL</b>	<b>MAY</b>	<b>JUNE</b>	<b>JUMLA</b>
KASHAULILI	912,229.61	912,229.61	912,229.61	2,736,6883.02
MWANGAZA	681,651.03	681,651.01	681,657.07	204,483.09
UHURU	609,576.01	609,576.01	609,576.01	1,828,728.03
<b>JUMLA</b>	<b>2,203,456.65</b>	<b>2,203,456.65</b>	<b>1,663,456.64</b>	<b>4,769,900.75</b>

**- UTORO SHULENI**

Swala la utoro kwa wanafunzi limepungua kidogo baada ya wazazi wa watoto kuchukuliwa hatua za Kisheria bado upo mtoro mdogo wa rejareja,

**4. AFYA**

Kata ya Kashaulili haina kituo cha afya wananchi wa Kata ya Kashaulili wanapata huduma ya afya katika Hospitali ya Manispaa, kituo cha afya Kata ya Majengo, Dispensali za watu binafsi, Pharmacy na maduka ya madawa baridi yaliyopo ndani ya Kata.

**- SHUGHULI ZA AFYA ZILIZOFANYIKA**

1. Kufanya msako wa usafi wa mazingira Kaya kwa Kaya
2. Uzoaji taka taka katika masoko, soko kuu, soko la buzogwe na stendi.
3. Ukaguzi wa usafi wa mazingira katika nyumba za kuishi na majengo ya biashara
4. Kusimamia na kuhamasisha usafi katika nyumba za kuishi katika mitaa yote **3**
5. Kila jumamosi ya mwisho wa mwezi tunafanya kazi ya usafi katika maeneo yao na kusimamia uzoaji wa taka katika masoko na mitaa.
  - Tunafanya kazi ya kuhamisisha usafi katika nyumba za kuishi katika mitaa yote **3**, ni kila jumamosi ya mwisho wa mwezi tunafanya kazi ya kuhamasisha wananchi kufanya usafi katika maeneo yao na kusimamia uzoaji wa taka katika masoko na mitaa.
  - Katika kata ya Kashaulili kuna majengo **114** ya biashara katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka kuanzia JanuaryApril hadi Juni ukaguzi ulifanyika kama ifuatavyo.
  - Katika robo hii ya nne hakuna magonjwa ya mlipuko yaliyojitokeza
  - Kamati ya Ukimwi ya Kata kimefanyika kikao kimoja (1) cha kamati ya Ukimwi, kazi iliyofanyika ni kuanzisha sense ya kaya kwa kaya kwa ajili ya kupata idadi ya hali halisi ya wanakaya na idadi ya maambukizi na kuhamasisha upimaji wa hiari.

<b>S/N</b>	<b>AINA YA BIASHARA</b>	<b>MAJENGO YALIYOKAGULIWA</b>	<b>NOTISI ZILIZOTOLEWA</b>	<b>MAJENGO YALIYOTENGWA</b>
1.	MAMA LISHE	70	30	1
2.	BUCHA	24	-	0
3.	GUEST HOUSE	24	15	0
4.	SALOON	15	15	0
5.	MIGAHAWA	3	1	0

**- SEKTA YA KILIMO**

Shughuli zilizofanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka kuanzia **April** hadi **June 2018** katika idara ya Kilimo, Chakula, Viwanda na ushirika.

- (i) Kusimamia bei za mazao

**- HALI YA CHAKULA**

Hali ya chakula inaridhisha kwani mazao mbalimbali kama Mihogo na Viazi vitamu vimevunwa na vinapatikana sokoni kwa wingi na kwa bei nzuri pia mahindi mabichi yanasaidia kupunguza bei ya nafaka (Mahindi)

**NAFAKA NA BEI ZAKE KATIKA JEDWALI KWENYE MASOKO.**

<b>NAFAKA</b>	<b>KIPIMO</b>	<b>BEI YA SOKO (TSHS)</b>
Mahindi	Kg	400/= 450/=
Muhogo	Kg	500 – 1000/=
Viazi vitamu	Kg	500/=
Maharage	Kg	1600 – 2000/=

**JEDWALI LA MALENGO NA UTEKELEZAJI WA KILIMO MSIMU 2017 – 2018**

<b>MAZAO YANAYOLIMWA</b>	<b>MALENGO YA KILIMO</b>			<b>UTEKELEZAJI WAKE</b>		
	Italimwa	Uzalishaji Tija/Tone	Makisio ya mavuno tone	Italimwa	Uzalishaji Tija/Tone	Mavuno halisi
Kabichi	0.5	3.0	1.5	0.35	3.0	1.05
Mchicha	1.0	2.0	2.0	0.5	2.0	1.0
Chainizi	1.0	1.5	1.5	0.5	1.5	0.75
Nyanya	0.5	3.5	1.7	0.4	3.5	1.4

**HUDUMA ZA UGANI**

Huduma za ugani zilizofanyika ni ushauri juu ya ufugaji bora kwa mifugo mbalimbali kama Kuku, Ng’ombe na Mbuzi jumla ya wafugaji **5** wamepata elimu juu ya ulishaji mzuri na jinsi ya kuandaa chakula cha Kuku. Umuhimu wa kufuga kuku bandani na kuzingatia chanjo. Kuwahamasisha wananchi kuhusu kilimo cha Korosho na Pamba.

**PEMBEJO ZA KILIMO**

Katika msimu huu wa kilimo pembejo za ruzuku hazikuwepo isipokuwa pembejeo za kilimo zimekuja kwa mfumo mpya wa bei elekezi ambapo mfuko wa **DAP** uliuzwa kwa shilingi

**53,732** na **UREA** Tsh. **41,133** ambapo maduka yote ya pembejeo yalizingatia bei hizo zilizotolewa na **TFC**.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO.**

Katika kipindi cha robo ya nne kuanzia **April** hadi **Juni 2018** kazi zilizofanyika

- (i) Kuhamasisha uundaji wa Vikundi katika mitaa mitatu ya Kata ya Kashaulili na kimeundwa kikundi kimoja na wapo katika hatua ya kuandaa katiba.
- (ii) Kutembelea kaya za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kaya zenye watoto walioathirika na walioathiriwa na zinazohudumiwa na shirika la **ACT Rukwa**.
- (iii) Kukutana na wanavikundi
- (iv)– Amani agriculture
- (v) Rahamani  
Ambao waliahidi kukamilisha mkopo wao tarehe **20/07/2018** na watarejesha pesa zote wanazodaiwa
- (vi) Kutoa mkopo kwa kikundi kimoja cha Pcohecago ambao walipewa Mkopo wa tshs **2,000,000/=** (Milioni mbili) tu na wataanza kurejesha tarehe **10/07/2018**
- (vii) Kufuatilia marejesho ya mikopo yote

JINA LA KIKUNDI	KIASI CHA MKOPO	MAREJESHO JUMLA			JUMLA
		APRIL	MAY	JUNE	
Kikundi cha GIFTSHEZA	2,000,000/ =	-	-	-	Wamemaliza kurejesha
Kikundi cha WAJANE	3,000,000/ =	272,000/ =	272,000/ =	272,000/ =	8,160,000/=
Kikundi cha SHOOTING	3,000,000/ =	275,000/ =	275,000/ =	275,000/ =	8,250,000/=
<b>JUMLA</b>					1,641,000/=

**ULINZI NA USALAMA**

- Katika kipindi cha robo ya nne ya mwezi April hadi Juni **2018** hakuna matukio makubwa yaliyotokea.
- Kilifanyika kikao kimoja cha kamati ya ulinzi na usalama cha Kata
- Mikutano ya hadhara haikufanyika kwa sababu wananchi walishindwa kufika katika Mkutano.

**(i) SEKTA YA MAJI**

**VISIMA VILIVYOPO**

MTAA	MAHITAJI	VILIVYOPO	PUNGUFU

KASHAULILI	5	1 na gati 1 la maji ya Ikorongo	4
BUZOGWE	5	2	3
KOTAZI	3	-	-

**(ii) MIUNDO MBINU – BARABARANI**

- Katika kipindi cha April hadi Juni Machi **2018**. Kata ya Kashaulili inaendelea na matengenezo ya barabara za Rami Km. **7.7** wameanza maeneo yote barabara zinakopita.

KATA	MTAA	IDADI YA VIKAO	AINA ZA VIKAO	MIKUTANO
Kashaulili		1	WDC	1
		1	Ulinzi na Usalama	
		1	Kamati ya Malalamiko	
		1	Kamati ya mazingira	
		1	Kamati ya Ukimwi	
	Kashaulili	3	MD	
	Buzogwe	3	MD	1
	Kotazi	2	MD	Hamna

- Kazi nyingine iliyofanyika ni uandikishaji wa zoezi la **NIDA**, ambao tuliandikisha watu **10,000/=**

**(iii) TAARIFA YA BARAZA LA KATA KATIKA KIPINDI CHA ROBO NNE YA MWAKA KUANZIA APRIL – JUNI 2018 .**

Baraza lilipokea mashauri 34 aina ya mashauri.

1. Ndoa mashauri - 2
2. Madai - 3



- Katika kipindi cha robo ya nne kuanzia April hadi Juni Baraza hawakupiga faini

Mapato ya Baraza kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2018 ni Tshs. **50,000/=** ambazo zimepatikana kwa ajili ya kufungua kesi

Nazimetumika kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kesi zimetumika kununua stationery.

#### **(iv) CHANGAMOTO ZA KATA**

##### **- AFYA.**

- (i) Ukosefu wa mafuta ya gari kwa wakati
- (ii) Wafanyabiashara kutofika kwa wakati asubuhi ya mwisho wa mwezi kufanya usafi katika maeneo yao hivyo kuleta usumbufu katika swala la uzoaji wa taka.
- (iii) Taasisi kutotoa fedha ya tozo ya taka kama vile Mabenki na mashirika mbalimbali ikiwemo makanisa pia.
- (iv) Kugomea viwango vya tozo vilivyowekwa

##### **- KILIMO**

- (v) Bei za madawa ya mifugo kuwa juu zinasababisha wafugaji wengi kushindwa kuwa na utaratibu wa tiba na chanjo kwa mifugo yao.

#### **(vi) MAPENDEKEZO AU USHAURI**

- (i) Tunashauri gari la takataka lipatiwe mafuta kwa utaratibu maalum ili kila siku liweze kuondoa taka ili mji wetu uwe katika mazingira safi.
- (ii) Tunashauri Mkurugenzi kuwaandikia barua taasisi na mashirika na kuwaelekeza utaratibu wa uzoaji taka.
- (iii) Upungufu wa askari mazingira kwenye swala la usafi wa mazingira wengi wamewekwa kwenye Ushuru.

##### **- MAFANIKIO**

- (i) Katika swala la kusimamia usafi wa mazingira tumefanikiwa kupunguza muonekano wa Rambo na Taka Mjini baada ya kuzuia kutupa taka kwenye vizimba
- (ii) Tumefanikiwa kwa aslimia **85%** kuondoa Taka kwenye mitaa

#### **TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**

Katika mwaka wa fedha **2017 – 2018** Kata imekisia kukusanya na kupokea kiasi cha Tsh **35,754,117.04** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo

#### **MAPATO**

- Kwa kipindi cha mwezi April Hadi Juni **2017/2018** Kata imepokea kiasi cha Tsh **13,166, 400.75** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato sawa na asilimia **37** ya makadirio yake ya Tsh **35,754,117.04**

**MATUMIZI**

- Kwa kipindi cha January Hadi Marchi Kata imetumia kiasi cha fedha **12,951,300.75** katika kutekeleza shughuli za maendeleo kama ifuatavyo:-

**MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI**

NA	KATA	MTAA	AINA YA MRAD I SHUGHULI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
					TOLEWA	TUMIKA	SALIO		
1.	KASHAULILI	BUZOGWE	Ukamili shaji wa Ofisi ya Kata	H/mashauri nguvu za wananchi	-	-	-	Finishing	Zinatakiwa fedha <b>19,037,579</b> ili kukamilisha kazi zilizobaki, kati ya hizo fedha fundi anadai <b>8,000,000/=</b>
		<b>KASHAULILI BUZOGWE KOTAZI</b>	Uendes haji wa shule za msingi	Captation	4,769,900.75	4,769,900.75	-	Fedha zinatumiwa kwa kufuata maelekezo	Fedha hizo zimeboresha ufundishaji mashuleni
		<b>KASHAULILI</b>	Tozo ya taka	Wananchi	524,000/=	524,400/=	-	Swala la usafi linaendelea	Jamii bado haijaelimika
		<b>KOTAZI</b>	Tozo ya taka	Wananchi	1,775,500/=	1,712,400/=	63,100/=	Zoezi la usafi linaendelea	Bado wananchi wanaendelea kulalamikia risiti za karatasi
		<b>BUZOGWE</b>	Tozo ya taka	Wananchi	1,097,000/=	945,000/=	152,000/=	Zoezi la usafi linaendelea	Bado wananchi wanaendelea kulalamikia risiti za karatasi
		<b>KASHAULILI BUZOGWE</b>	Posho za wenye vitaji na wajumbe serikali	Halmashauri	-	-	-	Fedha hazijapokelewa	Katika kipindi cha robo ya tatu na nne hakuna fedha asilimia <b>20%</b> zilizokuja

			za mitaa						
		<b>KASHAULILI BUZOGWE KOTAZI</b>	Uendes haji wa Ofisi za mitaa	Halmashauri	-	-	-	Fedha hazijapokelewa	Katika kipindi cha robo ya tatu na nne hakuna fedha asilimia <b>20%</b> zilizokuja
		<b>KASHAULILI BUZOGWE KOTAZI</b>	Uendes haji wa Ofisi ya Kata	Halmashauri	-	-	-	Fedha hazijapokelewa	Katika kipindi cha robo ya tatu na nne hakuna fedha asilimia <b>20%</b> zilizokuja
		<b>BUZOGWE</b>	Ujenzi wa mashi mo ya vyoo soko la buzogwe	Halmashauri	5,000,000/=	5,000,000/=	-	Mradi umekamilia na unatumika	Fundi anadai <b>2,833,000/=</b>
	<b>JUMLA KUU</b>				<b>13,166,400.75</b>	<b>12,951,300.75</b>	<b>215,100</b>		

Naomba kuwasilisha

**MHE :JOHN MATONGO  
DIWANI KATA YA KASHAULILI**

## **KATA YA KASOKOLA**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA KASOKOLA KWA KIPINDI CHA ROBO YA IV YA APRIL – JUNE 2018

### **UTANGULIZI:**

Kata ya Kasokola ni miongoni mwa Kata 15 zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na iko Kaskazini Magharibi mwa Halmashauri ya Manispaa pia imo ndani ya tarafa ya Kashaulili na ina Vijiji vitatu ambayo ni Kasokola Manga, na Sungamila na ka mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka 2012 Kata hii ina jumla ya wakazi kama ilivyooneshwa kwenye jedwari hapo chini:-

<b>NA</b>	<b>KIJIJI</b>	<b>VITONGOJI</b>	<b>KAYA</b>	<b>IDADI YA WATU</b>
1	Kasokola	08	397	1797
2	Manga	08	324	1964
3	Sungamila	04	122	626
<b>JUMLA</b>		<b>20</b>	<b>843</b>	<b>4387</b>

### **SHUGHULI ZA WAKAZI:**

Shughuli za wakazi katika kata hii ni kama ifuatavyo:

1. Biashara ndogo ndogo
2. Wakulima
3. Wafugaji
4. Wafanyakazi wa serikali na Mashirika

### **VIKAO VYA KISHERIA:**

- a) Ngazi ya Kata  
Imefanyika WDC mbili  
(i) Tarehe 05/4/2018 na 16/7/2018

Ambapo kazi yake ni kupokea kujadili na kupitisha raarifa mbalimbali za vikao na mikutano ya hadhara toka kwenye vijiji vyote vitatu vya kata ya Kasokola .

- b) Ngazi ya vijiji

- c) Kata ya Kasokola ina jumla ya vijiji vitatu ambapo mpaka sasa vimefanya vikao 09 vya ndani na mikutano 04 ya hadhara ambayo kazi yake ni kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na mambo mengine.

Shughuli za maendeleo ziizoelekezwa kwa robo ya IV ya JULY - SEPTEMBER 2018

- (i) Ujenzi wa ukuta wa jiko Sekondari Kasokola
- (ii) Michango ya tofali Kijiji cha Kasokola imekamilika.

## UTAWALA BORA NA UTAWALA WA KISHERIA:

Utawala bora wa Demokrasia inatumika katika kushirikisha jamii katika vikao na mikutano ya hadhara kama ifuatavyo:-

### (i) Ngazi ya Kata

Kupitia vikao vya WDC ambavyo wajumbe wake ni wenyeviti wa Serikali za vijiji ya kata ya kasokola wataalamu ndani ya kata hii ya kasokola wazee maarufu viongozi wa chama tawala ambapo kazi yake ni kupokea taarifa toka kwenye vijiji na kuzijadili.

### (ii) **VIONGOZI WALIOPO KATIKA KATA:**

	<b>MAHITAJI</b>	<b>WALIOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>	<b>MAELEZO</b>
VIONGOZI WA KUCHAGULIWA WAH:MADIWANI	2	2	-	WAKATI 1
WENYEVITI WA MTA	3	3	-	VITI MAALUMU 1
WAJUMBE ZA SERIKALI ZA MITAA	20	20	-	WOTE WAMETOKA CHAMA TAWALA CCM

### (iii) Ngazi ya vijiji.

Kupitia vikao vya ndani vya serikali za vijiji pamoja na mikutano ya hadhara ambapo wananchi wanapata nafasi ya kuzungumza na kupanga mipango yao. Utawala wa kisheria unatumika kupitia baraza la kata ambapo watu huelekezwa kupeleka malalamiko yao na kusikilizwa na maamuzi kutolewa. Pia kupitia kamati ya ulizu na usalama na mikutano ya hadhara ya viongozi likiwemo jeshi la polisi wananchi wanaendelea kuelimishwa juu ya utii wa sheria bia shuruti.

## HUDUMA ZA JAMII.

### (i) **ELIMU MSINGI NA SEKONDARI**

#### **TAARIFA YA ELIMU MSINGI NA ELIMU SEKONDARI 2017/2018**

<b>NA</b>	<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI YA MADARASA</b>	<b>MADARASA YALIYOPO</b>	<b>UPUNGUFU ULIYOPO</b>
1	S/S KASOKOLA	10	8	2
2	S/M KASOKOLA	13	9	4
3	S/M MANGA	9	6	3
4	S/M SUNGAMILA	9	9	0

Kuhusu upungufu wa madarasa WDC ya tarehe 05/07/2018 pamoja na mikutano mikuu ya hadhara wameamua kuwa kila mtaa kujenga madarasa 2 kila shule. Lakini kwa sekondari wataunganisha nguvu za vijiji vyote kujenga darasa 1. Shule mpya ya Kasorwa wananchi walijitolea tofali 10,000/= ujenzi unaendelea.

### **IDADI YA WALIMU MSINGI NA SEKONDARI:**

<b>NA</b>	<b>JINA LA SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>WALIOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
1	S/S KASOKOLA	20	16	4
2	S/M KASOKOLA	13	13	0
3	S/M MANGA	9	11	0
4	S/M SUNGAMILA	9	8	1
	<b>JUMLA</b>	<b>31</b>	<b>32</b>	<b>5</b>

**IDADI YA WANAFUNZI SEKONDARI NA MSINGI:**

NA	JINA LA SHULE	IDADI ME	IDADI KE	JUMLA
1	S/S KASOKOLA	168	131	299
2	S/M KASOKOLA	244	258	502
3	S/M MANGA	179	176	355
4	S/M SUNGAMILA	176	183	359

**INTERNATIONAL SCHOOL (MEDIUM SCHOOL)**

1. REIMETER (ENGLISH MEDIUM)
2. NZELA ENGLISH MEDIUM
3. MWIGA MEDIUM SCHOOL

**TAARIFA ZA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU ZA SHULE ZA MSINGI KATIKA ROBO YA NNE.**

SHULE	FEDHA ZILIZOTOLEWA
KASOKOLA	124,201/=
MANGA	1,809,604/=
SUNGAMILA	1,674,060/=

**UANDIKISHAJI WA DARASA LA AWALI:**

WALIOTARAJIWA				WALIOANDIKISHWA			WANAOSOMA		
SHULE	ME	KE	JMLA	ME	KE	JMLA	ME	KE	JMLA
KASOKOLA	6	6	12	6	6	12	6	5	11
MANGA	5	6	11	5	6	11	5	6	11
SUNGAMILA	5	3	8	5	3	8	5	3	8

**UTORO SHULENI**

Swala la utoro kwa wanafunzi lipo, utoro wa reja reja hivyo kupitia kikao cha wadau wa elimu ngazi ya kata kiliazimia wazazi na watoto watoro wafikishwe baraza la kata kwa sababu suala la utoro lina changia kushuka kwa elimu na fedha ila hayatopatikana kutokana na faini irudiswe shuleni kwa kusaidia uchapaji wa mitihani ya mazoezi ya watoto.

SHULE	IDADI WATORO	YA	WALIOFIKISHWA BARAZA LA KATA	WALIOLIPA FAINI	MAELEZO
KASOKOLA	29		29	0	Kesi ndo imeanza kutolewa maelezo
MANGA	18		18	0	Kesi ipo baraza la kata
SUNGAMILA	20		19	0	Bado kesi inasikilizwa maamuzi

**HUDUMA:**

SOKO – Hakuna  
BANK – Hakuna

(ii) Maji

NA	VIJIJI	VISIMA VIREFU		VISIMA VIFUPI		MAGATI MAGATI	
		VIZIMA	VIBOVU	VIZIMA	VIBOVU	VIZIMA	VIBOVU
1	Kasokola	3	1	0	0	0	0
2	Sungamila	0	0	0	0	2	0
3	Manga	1	0	2	0	0	0

Swala la maji bado ni tatizo kwa kata hii ya kasokoa na vijiji vyake vyote vitatu kwa sababu bado hatujapata huduma ya maji kupitia mtando wa mabomba richa ya kuwepo na vyanzo vya maji katika kijiji cha manga na ikolongo ambavyo hutumika kusambaza maji mjini

**(iii) Afya na Tiba**

Kata ya kasokola ina zahanati moja ambayo ipo kijiji cha kasokola zahanati hii inahudumia vijiji vitatu ambavyo ni:-

1. Kijiji cha Kasokola
2. Kijiji Manga
3. Kijiji cha sungamila.

(a) Watumishi waliopo katika zahanati ni wane (4)

JINA KAMILI	CHEO
JUSTINE NOEL	ACO – MGANGA WA KITUO
ADELIN FUSI	EN
VENERANDA KALYALYA	EN
JOYCE BILAGO	MA

Zahanati ina upungufu wa watumishi 8 kutokana na idadi inayotakiwa 12 ya watumishi katika zahanati.

(b) Huduma zinazotolewa katika zahanati ya kasokola ni kama ifuatavyo:-

- i. Kutibu wagonjwa wa nje (OPD)
- ii. Klinick ya wajawazito (ANC)
- iii. Klinick ya watoto (RCH)
- iv. Klinick ya uzazi wa mpango (FAMILY PLANING)
- v. Kutoa dawa kwa wakina mama wenye maambukizi ya VVU (PMCT)
- vi. Huduma ya kina mama kuja kujifungua.

Tuliketi kikao cha WDC tarehe 16/7/2018 kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali yaliyojadiliwa katika kamati ya ukimwi kilichoketi tarehe 14/07/2018 kwa ajili ya kutoa elimu mbalimbali kuhusu kudhibiti ukimwi na kupunguza maambukizi ya ukimwi kwa kutumia kamati kuzungukia wananchi na kuwaelimisha. Upimaji bado unasisitizwa ili wananchi waweze kufahamu afya zao kwa kupitia kamati ya ukimwi ya kata.

**Changamoto ya zahanati.**

- I. Uchakavu wa miundombinu – jengo limechakaa.
- II. Ukosefu wa maji katika zahanati
- III. Ukosefu wa nyumba za watumishi idara ya afya

(c) Kata ya Kasokola ina maduka matatu ya dawa muhimu ya binadamu yaliyosajiliwa kisheria.

(d) Shughuli za afya zilizofanyika

- i. Kusimamia na kuimarisha usafi wa mazingira katika vijiji vitatu
- ii. Kila jumamosi ya mwisho wa mwezi kitaifa tunafanya usafi.
- iii. Kufanya msako wa mazingira wa usafi kwa kila kaya
- iv. Ukaguzi wa usafi wa mazingira katika nyumba za kuishi na biashara unafanyika kila wakati.

Na	AINA BIASHARA YA	MAJENGO YALIYOKAGULIWA	NOTISI ZILIZOTOLEWA	MAJENGO YALIYOJENGWA
1	MAMA LISHE	5	-	-
2	BUCHA	1	-	1
3	SALOON	3	-	3
4	MGAHAWA	1	1	0

**(iv) Afya na kinga**

Wananchi wanaendelea kutekeleza maagizo ya serikali ya kufanya usafi kila mwisho wa mwezi ikiwa ni ukaguzi wa vyoo kupalilia na kufyeka nyasi na ili kutekeleza swala hili la kinga kata vya kasokola imeagiza ziundwe kamati za afya za kila kijiji ambazo zitakuwa zinasaidiana na kamati za afya za kata.

**(v) Kilimo/Mifugo.**

Hali ya chakula inaridhishwa kwani maeneo mbalimbali kama mihogo na viazi vitamu vimevunwa na vinapatikana sokoni kwa wingi na kwa bei nzuri pia mahindi.

**NAFAKA NA BEI ZAKE KATIKA JEDWALI.**

NAFAKA	KIPIMO	BEI YA SOKO TSHS.
Mahindi	Kg	400/450
Mihogo	Kg	500-1000
Viazi vitamu	Kg	500
Maharage	Kg	1600-2000

**HUDUMA ZA UGANI.**

Huduma za ugani zilifanyika ni ushauri juu ya ufugaji kwa mifugo mbalimbali kama Ng'ombe na mbuzi, kuku, jumla ya wafugaji 10 wamepata elimu juu ya uzalishaji na jinsi ya kuandaa chakula cha kuku na kuzingatia chanjo.

Kuhamasisha wakulima kuhusu kilimo cha korosho na pamba na mihogo kata ya kasokola imelima na kupanda miche ya korosho.

**PEMBEJEO ZA KILIMO.**

Katika msimu wa kilimo pembejeo za ruzuku hazikuwepo isipokuwa pembejeo za kilimo zimekuja kwa mfumo mpya wa bei elekezi ambayo mfuko wa DAP ulizwa kwa **tshs 53,732** na UREA **tshs 41,133** ambapo maduka yote ya pembejeo yalizingatia bei hizo zilizotolewa na TFC.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII.**

**JINSIA NA WATOTO.**

Katika kipindi cha robo ya nne kuanzia MAY-AUGUST 2018 Kazi zilifanyika

- i. Kuhamasisha kazi zilifanyika
- ii. Kufuatilia marejesho kwa vikundi vy kata ya Kashaulili vilivyopo kama ifuatavyo.

JINA LA KIKUNDI	KIASI CHA MKOPO	MAREJESHO
KISUNGE	1,000,000/=	
KIWASU	1,000,000/=	
KIVICHA	3,000,000/=	
YAGASAMA	1,150,000/=	
KIWAKA	1,000,000/=	

**MAENDELEO YA JAMII:**

**(I) VIKUNDI:**

Vipo vikundi mbalimbali vya vijana na wakina mama ambavyo ujishughuisha na shughuli mbalimbali za ujasiliamari ikiwa ni pamoja na kilimo cha bustani.

**(II) TASAF:**

Vilevile katika Nyanja hii ya maendeleo ya jamii sekta ya tasaf walengwa wa mfuko huu wanaendelea kunufaika kupitia halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.



### **Mifugo katika kata ya kasokola ni kama ifuatavyo:-**

<b>NA</b>	<b>VIJIZI</b>	<b>NG'OMBE</b>	<b>MBUZI</b>	<b>MBWA</b>	<b>NGURUWE</b>
1	Kasokola	400	160	67	21
2	Manga	270	33	17	32
3	Sungamila	34	28	12	16
	<b>JUMLA</b>	<b>704</b>	<b>221</b>	<b>96</b>	<b>79</b>

### **TAARIFA ZA BARAZA LA KATA KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA KUANZIA APRILI-JUNI 2018**

Baraza lilipokea mashauri aina ya mashauri

1. Ndoa mashauri
2. Mgogoro wa Ardhi
3. Madai
4. Utoro mashuleni -25

Mapato ya baraza kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka ni shilingi 100,000/= kwa ajili ya kufungua kesi na faini. Zimetumika kama ifuatavyo:-

1. Faini za utoro wa wanafunzi bado kesi zina jadiliwa kwa utekelezaji
2. Kufungua kesi zimetumika kununua stationary
3. Faini za usafi wa mazingira hakuna.

**NB:** Yamelimwa mashamba darasa Ekari tatu (3) katika maeneo ya shule ya msingi kasokola, shule ya msingi manga na shue ya msingi sungamila. Pia zinatarajiwa kulimwa ekari (50) za zao la pamba na korosho.

#### **ARDHI:**

Bado maeneo ya makazi na maeneo mengine ardhi hayajapimwa swala linao pelekea wananchi kujenga kiholea. Tumeomba kupimiwa ardhi eneo la manga kwa kupitia mkutano wa wananchi kwa awamu ya kwanza.

#### **BIASHARA/MASOKO:**

Wanachi wa kata ya kasokola wanaendelea kufanya shughuli zao ndogondogo za biashara kwenye masoo ya mjini.

#### **ULINZI NA USALAMA:**

Swala la ulinzi na usaama linaendelea kufanyiwa kazi kwa msisitizo wa hali ya juu kwa kuandikisha wakazi wote kwenyemadaftari ya wakazi kwa kila kijiji na kuzingatia vibali kwa wahamiaji wanaotoka sehemu mbalimbali ili kudhibiti hali ya usalama katika kata yetu ya kasokola.

Ulinzi shirikishi unafanyika kila wakati ili kuweka hali ya usalama vizuri.

#### **MAJANGA**

Mpaka sasa hakuna majanga yoyote yaliyojitokeza katika kata ya Kasokola

#### **Changamoto:**

1. Kuto pimwa kwa maeneo ya kasokola kunapelekea kujenga kiholela .
2. Upungufu wa watendaji wa vijiji kwa ajii ya usimamizi wa shughuli mbali mbali za kiutawala .
3. Uchakavu jengo la zahanati ya kasokola
4. Uchakavu wa nyumba ya mganga mkuu wa zahanati.

5. Ukosefu wa usafiri wa ofisi eg pikipiki.
6. Ukosefu wa vitendea kazi eg. Kompyuta.
7. Ukosefu wa umeme katika jengo la serikali.

**HITIMISHO:**

Uongozi wa kata pamoja na uongozi wa mitaa utaendelea kuhamasisha wanachi juu ya umuhimu wa kuchangia nguvu zao katika miradi ya maendeleo pia ofisi ya mkurugenzi inaombwa kuleta fedha kwa wakati mara tu wananchi wanapokuwa wameibua miradi hiyo na kuanza kutekeleza kwa kusogeza nguvu zao katika mradi. Pia sheria ya uanzishwaji wa miradi bila kuwepo katika bajeti katika kata yetu umezingatiwa kuhakikisha hakuna mradi wowote ambao unaanzishwa bila kuwepo katika bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,  
Naomba kuwasilisha.**

**CHRISANT A MWANAWIMA  
DIWANI KATA YA KASOKOLA.**

## KATA YA KAWAJENSE

TAARIFA YA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018 KWA KATA YA KAWAJENSE KWA ROBO YA NNE APRIL HADI JUNI 2018

A: UTANGULIZI:

Kata ya Kawajense ni miongoni mwa kata 15 zinazounda manispaa ya Mpanda ambayo ipo Tarafa ya Kashaulili.

B: MIPAKA YA KATA.

- Upane wa Mashariki inapakana na kata ya Kazima na Nsemulwa,
- Upane wa Kaskazini inapakana na kata ya Shanwe na Kazima,
- Upane wa Magharibi inapakana na kata ya Makanyagio,
- Upane wa Kusini inapakana na kata ya Kashaulili na Nsemulwa.

C: MAENEO YA KIUTAWALA

Kata ya Kawajense ina jumla ya mitaa mitatu(3) ambayo ni:- Mtaa waKawajense, mtaa wa Majengo Mapya na Mtaa wa Ikulu.

D: UONGOZI ULIOPO KATIKA KATA

- i. Diwani wa Kata
- ii. Diwani viti maalumu
- iii. Afisa mtendaji Kata
- iv. Wenyeviti wa mitaa
- v. Wataalamu ngazi ya kata
- vi. Watendaji wa mitaa.

E: IDADI YA VIKAO VYA KISHERIA.

VIKAO VYA WDC			VIKAO VYA MITAA				
VIKAO HITAJIKA KWA MWAKA	VIKAO VILIVYO FANYIKA	VIKAO MAALUMU	JINA LA MTAA	VIKAO HITAJIKA KWA MWAKA	VILIVYO FANYIKA	MIKUTANO HITAJIKA	ILİYOFANYIKA
4	4	3	KAWAJENSE	12	5	4	1
			MAJENGO MAPYA	12	11	4	3
			IKULU	12	11	4	2

NB:Kwa mtaa wa kawajense vikao havikufanyika kwa mujibu wa kalenda ya vikao kwa sababu mtendaji wa mtaa alikuwa likizo ya uzazi.

Pia vikao hivyo vimefanyika kwa tarehe kama ifuatavyo: Julai hadi Septemba tarehe 4.10.2017, Octoba hadi Desemba tarehe 5.1.2018, Januari hadi Machi tarehe 28.3.2018 na April hadi Juni tarehe 5.7.2018.

F: IDADI YA KAYA NA WAKAZI WA KATA YA KAWAJENSE.

JINA LA KATA	JINA LA MTAA	IDADI YA KAYA	IDADI YA KAYA			WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI			WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI		
			ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML
	KAWAJENSE	812	1632	1694	3326	418	436	854	532	572	1104
	MAJENGO MAPYA	703	812	1720	2532	1147	1160	2307	545	585	1130
	IKULU	691	1686	1715	3401	1137	1157	2294	554	563	1117
	JUMLA	2206	5038	5147	10185	3402	3453	6855	6131	1715	7846

## SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Wananchi wa kata ya Kawajense wanajishughulisha na kazi zifuatazo:-

- i. Kilimo na ufugaji mdogomdogo,
- ii. Wafanyakazi na watumishi wa mashirika,
- iii. Wachimbaji wadogo wa madini mbali mbali,
- iv. Wafanyabiashara wakubwa na wadogo,
- v. Mafundi wa fani mbali mbali.

## E: HALI YA UONGOZI

Katika kata ya Kawajense kuna ushirikiano mzuri kati ya viongozi wa serikali, vyama vya siasa na madhehebu ya dini kwa kushirikiana katika vikao vya ndani (WDC) na mikutano ya hadhara katika kuhamasisha wananchi kwa miradi ya maendeleo.

## F: IDADI YA WATUMISHI KILA IDARA

IKAMA	UTAWALA	KILIMO	AFISA AFYA	MAENDELEO	ELIMU MSINGI
MAHITAJI	4	2	2	1	123
WALIOPO	4	1	1	1	68
PUNGUFU	0	1	1	0	65

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MIRADI APRIL-JUNE 2018 KWA KIPINDI CHA MWEZI APRIL-JUNE 2018

MTAA	JINA LA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA TOLEWA	FEDHA TUMIKA	SALIO	UTEKELEZAJI
KAWAJENSE IKULU MAJENGO MAPYA	Posho za wenyeviti na wajumbe na uendeshaji ofisi.	Halmashauri	1,034,439/=	635,000/=	399439/=	Walengwa wamelipwa wote.
MAJENGO MAPYA	Ujenzi wa choo cha soko na cha ofisi ya kata.	Asilimia 20% zilizorejeshwa na Halmashauri.	919,150/=	919,500/=		Choo cha ofisi ya kata kimekamilika na kinatumika Choo cha soko kimekamilika bado kumalizia rangi nje tu.
MAJENGO MAPYA	Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya msingi Nyerere.	Mfuko wa jimbo	1,000,000/=	1,000,000/=		Madarasa yamekamilika .
IKULU	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Mfuko wa Jimbo.</li> <li>➤ Nguvu za</li> </ul>	1,500,000/=	1,050,000/=	450,000/=	Msingi umeanza kujengwa.

	moja.	wananchi.				
KAWAJENSE	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Nguvu za wananchi.</li> <li>➤ Mfuko wa Jimbo.</li> </ul>	1,500,000/=		1,500,000/=	Hatua za maandalizi ya ujenzi yanaendelea kwa kutafuta fundi.
OFICE YA KATA KAWAJENSE	Ujenzi wa choo cha ofisi ya kata Kawajense	20% Inayorejeshwa kwenye shughuli za maendeleo..	1,551,000/=	928,300/=	622,700/=	Choo kimekamilika na kinafanya kazi.

#### SEKTA YA AFYA KINGA

Kata ya Kawajense inapanga shughuli zifuatazo:-

- i. Kusimamia usafi wa mazingira na uzoaji taka.
- ii. Kuwahasisha wananchi kutumia vyandarua vyenye viuatilifu.
- iii. Kutoa elimu juu ya kujikinga na VVU/Ukimwi.
- iv. Kuwashauri wananchi kupima afya zao kuhusiana na VVU/Ukimwi.
- v. Katika kusimamia usafi wa mazingira ratiba ya usafi imepangwa kila siku ya Jumatano kuwa siku ya usafi katika Kata.

#### RATIBA YA UKAGUZI WA USAFI KILA JUMATANO YA WIKI

S/N	JINA LA MTAA NA ENEO LA KAZI	WASIMAMIZI	MFUATILIAJI
01.	Mtaa wa Majengo mapya kuanzia Mpaka njia mbili unashuka hadi barabara ya sokoni Majengo mapya hadi barabara ya Mikocheni.	Brycyson Mwalugala Mwl. Emable Kabale Patrick Mtandula	PRISCA CHOKOLA
02.	Eneo kuanzia barabara ya kanisa la New Harvest (Kwa Labani hadi kwa baba John makaburini.	Antonia Kakokere Wilbroad Milambo Lauliana Benard Odeta Michael.	ASNATI DIBWE
03.	Mtaa wa Kawajense kuanzia Mikocheni kushuka hadi barabara ya Mkombe hadi ofisi ya Tanesco kwa Mayeye hadi shule ya msingi Msakila kotazi hadi kompaundi kwa Mkurugenzi na shule ya msingi Msakila.	William Jumapili Edmund Mbunda Mwl. Mkuu Msakila Mary Kabeja	JOSEPH SANGANA
04.	Kutoka barabara ya Mkombe	Gervas Ntelengula Albert Kamsini Anna Sundu	AGNESS URASA

05.	hadi kwa Mzee Mzimya kupitia kwa DSO hadi nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya unarudi hadi Msikitini hadi kwa Betabula unapandisha hadi maeneo ya Endita "B" hadi kwa Mwanalinze	Elizabeth Mpigauzi J.	GIRBERT NYENYERI
06.	Mtaa Ikulu Eneo kuanzia Ikulu hadi barabara ya kutoka hospitali kwa Dhalla hadi Msikiti wa Madukani unashuka hadi darajani kwa Itala hadi soko la matunda unarudi kwa Zahoro na Misasi gereji na eneo lote la soko la matunda  Mtaa wa Ikulu. Kuanzia kwa marehemu Zacharia hadi kwa Kalubu unatokea kwa Betabula hadi soko la matunda hadi kisima cha maji kwa Simbao unarudi hadi Ikulu ndugo	Clement Mbamba Uwezo Bacho Peter Robert Rehema Masoud  Stephen Temezya Mary Kalubu Onesmo Kemanzi	PASCAL PELEKA

#### (A) HALI YA USAFI

Hali ya usafi inaridhisha, ratiba iliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa kwamba kila Ijumaa gari ya usafi litafika kuzoa taka Kawajense, lakini ratiba haizingatiwi kwa wakati husika.

#### (B) CHANGAMOTO

- i. Maeneo yasiyoendelezwa kama vile mapagala na viwanja visivyo endelezwa yanatunza uchafu na watu kutupia taka nyakati za usiku kwa kukwepa kulipa pesa ya ushuru wa taka Tshs. 2000/= kila mwezi ya umwagaji taka.
- ii. Wananchi wengi hawachangii hela ya ushuru wa taka na wenye nyumba wanaficha wapangaji wao na kusema ni familia moja.
- iii. Eneo la kata ya Kawajense ni kubwa sana kwa siku moja inashindikana kumaliza uzoaji taka.

#### ELIMU NA MAFUNZO

##### 1.1 HABARI ZA WANAFUNZI

SHULE	JINSIA	AWALI	MADARASA							JUMLA
			I	II	III	IV	V	VI	VI	
NYERERE	WV	192	244	266	226	130	132	93	44	1160
	WS	184	297	249	160	136	136	108	40	1193
	JML	376	541	515	586	266	268	201	84	2358
MSAKILA	WV	83	136	133	87	57	48	77	40	659
	WS	70	134	136	106	81	54	69	49	724
	JML	153	270	269	193	138	102	146	89	1383
MIZENGO PINDA	WV	120	144	58	52	54	43	60	43	
	WS	112	99	46	39	55	50	51	42	

	JML	232	213	104	91	109	93	111	85	903
JUMLA YA KATA	WV	216	447	457	365	241	223	230	127	2297
	WS	307	425	305	372	272	240	228	131	2342
	JML	523	872	888	670	513	463	458	258	4639

## 1.2 HABARI ZA WALIMU

SHULE	MAHITAJI			WALIOPO			PUNGUFU		
	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML
NYERERE	20	38	58	11	24	35	9	14	27
MSAKILA	15	25	40	7	17	24	8	8	16
MIZENGO PINDA	8	17	25	6	12	18	2	5	7
JUMLA YA KATA	43	80	123	19	49	68	24	31	55

## 1.3 MAJENGO

SHULE	MADARASA			VYUMBA WALIMU			STOO			VYOO			OFISI		
	MAH	VI L	PU N	MA H	VI L	PU N	MA H	VI L	PU N	MAH	VIL	PAPUNA	MAH	VIL	P U N
NYERERE	58	8	50	58		58	3	2	1	WV 47 WS 58	WV 7 WS 3	WV 40 WS 56	5	2	3
MSAKILA	35	6	29	35		35	2	1	1	WV 26 WS 36	WV 11 WS 10	WV 15 WS 26	5	2	2
MIZENGO PINDA	25	6	19	25		25	2		2	WV 29 WS 21	WV 6 WS 5	WV 13 WS 16	3	1	2
JML KATA	118	20	98	118		118	7	3	4	WV 92 WS 116	WV 24 WS 18	WV 88 WS 98	12	5	7

## 1.4 SAMANI

SHULE	MADAWATI			VITI			MEZA			SHUBAKA			KASIKI			KABATI		
	MAH	YA L	PU N	MA H	YA L	PU N	MA H	YA L	PU N	MA H	YA L	PU N	MA H	YA L	PU N	MA H	YA L	PU N
NYERERE	784	42 3	361	42	24	18	42	15	27	2	2		1		1	11	3	8
MSAKILA	461	23 5	226	33	15	8	25	10	15	3		3	1		1	11	2	9
MIZENGO PINDA	312	27 2	40	31	13	30	30	9	21	2	1	1	1		1	8	2	6
JML KATA	155 7	93 0	627	106	52	54	97	34	63	7	3	4	3		3	30	7	23

## HABARI ZA MIRADI SHULE ZA MSINGI

SHULE	AINA YA MRADI	KUANZA KUJENGWA	HATUA ILIYOFIKIWA	MAELEZO
NYERERE	-Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa -Ufyatujaji tofali za block	Februari 2018	Madarasa yamekamilika  Zimefyatuliwa tofali	Madarasa yamekamilika na yanatumika

MSAKILA	Ujenzi wa uzio wa shule	Marchi 2018	Sehemu ya kuingilia (Getini) imeshajengwa	Fedha inahitajika kukamilisha uzio huo
MIZENGO PINDA	Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na ofisi moja ya Mwalimu mkuu	Juni 2018	Ukusanyaji wa mawe Tripu 9 na michango ya wananchi inaendelea -Mchanga tripu tano zimeletwa	Ujenzi wa msingi umeanza hatua iliyofikia wametandaza mawe ¾ ya eneo lote la msingi

TAARIFA YA ROBO YA NNE (4) KILIMO APRIL - JUNE 2018

S/N	MAZAO	UKUBWA (h)	Sn	MAZAO	UKUBWA
1.	Mahindi	23.5	10	Pilipili	0.05
2.	Mpunga	0.5	11	Matango	0.05
3.	Mihogo	5.1	12	Mchicha	1.6
4.	Viazi vitamu	6.5	13	Chinese	1.5
5.	Magimbi	0.6	14	Nyanya	2
6.	Miwa	1.5	15	Nyanya chungu	0.05
7.	Alizeti	2.5	16	Bamia	0.6
8.	Karanga	6.5	17	Vitunguu	2.5
9.	Maharagwe	9			
	Jumla				9.35

Jumla ya eneo lililolimwa msimu wa kilimo 2017/2018 kata ya Kawajense ni ekari 65.25;

- Hali ya chakula ni nzuri mazao yanapatikana pia bei ya chakula ni nzuri mfano mahindi yanapatikana kwa Tsh. 350 1=kg

MIFUGO

MFUGO	Ng'ombe wa kisasa	Ng'ombe wa kienyeji	Mbuzi	Kondoo	Nguruwe	Kuku	Bata	Njiwa	Mbwa
IDADI	54	31	77	4	90	1184	368	234	74

SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

TAARIFA ZA MAKUNDI MAALUM KATA YA KAWAJENSE

MTAA	WALEMAVU			WAZEE			WATOTO WAISHIO MAZINGIRA HATARISHI		
	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML
KAWAJENSE	5	13	18	51	88	139	50	77	127
IKULU	15	22	37	42	76	118	44	59	103
MAJENGO MAPYA	6	1	7	51	54	105	7	8	15
JUMLA	26	36	52	144	222	362	101	144	245

- Jumla ya vikundi katika kata ni 40
  - Vikundi vya wanawake ni 26
  - Vikundi vya vijana ni 7
  - Vikundi mchnganyiko ni 7
- Vikundi vilivyopata mkopo jumla 9.
  - Wanawake 8 na vijana 1.
- Mkopo ngazi ya Halmashauri vikundi 6, wanawake 5 na vijana 1.
- Mkopo ngazi ya kata vikundi 3 vya wanawake vilivyomaliza mkopo ni vitatu ambavyo ni Kwaito, Katwezye na Nakilima.
- Kati ya vikundi 9 vilivyopata mkopo vikundi 7 vimemaliza marerejesho vya wanawake na vikundi 2 bado vipo kwenye marejesho ambapo 1 cha vijana na wanawake 4.
- Day care centre katika kata zipo 4 ambapo 1 imesajiliwa na 3 zipo kwaAenye mchakato wa usajili.



## ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama ni ya kuridhisha kwani matukio ya wizi yamepungua. Na jamii inaendelea kuelimishwa juu ya kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili kutokomeza kabisa wizi.

## UKIMWI

Katika kata ya Kawajense wananchi wanaendelea kupatiwa elimu juu ya kujikinga na VVU na Ukimwi kupitia vikao na vikundi mbalimbali kama vile SHIDEPHA+ na mradi wa Anglikana wa kizazi kipya wanaopita kwenye kaya mojamoya na kutoa elimu juu ya kujikinga na VVU na Ukimwi.

Pia makundi haya yameteua watu maalumu wanaopita kwenye kaya mbalimbali na kutoa elimu na kupata taarifa za wanaoishi na VVU na Ukimwi na kuwaelimisha.

## MAFANIKIO

- Tumeweza kujenga madarasa matatu shule ya msingi Nyerere.
- Tumeweza kusomba mawe tripu tisa (9) shule ya msingi Mizengo Pinda.
- Tumeweza kujenga choo cha ofisi ya kata na kukamilisha.
- Kamati ya kudhibiti Ukimwi iko hai na hukutana kila baada ya miezi mitatu

## CHANGAMOTO

1. Upungufu wa vyumba vya madarasa mahitaji ni vyumba 118 yaliyopo 23 pungufu 95 kulingana na idadi ya wanafunzi 4639.
2. Upungufu wa vyoo vya walimu na wanafunzi mahitaji matundu 208 yaliyopo 42 pungufu 76 uwiano wa vyoo ni wasichana 1:20 wavulana 1:25.
3. Ukosefu wa nyumba za walimu kwa kata nzima ambapo mahitaji ni nyumba 68 hakuna hata moja.
4. Ukosefu wa vidhibiti mwendo katika barabara zinazozunguka shule zote hata kusababisha ajali za mara kwa mara kwa wanafunzi mfano shule ya msingi Nyerere.
5. Mwitikio hasi wa wazazi kuchangia chakula cha mchana shuleni.
6. Upungufu wa walimu, kata ina waalimu 68 na pungufu 55. Jumla ya wanafunzi ni 4639 hivyo kwa uwiano 1:40 tunahitaji walimu 123 waliopo ni 68 upungufu ni 65.
7. Mwitikio hasi wa wazazi/jamii katika kuchangia ujenzi wa miundo mbinu ya shule kwani pamoja na kutoa ufafanuzi kuhusu sera ya elimu bure bado kuna wazazi ambao bado ni wagumu kuelewa.
8. Utoro wa wanafunzi bado ni kikwazo katika kufanikisha malengo ya ufaulu wa juu.
9. Mahitaji ya madawati kwa kata ni 1557 yaliyopo ni 930 pungufu 627 hii inasababishwa na upungufu wa madarasa.

## UFUMBUZI WA CHANGAMOTO

1. Kutokana na changamoto namba 1,2,3,5,6 na 7 Kata imepanga kufanya mikutano ya hadhara katika mitaa yote mitatu kutoa Elimu na hamasa juu ya uchangiaji wa ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu. Uchangiaji madawati na chakula cha mchana shuleni ili wananchi waweze kuchangia kwa hiari.
2. Kuwataarifu TARURA na TANROAD kuangalia barabara zote zinazozunguka shule zetu na kuziwekea vidhibiti mwendo kuzuia ajali.
3. Mamlaka husika kuongeza waalimu kulingana na mahitaji ya kila shule.
4. Walimu wameelekezwa kuandaa orodha ya wanafunzi watoro kuiwasilisha Ofisi ya kata ili wafikishwe Baraza la kata na kuchukuliwa hatua za kisheria.

## NAOMBA KUWASILISHA

PIUS BUZUMALLE  
MHE. DIWANI KATA KAWAJENSE

## KATA YA KAZIMA

KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA

APRIL-JUNE 2018.

### UTANGULIZI

Mh. Mstahiki Meya , kata ya Kazima ni miongoni mwa kata kumi na tano (15) zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Kata hii kiutawala inaundwa na mitaa mitatu (3) ambayo ni.

- ❖ Mtaa wa Kazima
- ❖ Mtaa wa Rungwa
- ❖ Mtaa wa Kapalangao

### IDADI YA WATU NA MAKAZI.

Kata ya kazima inajumla ya wakazi wapatao **12,270** kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya zoezi kwa mchanganuo ufuatao.

JINA LA KATA	MAJINA YA MITAA	ME	KE	JUMLA
KAZIMA	MTAA WA KAZIMA	2262	2579	4841
	MTAA WA KAPALANGAO	1592	1939	3531
	MTAA WA RUNGWA	1896	2002	3898
<b>JUMLA</b>		<b>5750</b>	<b>6520</b>	<b>12270</b>

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi **2012**. Kata hii ya Kazima inajumla ya kaya **2575**, Zenye wakazi **12270** ambapo kati yao wanaume **5750** na wanawake wapatao **6520**.

Katika mwaka wa fedha **2017/2018**. Kata ilikisia kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs 1,472,767,624** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

### 1.2. MAPATO.

Kwa kipindi cha mwezi **Aprili** hadi **June** 2018. Kata imekusanya na kupokea kiasi cha **Tshs 7,983,216/=** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani ya Halmashauri ambayo ni sawa na Asilimia ya makadilio ya **Tshs 1,472,767,624** kwa mwaka.

### 1.3. MATUMIZI.

Kwa kipindi cha mwezi **Aprili** hadi **June** 2018. Kata imetumia kiasi cha **7,500,00/=** katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

### MCHANGANUO WA TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI JUNE 2018

N O.	JINA LA MRADI/SHUGHULI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA TOLEWA	FEDHA TUMIKA	FEDHA BAKI BENKI	MAELEZO
1	Ujenzi wa choo shule ya Msingi Mkapa	Mfuko wa jimbo	1,000,000/=	1,000,000		Ujenzi wa boma la choo matundu 16 umekamilika
2	Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa na Ofisi moja (1)	<ul style="list-style-type: none"><li>• Mfadhili SRSG MAGAMBA</li><li>• Maendeleo ya Kata</li><li>• Nguvu za wananchi</li></ul>	6,000,000 1,483,216/= 500,000/=	6,000,000/= 1,000,000/=	483,216/=	Hatua ya ujenzi wa boma unaendelea

			500,000/=	483,216/=	
	Jumla ndogo		7,983,216/=	7,500,000/=	483,211/=
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>7,983,211/=</b>	<b>7,500,000/=</b>	<b>483,216</b>

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII ROBO YA NNE APRIL-JUNI 2018**

NA	LENGO	SHUGHULI	UTEKELEZAJI	CHANGAMOTO /MAFANIKIO
1	Utoaji wa huduma bora za kiuchumi kwa usawa	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kutoa maelekezo ya jinsi ya kuandika barua ya maombi ya mkopo kwa vikundi</li> <li>Kutembelea vikundi na kukagua miradi yao</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jumla ya vikundi <b>4</b> viliandika barua ya mkopo ambayo ni Magufuli na Maendeleo, warungwa, Faru group na Amkeni.</li> <li>Vikundi <b>4</b> vilitembelewa na kukaguliwa shughuli za miradi yao ambavyo ni Tumaini Agriculture na Faraja</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Vikundi hivi vinatarajia kupata mkopo tobo ya nne mwezi huu.</li> <li>Vikundi vingine vinafanya shughuli za kilimo mbali na nje ya Mji hivyo kuna umbali wa kufika kukagua shughuli hizo</li> </ul>
		Nimefanya ziara ya kutoa elimu ya vikundi kwa watoa huduma ngazi ya jamii ya shirika la ACT	Ziara hii ilifanyika katika Kata <b>15</b> za Manispaa kwa muda wa wiki moja. Taarifa imeambatanishwa na nipoti hii	Nilifanikiwa kutoa elimu hiyo iliyo kusudiwa na pia tuliweza kutatua changamoto mbalimbali
2	Kuimalisha huduma za utawala wa sheria na utawala bora	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuhamasisha wananchi kufuata sheria .</li> <li>Zoezi la uandikishaji wa vitambulisho vya utaifa</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Nimeelimisha viongozi mbalimbali wa Kata katika mikutano <b>2</b> ya ndani kuhusu matumizi ya sheria katika utatuzi migogoro ya kesi mbalimbali ili kuboresha utawala bora.</li> <li>Wananchi kwa asilimia kubwa wanauelewa juu ya utwala wa sheria kwa sababu hufika Ofisini kulipoti migogoro yao.</li> <li>Ambapo fomu zimeshagawiwa kwa wananchi wote wenye vigezo</li> </ul>	<p>Zoezi hili lilifanikiwa</p> <p>Zoezi hili linaendelea</p> <p>Zoezi hili lilifanikiwa</p>
3	Kuimarisha maswala ya jinsia na utawala bora	Kaya za walengwa wa mazingira hatarishi na VVU/UKIMWI zilitembelewa	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kaya 27 ziliweza kutembelewa</li> <li>Rufaa 15 zilitolewa kwa mlengwa aliye hitaji huduma tofauti tofauti</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Baadhi ya kaya wanahama kutoka sehemu mmoja kwenda nyingine bila kutoa taarifa kwa watoa huduma</li> </ul>
		Vikundi vilivyo kopeshwa vinaendelea na marejesho	<ul style="list-style-type: none"> <li>Vikundi vitatu vinaendelea na marejesho ambanyo ni:- amkeni , faruna Tushikamane ambapo kikundi kimoja kimemaliza mkopo huo ambacho ni magufuli na maendeleo</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Zoezi la urejeshaji mikopo katiika Kata linaendelea vizuri</li> </ul>
		<ul style="list-style-type: none"> <li>Huduma mbalimbali ziliweza kutolewa</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Huduma hizo ni kama elimu ya lishe, Uchizi na</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Zoezi lilifanikiwa</li> </ul>

		katika kaya 27 za watu wanaoshi katika mazigira hatarishi <ul style="list-style-type: none"> <li>• Nilisimamia kuunda jiwa Club ya Ukimwi nyerere</li> </ul>	usalama wa mtoto na elimu ya kujiinua kuichumi <ul style="list-style-type: none"> <li>• Club hiyo inajumla ya washi na ilizinduliwa na mwenge wa uhuru 2018</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Zoezi zililifanikiwa kwa asilimia kubwa</li> </ul>
4	Kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya HIV/AIDS	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Elimu ya umuhimu wa upimaji inaendelea mabapo watoa huduma ngazi ya jamii CCW hufanya upimaji kwa mtu aliyehiyari</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Baadhi ya kaya hizo wamefanya upimaji na ukikitwa na maambukizi hupewa rufaa kwenda (CCT)</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Zoezi linaendelea vizuri</li> </ul>

### HUDUMA ZILIZOPO

NA	HUDUMA KIUCHUMI ZA	HUDUMA ZA KIJAMII	SEKTA BINAFSI
1	Barabara	- Elimu ya Msingi/Sekondari	- Mashine za kusaga na kukoboa
2	Umeme (Nishati)	-Maji	- Maduka madogo madogo
3	Mawasiliano (Simu)	-Misikiti	- Migahawa midogo midogo
4	Soko la wakulima	-Makanisa	- Baa za pombe za kienyeji/kisasa

### 1.3 SHUGHULI ZA KIUCHUMI WANAZOFANYA WANANCHI WA KATA HII.

1. Biashara ndogondogo
2. Kilimo
3. Ufugaji mdogomdogo
4. Ususi
5. Ufyatuuji wa matofali
6. Ushonaji na ujenzi
7. Wafanyakazi wa serikali na Mashirika.

### 2.0 KILIMO NA MIFUGO.

NA:	AINA YA MAZAO	ENEO LILILOPANGWA	MAVUNO (TANI)	MAZAO YA BUSTANI	MAVUNO TANI
1	MAHINDI	42.5 (HA)	106.25	PILIPILI	0.5-0.6
2	MPUNGA	6.5	22.75	MATANGO	0.5-5
3	MTAMA	1.8	2.7	MCHICHA	0.6-0.48
4	MIHOGO	4.8	48	CHINESE	3.5-4.2
5	VIAZI VITAMU	9.5	95	NYANYA	2.5-15
6	GIMBI	2	16	NYANYA CHUNGU	0.2-1.4
7	PAMBA	1.0	1.3	PAPAI	0.9-13.5
8	MIWA	4.6	6.9	TIKITI MAJI	1.2-2.4
9	KOROSHO	2	2.2	JUMLA	6.4.18 (TANI)
10	ALIZETI	1.5	2.1		
11	KUNDE	1.0	1.1		
12	KARANGA	5.7	8.55		
13	NJUGU MAWE	1.6	2.56		
14	MAHARAGE	5.3	7.95		
	<b>JUMLA</b>	<b>89.8</b>	<b>323.36 (TANI)</b>		

Jumla ya eneo lililolimwa msimu wa kilimo **2017/2018** Kata ya Kazima ni **106.9** hekta. Hali ya chakula ni nzuri mazao yanaendelea kuvunwa. Pia bei ya chakula ni nzuri mfano Mahindi yanapatikana kwa Tsh. 325/= kwa kilo, shamba darasa lipo katika hatua ya kuvunwa.

### **SEKTA YA MIFUGO.**

Walimu wa kata hii hujishughulisha na ufugaji wa mifugo mbalimbali kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini.

<b>AINA YA MIFUGO</b>	<b>NG'OMBE WA MAZIWA KISASA</b>	<b>NG'OMBE WA MAZIWA KIENYEJI</b>	<b>MBUZ I</b>	<b>KONDO O</b>	<b>NGURUWE</b>	<b>KUKU</b>	<b>MBWA</b>	<b>BATA</b>	<b>NJIWA</b>
IDADI	46	105	457	54	297	2351	130	809	254

### **2.5 SEKTA YA MAJI.**

Kata ya Kazima ina kisima kirefu kimoja kirefu na kifupi kimoja vyote hivi vipo mtaa wa kazima na gati moja la bomba la maji lililopo katika eneo la yelusallemu mtaa wa Kalangao.

### **CHANGAMOTO.**

Kata ya Kazima ni moja ya eneo lenye shida kubwa ya maji ukilinganisha na idadi ya watu kama inavyoonekana katika jedwali na idadi ya watu wa makazi hivyo kuna hitajika jitihada za makusudi katika kutandaza mabomba na uchimbaji wa visima vya maji katika eneo hilo.

### **SEKTA YA AFYA.**

Kata ya Kazima haina kituo cha afya wala zahanati hivyo kupelekea wakazi wa kata hii kulazimika kupata huduma za afya katika vituo vyqa watu binafsi ambavyo ni ghali sana.

### **B. AFYA KINGA.**

Ofisi ya kata kwa kushirikiana na wataalamu waliopo katika kata hii pamoja na viongozi wa serikali za mitaa huratibu na kusimamia usafi wa mazingira kwa kudhibiti uchafu katika Kata. Pamoja na jitihada hizo tunaendelea kuwafundisha wakazi umuhimu wa kutunza mazingira na usafi kwa ujumbe na ujenzi wa vyoo bora.

### **CHANGAMOTO.**

Maeneo mengi katika kata hii kutopimwa kupelekea kutokuwa na eneo maalum la ukusanyaji wa mifumo ya maji hapa kipindi cha mvua hususani mitaa ya kazima na Kapalangao.

### **2. SEKTA YA ELIMU.**

Kata ya Kazima ina shule mbili (2) Mkaipa shule ya msingi na Rungwe Sekondari

**SHULE YA MSINGI MKAPA.  
TAARIFA YA WANAFUNZI**

<b>SHULE</b>	<b>IDADI</b>		<b>AWALI</b>		<b>I</b>		<b>II</b>		<b>III</b>		<b>IV</b>		<b>V</b>		<b>VI</b>		<b>VII</b>	
MKAPA	WV	WS	WV	WS	WS	WV	WS	WV	WS	WV	WS	WV	WS	W V	WS	WV	WS	WV
	1183	1289	149	201	270	276	228	219	161	188	112	131	109	99	88	104	65	72
<b>JML</b>	<b>2,472</b>		<b>350</b>		<b>546</b>		<b>447</b>		<b>349</b>		<b>243</b>		<b>208</b>		<b>192</b>		<b>137</b>	

**IDADI YA WALIMU.**

MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
45	21	24

**MAJENGO YA SHULE /MIUNDO MBINU YA SHULE.**

MAELEZO	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
MADARASA	52	08	43
NYUMBA ZA WALIMU	21	01	20
OFISI	6	2	4
MATUNDU YA VYOO	92	11	81
STOO	2	-	2

**SAMANI ZA SHULE**

AINA	MAHITAJI	VILIVYOPO	PUNGUFU
MEZA	21	11	10
VITI	21	14	7
MADAWATI	686	566	120
KABATI	6	2	4

**(B) ELIMU YA SEKONDARI**

Kata Kazima ina Shule ya Sekondari moja ambayo ni Sekondari ya Rungwa.

**IDADI YA WANAFUNZI.**

ME	KE	JUMLA
487	463	950

**2. IDADI YA WALIMU.**

Shule ya sekondari Rungwa ina walimu wafuatao.

MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
33	41	-

Katika takwimu hizi za walimu tatizo lipo kwa masomo ya Sayansi ambapo kuna upungufu wa walimu watatu **(3)**

**MIUNDOMBINU YA SHULE.**

AINA	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
MADARASA	26	23	3
NYUMBA ZA WALIMU	41	2	39
OFISI	-	-	-
STOO	2	-	2
MEZA/VITI	41	20	21
VITI/MEZA/WANAFUNZI	1,041	894	147
VYOO MATUNDU	33	20	13
BWALO	1	-	01
MAKTABA	1	-	01
MABWENI	2	2	-
JENGO/UTAWALA	01	-	01
MAABARA	4	3	1
JIKO	1	1	-

Changamoto upande wa Rungwa sekondari eneo ni dogo sana kiasi kwamba hakuna hata viwanja vya michezo. Hivyo tunaomba liongezwe ili kukidhi mahitaji yote yanayotakiwa katika utoaji wa elimu.

Utatuzi wa changamoto tunaishauri ofisi ya Mkurugenzi kutoa ushirikiano juu ya mgogoro wa ardhi katika eneo la Rungwa Sekondari.

### **IDADI YA WATUMISHI WALIOPO KATANI.**

UATAWAL A		ELIMU/MSINGI SEKONDARI		NA		KILIMO /MIFUGO		M/JAMII		AFYA		MISITU		JUMLA
ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME\$KE
2	2	35	27	1	1	-	1	-	-	-	-	-	-	69

OMBI; Tunaomba tupatiwe Afisa wa Afya wa kata ya Kazima.

### **ULINZI NA USALAMA.**

Hali ya ulinzi na usalama kwa kipindi hiki katika kata ni ya wastani kwani vikao vinaendelea kufanyika katika kuhamasisha ulinzi na usalama wa wananchi wamejiwekea utaratibu wa ulinzi shirikishi katika maeneo yao Hakuna matukio makubwa yanayojitokeza kwa kipindi hiki.

### **UTAWALA BORA.**

Kwa kipindi cha April –June 2018. Vikao mbalimbali vimefanyika vikiwemo mikutano ya hadhara, katika vikao hivyo kero mbalimbali na malalamiko mbalimbali vimeshughulikiwa.

### **IDADI YA VIKAO**

VIKAO VYA WDC			VIKAO VYA S/MITAA			MIKUTANO YA HADHARA		
KAWAIDA	MAALUM	JUMLA	KAWAIDA	MAALUM	JUMLA	KAWAIDA	MAALUM	JUMLA
1	-	1	3	2	5	3	-	3

### **CHANGAMOTO.**

- Kata ya kazima haina jengo la ofisi hivyo shughuli zote za ofisi bado zinafanyika kata ya Kawajense kiasi ambacho kinapelekea wananchi kushindwa kuhudumiwa kutokana na umbali
- Ukosefu wa miundombinu ya Barabara mifereji ya maji
- Ukosefu wa maji safi na salama

### **ELIMU YA URAIA NA UTAWALA BORA.**

Wananchi wanaendelea kupewa elimu ya uraia na utawala bora katika mikutano ili waweze kuelewa wajibu wao na majukumu ya serikali katika kuleta maendeleo. Aidha elimu ya mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na ukimwi kupewa kipaumbele kwani serikali ya awali ;ya tano imeamua kushughulika na matatizo hayo

### **RUSHWA NA UBADHIRIFU**

Wananchi kila mkutano wa hadhara wamekuwa wakielimishwa umuhimu wa kuwafichua wanaotoa na kupokea rushwa na wabadhilifu wa mali za umma.

Na wale wanaosemwa semwa hatua huchukuliwa ili wahudumie wananchi na kuwapa wananchi uhuru wa kutoa mawazo yao, na sasa hivi wananchi walio wengi wanaimani na serikali yao ya awamu ya tano (5) kwa kutoa huduma ipasavyo.

### **UKIMWI.**

Viongozi na wataalamu wamefanya mikutano ya hadhara na kutembelea baadhi ya maeneo, kutoa tahadhari ya ugonjwa huu hatari ambao hauna dawa na kuwasisitiza kupima afya zao mara kwa mara na kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu au kuacha kabisa ngono zembe na kutumia salama.

NAOMBA KUWASILISHA



## **KATA YA MAGAMBA**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KATA YA MAGAMBA ROBO YA NNE KUANZIA MWEZI WA 4/2018 HADI MWEZI WA 06/2018

### **UTANGULIZI**

Kata ya magamba ni miongoni mwa kata zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, vijiji vya kata hii ya Magamba ni

1. Magamba
2. Mtakumbuka
3. Makongoro
4. Society
5. Dirifu

### **Idadi ya wakazi**

Kata ya Magamba ina wakazi 7864 Me 4044 na Ke 3820 na ina kaya 1479 kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012.

### **Mipaka ya kata idadi ya vijiji, vitongoji na wakazi wake**

#### **i. Mipaka ya kata**

Upande wa Kaskazini inapakana na kata ya Ilembo, upande wa kaskazini Magharibi inapakana na kata ya Misunkumilo, na Magharibi inapakana na kata ya Itenka, upande wa Kusini inapakana na kata ya Machimboni upande wa mashariki Stalike inapakana na kata ya Kapalala upande wa kaskazini mashariki inapakana na kata ya Mtapenda na uwanja wa ndege.

#### **ii. Idadi ya vijiji na Vitongoji kata na Tarafa**

<b>KATA</b>	<b>KIJIJI</b>	<b>KITONGOJI</b>
<b>MAGAMBA</b>	MAGAMBA	• Migazini
		• Ntakata
		• New-camp
		• Ikulu
		• Beling
		• Burunga
	MTAKUMBUKA	• Kabatini
		• Igonda
		• Mtakumbuka kati
		• Mkakumbuka kusini
		• Mtakumbuka kaskazini
		• Mtakumbuka mashariki

	MAKONGORO	• Mailikumi	
		• Igalukilo	
		• Makongoro	
		• Kanondo	
		• Mlimani	
	SOCIETY	• Njia panda	
		• Mwenge	
		• Ikulu	
		• Society	
		• Mafuanguo	
	DIRIFU	• Msangama	
		• Kagela	
		• Kamsofu	
		• Ikulo	
		• Mkuyuni	
		• Lumuka	
	<b>JUMLA YA VIJIJI 5</b>		<b>VITONGOJI 28</b>

**iii. Idadi ya Ofisi za vijiji, Kata na Tarafa**

IKAMA	KATA	KIJIJI	TARAFU
MAHITAJI	1	5	1
ZILIZOPO	0	3	1
PUNGUFU	1	2	-
ZIADA	-	-	-

**iv. Uongozi wa kata na vijiji**

1. Mh diwani wa kata (1)
2. Afisa mtendaji wa kata (0)
3. Maafisa kilimo na mifugo (3)
4. Wenyeviti wa vijiji (3)
5. Watendaji wa vijiji (2)

**Idadi ya watumishi, sekta mbalimbali ngazi ya kata**

IKAM A	UTAWAL A	ELIMU YA MSING I	ELIMU YA SEKONDA RI	ULINZI NA USALAM A	MAENDELE O YA JAMII	AFY A	KILIM O
Mahitaji	6	50	20	4	6	16	6
Waliopo	2	36	16	2	-	6	3
Pungufu	4	14	4	2	6	10	3
Ziada	-	-	-	-	-	-	-

**v. Shughuli za Kiuchumi**

- Kilimo cha jembe la mkono
- Biashara ndogondogo
- Ufugaji mdogomdogo
- Uchimbaji wa madini aina ya Dhahabu

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA KATA**

I. Taarifa ya miradi na fedha (mapato na matumizi)

• **UTEKELEZAJI WA MIRADI**

KATA	ENEO LA MRADI	AINA YA MRADI	CHAN ZO CHA FEDH A	MCHAN GO WA JAMII	ILİYOTOL EWA	ILİYOTUM IKA	ILİYOBA KI	HATU A YA MRAD I	MAELE ZO
MAGAM BA	S/Msing i makong oro	Vyumba 2 vya madaras a na ofisi	Halma shauri	Tofari mchang a na mawe	17,500,000/ =	5,036,000/ =	12,464,00 0/=	Upigaji lipu	Kazi inaende lea
	Makong oro	Upauaji na ujenzi wa	Halma	Tofari	2,700,000/ =	13,336,000	1,364,000/ =	Jengo lipo hatua	Kazi inaende

	matundu 8 ya vyoo	shauri	na mchang a	=	/=	=	ya boma	lea
Magamba	Machinjio ya kisasa	Halma shauri	-	284,000,00 0/=		284,000,0 00/=	Maand alizi ya mradi	Mradi bado haujaan za

## II. Taarifa ya kilimo na mifugo

Kata ya magamba ina jumla ya maafisa wa kilimo na mifugo 3, katika robo ya nne wameweza kuwatembelea wakulima 117 na wafugaji 68 na kutoa ushauri wa kuzingatia kanuni bora za kilimo na ufugaji bora wa kuleta tija. Lifuatalo ni jedwali kuonesha idadi ya wakulima na wafugaji waliotembelewa kutoa ushauri huo.

JINA LA KIJIKI	IDADI YA WAKULIMA WALIOPEWA USHAURI	IDADI YA WAFUGAJI WALIOPEWA USHAURI
Magamba	26	21
Society	19	-
Makongoro	20	12
Dirifu	34	26
Mtakumbuka	18	9

Pia wameweza kufanya ukaguzi wa nyama kama inavyoonesha chini ya jedwali

Aina ya mifugo	Idadi ya waliochinjwa na kukaguliwa	Bei ya wastani
Mbuzi	15	6,000/=
Ng'ombe	94	6,000/=
Nguruwe	12	6,000/=

## III. Taarifa ya vikao na mikitano

kwa kipindi cha robo ya nne tumefanikiwa kufanya mikitano 03 na vikao 11 sawa na asilimia 75% ya kufanikisha lengo. Kama inavyoonesha chini ya jedwali

Vijiji	Idadi ya mikitano	Idadi ya vikao
Mtakumbuka	1	3

Makongoro	1	1
Society	1	3
Magamba	-	2
Dirifu	-	2

Pia katika robo ya nne tumefanikiwa kufanya kikao kimoja (1) cha kamati ya Ukimwi kata iliyokaa na kujadili Agenda nne kama ifuatavyo;-

1. Kufungua kikao
2. Kujadili njinsi ya kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU)
3. Mengineyo
4. Kufunga kikao

Kama ilivyowailishwa katika muhtasari wa kikao kilichoketi tarehe 17/07/2018

#### **IV. Taarifa ya mazingira na vyanzo vya maji**

Kata ya magamba ina jumla ya jumuiya 5 za watumia maji zenye usajiri wa watumia maji Mpanda pia katika utafiti uliofanyika robo ya tatu ya uchimbaji wa visima vitatu katika kijiji cha Makongoro, Magamba na society watafiti wao wameweza kuchimba kisima kimoja katika kijiji cha Magamba kitongoji cha Ntakata kazi inaendelea.

#### **V. Maendeleo ya jamii**

Tunavyo vikundi 6 vilivyosajiliwa kata ya Magamba aidha vikundi 4 vimesajiliwa kutipia Halmashauri ya Manispaa Mpanda na vijiji 2 vimesajiliwa kupitia Halmashauri ya wilaya Nsimbo. Kupitia kikao cha WDC kilichoketi tarehe 10/07/2018 kiliona ni vyema kupitisha barua ya maombi ya kujitolea katika ngazi ya Afisa Maendeleo ya Jamii ili kuwezesha huduma ya vikundi na maendeleo kuwa yenye tija.

### **C. TAARIFA ZINAZOHUSU HALI YA KATA**

#### **I. ELIMU**

Kata inajumla ya shule 5 za idara ya msingi na sekondari yaani shule nne za msingi na shule moja ya sekondari.

#### **IDADI YA WALIMU -MSINGI**

ME	KE	JUMLA
18	17	36

#### **IDADI YA WALIMU –SEKONDARI**

ME	KE	JUMLA
12	4	16

**MIUNDOMBINU  
VYUMBA VYA MADARASA**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>VILIVYOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
S/M MAGAMBA	15	9	6
S/M MTAKUMBUKA	10	7	3
S/M DIRIFU	11	9	2
S/M MAKONGORO	5	2	3
MAGAMBA SEKONDARI	16	8	8

**NYUMBA**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>VILIVYOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
S/M MAGAMBA	21	6	15
S/M MTAKUMBUKA	18	5	13
S/M DIRIFU	16	4	12
S/M MAKONGORO	11	1	10
MAGAMBA SEKONDARI	18	3	15

**VYOO VYA WANAFUNZI**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>VILIVYOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
S/M MAGAMBA	24	18	6
S/M MTAKUMBUKA	16	7	9
S/M DIRIFU	16	6	10
S/M MAKONGORO	10	2	8
MAGAMBA SEKONDARI	28	18	10

**VYOO VYA WALIMU**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>VILIVYOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
S/M MAGAMBA	2	2	-
S/M MTAKUMBUKA	2	-	2
S/M DIRIFU	2	-	2
S/M MAKONGORO	2	-	2
MAGAMBA SEKONDARI	4	4	-

**MADAWATI**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>VILIVYOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
S/M MAGAMBA	256	220	36
S/M MTAKUMBUKA	166	107	59
S/M DIRIFU	182	148	34
S/M MAKONGORO	96	64	32

**MAABARA**

<b>SHULE</b>	<b>MAHITAJI</b>	<b>ZILIZOPO</b>	<b>PUNGUFU</b>
CHEMISTRY	1	1	-
BIOLOGY	1	1	-
PHYSICS	1	1	-

## VIWANJA VYA MICHEZO SHULENI

SHULE	MAHITAJI	VILIVYOPO	PUNGUFU
S/M MAGAMBA	5	2	3
S/M MTAKUMBUKA	5	1	4
S/M DIRIFU	5	2	3
S/M MAKONGORO	5	1	4
MAGAMBA SEKONDARI	5	1	4

Aidha kamati ya maendeleo ya kata inatarajia kuanzisha mradi wa madarasa mawili (2) shule ya sekondari Magamba ambapo katika vijiji 5 vinavyounda kata hiyo michango inaendelea baada ya kufuata taratibu za vikao na mikutano ya wananchi.

### II. Afya

Tunazo Zahanati 2 zilizopo katika kijiji cha Magamba na Mtakumbuka zinazohudumia vijiji hivyo na vijiji vingine jirani.

#### ❖ Idadi wa watumishi wa afya na miundombinu yake

	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
Watumishi	12	6	6
Nyumba	12	6	6
vyoo	8	4	4

### III. Matukio

Kata ya magamba ina jumla ya matukio kadhaa yaliyotokea katika robo ya nne yafuatayo ni watukio

- Tukio la kitaifa la uwandikishaji wa vitambulisho vya Taifa lililofanyika tarehe 4/06/2018 hadi 6/06/2018 na jumla ya wananchi 4800 walifanikisha zoezi la upigaji picha.
- Wizi mdogomdoto unaowafanya watu kutokuwa na amani na mali zao
- Kuchinjwa kwa bodaboda mmoja kijiji cha Magamba
- Tembo kuingia katika eneo la kijiji na kufanya uharibifu katika mashamba ya viazi na mahindi.

### IV. Ziara za Viongozi

- ❖ 29/07/2018 Mh diwani kufanya mkutano katika kijiji cha Makongoro kusikiliza kero za wananchi

### V. Ulinzi na usalama

Kata ya Magamba imeweza kuunda kamati ya miundombinu ya ulinzi na usalama na vikao vyake kufanyika mara kwa mara ili kuimalisha ulinzi na usalama wa kata hiyo.

## **VI. Changamoto**

1. Ukosefu wa usafiri kulingana na geografia ya kata na umbali kutoka kijiji kimoja na kijiji kingine.
2. Ukosefu wa nishati ya umeme
3. Wananchi kukataa ulinzi shirikishi kwa hiyari yao
4. Wajumbe kutohudhuria vikao vya serikari ya kijiji kwa wakati
5. Ud hululaji wa mifugo na kusababisha kero kwa wakulima
6. Bei ya dawa ya mifugo na viwatilifu kuwa juu
7. Kutokuwepo kwa mabucha yenye sifa stahiki kwa ajili ya kuuzia nyama

## **VII. Utatuzi wa changamoto hizo**

1. Halmashauri itenge bajeti ya upatikanaji wa usafiri hata kwa kukata asilimia ya mishahara yetu.
2. Kuendelea kutoa elimu juu ya faida ya ulinzi shirikishi.
3. Kukamata mifugo yote inayodhulula na kutoza faini kwa wahusika wa mifugo.
4. Kutoa elimu ya uwepo wa mabucha na kuzuia kuendelea kwa biashara kwa kutokidhi vigezo.

Naomba kuwasilisha,

**MHE.PHILIP J. KALYALYA**  
**DIWANI KATA YA MAGAMBA**



## KATA YA MAKANYAGIO

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017-2018 KWA KIPINDI CHA MWEZI APRIL – JUNI 2018

### UTANGULIZI.

1. Kata ya Makanyagio inaundwa na mitaa **(5)** ambayo ni mtaa wa **Makanyagio, Kigoma, Kachoma, Mwangaza** na mtaa wa Mpadeco na ni miongoni mwa Kata **9** zinazounda tarafa ya Kashaulili katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Mkoa wa Katavi.
2. Kata ya Makanyagio ina jumla ya kaya **3048** zenye jumla ya wakazi wapatao **15823** kati yao wanaume **6,325** na wanawake **9498**.
3. Kata ya Makanyagio ina jumla ya Shule **2** za Msingi na **2** za Sekondari, na Zahanati **1** ya mtu binafisi.

### MIPAKA YA KATA.

- Makanyagio kwa upande wa mashariki imepakana na Kashaulili
- Upende wa kusini imepakana na Kata ya Majengo na M/Hotel.
- Upande wa magharibi imepakana na Kata ya Misunkumilo
- Upande wa kaskazini imepakana na Kata ya shanwe.

### MCHANGANUO WA WAKAZI

KAYA	IDADI YA WATU			WENYE UWEZO WA KAZI			WASIO UWEZO KAZI			NA WA	WALEMAVU			WATOTO UMRI 0-17		
	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML		ME	KE	JML	ME	KE	JML
3048	6325	9498	15823	5870	8806	14676	458	689	1147	5	10	15	2385	3569	5954	

### SHUGHULI ZA KIUCHUMI.

- Wananchi wa Kata ya Makanyagio wanajishughulisha na biashara kubwa na ndogo (wajasiriamali). Vilevile wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula kama vile **mpunga, mahindi** na **karanga** shughuli hizo hufanyika nje ya Kata kama **Kasokola, Kakese, Kabungu** n.k

### IDADI YA WATUMISHI KATA YA MAKANYAGIO.

UTAWALA		ELIMU YA MSINGI		ELIMU YA SEKONDARI		KILIMO NA MIFUGO		AFYA		MAENDELEO YA JAMII	
ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE
1	3	15	28	27	14	-	2	1	-	-	1

### HUDUMA ZA JAMII ZILIZOPO

Kata ya Makanyagio inahuduma za kijamii zinazomilikiwa na Serilikali, Makapuni na watu Binasi

#### A. ELIMU

- Shule za msingi 2 Kashato na Katavi
- Shule za sekondari 2 Mwangaza na Istiqama

#### B. HUDUMA ZA MAWASILIANO

Minara ya kunasia mawasiliano:-

- Voda minara 2
- Hallotel mnala 1
- Barabara

## SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

- Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuunda vikundi vya wakina mama vijana kufanya shughuli za ujasiriamali kupitia kilimo ufugaji
- Kutoa elimu juu ya kukopa na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kwa vikundi
- Vikundi vimeundwa na vinaendelea kukopa na kurejesha mikopo
- Vilevile kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia fedha na kusaidia makundi ya wasiojiweza katika huduma za jamii

## SHUKRANI KWA WADAU WA MAENDELEO MAKANYAGIO KUCHANGIA UENDELESHAJI SHUGHULI ZA UANDIKISHAJI VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

Kamati ya maendeleo ya Kata inatoa shukurani za dhati kwa wadau wa maendeleo kuchangia uendeshaji wa shughuli za uandikishaji vitambulisho vya Taifa (NIDA) wadau wameweza kuchangia jumla ya **Tshs. 715,000/=** tutakuwa wachoyo wa fadhila tusipo wataja kwa majina.

- **KASSCO KWA KUTUPATIA VIFUSI TRIP 4 @ Tshs. 120,000/= JUMLA TSHS. 480,000/=**

## MH: MBUNGE

Kamati inatoa shukurani kwa Mhe. Mbunge Ndugu Sebastian Kapufi kwa kushawishi na kuletewa fedha za madarasa matatu (3) Mwangaza Sekondari jumla ya Tshs. 60,000,000/=

### SEKTA YA KILIMO NA VIWANDA

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka April hadi Juni 2018 shughuli zilizotekelezwa.

- Kutoa elimu kwa wakulima wa mboga mboga kwa kutumia umwagiliaji (Bustani)
- Kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa kisasa
- Kutoa elimu juu ya chanzo ya mifugo na faida ya kuhifadhi kwa njia salama ili yasiharibiwe na wadudu
- Kuendelea Kuelimisha jamii juu ya upandaji wa zao la pamba na korosho (mazao ya Biashara) katika kipindi kijacho
- Kuendelea kutoa elimu kwa mwisho wa kilimo ndipo mwanzo wa maadalizi ya msimu ujao wa kilimo kwa kuandaa mashamba mapema
- Elimu ya maandalizi ya zao la biashara, korosho na pamba

## IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

SHULE	WALIMU			WANAFUNZI			MADARASA			MADAWATI			VYOO		
	ME	KE	JM L	ME	KE	JML	MA H	YA P	PUN G	MA H	YA P	PUN G	MA H	YA P	PUN G
KASHATO	86	15	21	57 2	55 8	113 0	31	9	22	329	309	30	18	18	-
KATAVI	6	15	21	78 2	77 6	155 8	38	9	29	460	460	0	28	7	21
MWANGAZ A	18	12	30	51 1	44 4	955	24	16	9	948	799	142	20	9	11
ISTIQAAMA	9	2	11	36	34	70	4	5	-	-	-	-	5	5	-

## WANAFUNZI WA ELIMU MAALUMU SHULE YA MSINGI KASHATO

S/N	WAVULANA	WASICHANA	JUMLA
1	15	10	25

## DARASA LA AWALI SHULE YA MSINGI KASHATO NA KATAVI

SHULE	WALIOANDIKISHWA		
	WV	WS	JML
KASHATO	77	68	145
KATAVI	89	90	179

## TAARIFA ZA MAPATO YA FEDHA ZA RUZUKU SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ROBO YA NNE YA MWAKA APRIL – JUNI 2018

SHULE	APRIL	MAY	JUNE
KASHATO	888,336.92	888,336.92	2,665,010.76
KATAVI	648,675.17	648,675.17	1,946,025.51
MWANGAZA	883,366	883,366	2,650,098

### SEKTA YA AFYA

Kata ya Makanyagio ina Zahanati moja ya mtu binafsi itambulikayo kwa jina la Afya Dispensari wananchi hupata huduma za matibabu hapo na Hospital ya Wilaya. Na madawa katika maduka ya watu binafsi ndani na nje ya Kata.

### HUDUMA ZA AFYA ZINAZOPATIKANA

1. Kuelimisha jamii katika shughuli za usafi wa mazingira kwa kila kaya na kujikinga na mbu waenezao malaria kwa kutumia chandaruwa kwa muda wote
2. Kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo safi na bora na kukitumia
3. Kutoa elimu ya kuchemsha maji ya kunywa na kunawa na sabuni kipindi wanapotoka chooni na wanapotaka kula chakula
4. Kuhakikisha taka ngumu zinazolewa na kupekwa kwenye Dampo kuu
5. Kukagua biashara zote na ziwe kwenye ubora unaoridhisha kwa muda wote ili kumkinga mtumiaji na mlaji
6. Kuhakikisha mamalishe wanapima afya zao kabla ya kuanza biashara
7. Kutoa elimu dhidi ya kujikinga maambukizi mapya ya UKIMWI (VVU).

### SEKTA YA MIUNDO MBINU

Kipindi cha April–Juni kata ya Makanyagio hali ya barabara nyingi zimehalibika na mvua hasa mtaa wa Mpadeco, Mwangaza na Makanyagio vilevile matengenezo ya barabara ya lami yanaendelea kipande cha kutoka afya Dispendari hadi Kigamboni na barabara itokayo afya Dispensari kwenda Ofisi ya zamani ya Kata

### ULINZI NA USALAMA

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka Aprili hadi Juni 2018 hakuna matukio ya uharifu yaliyojitokeza.

### TATIZO LA VIBOKO

Viboko kuzurula mitaani na kutishia usalama wa wananchi hivyo kamati ya ulinzi na usalama ya Kata kutoa taarifa kuangalia utaratibu wa kuondosha viboko hao wanaotoka bwawa la Milala.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 kata ilikisia kukusanya na kupokea kiasi cha **Tshs 91,975,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbili mbali za maendeleo

## MAPATO

Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2018 Kata kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato imeweza kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs. 88,182,884.27** na kufanya mapato yote toka Julai 2017 hadi Juni 2018 kufikia kiasi cha **Tshs. 134,484,820.36** mapato kuongezeka kwa **46%** ya makisio

## MATUMIZI

Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2018 kata imeweza kutumia kiasi cha Tshs **28,182,884.27** Katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na kufanya matumizi yote kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Juni 2018 kufikia Jumla Tshs **74,484,820.36**.

## MCHANGANUO WA MATUMIZI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI APRIL JUNI 2018

1. Uendeshaji wa taaluma (capitation) kwa shule za msingi **Tshs 4,611,036.27**
2. Uendeshaji wa taaluma (capitation) kwa shule ya sekondari **Tshs 2,650,098.00**
3. Jumla ya Tshs. 1,392,000/= zimetumika kwa ajili ya kuondosha taka ngumu hadi Dampo
4. Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 sekondari mwangaza Tshs 60,000,000/=
5. Umaliziaji wa maabara Mwangaza Sekondari Tshs 17,000,000/=
6. Mpango wa kunusuru kaya masikini (Tasaf III) Tshs 2,049,750.00

## VIKAO VILIVYOFANYIKA YA MTAA NA KATA

NA	KATA/MTAA	IDADI YA VIKAO			MIKUTANO MIKUU			KAMATI YA MAZINGIRA			KAMATI YA MALALAMIKO		
		hitajika	fanyika	%	Hitajika	fanyika	%	hitajika	Fanyika	%	hitajika	fanyika	%
	Kata (WDC)	4	4	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100
	Makanyagio	12	12	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100
	Kigoma	12	12	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100
	Kachoma	12	12	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100
	Mwangaza	12	12	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100
	Mpadeco	12	12	100	4	4	100	4	4	100	4	4	100

**MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI KWA KIPINDI CHA APRIL – JUNI 2018**

<b>KATA</b>	<b>MTAA</b>	<b>AINA YA MRADI</b>	<b>CHANZO CHA FEDHA</b>	<b>ILIYOPOKELEWA</b>	<b>ILIYOTUMIKA</b>	<b>ILIYOBAKI</b>	<b>HATUA YA UTEKELEZAJI</b>	<b>MAELEZO</b>
<b>MAKANYAGIO</b>	Kachoma	Mpango wa kunusuru kaya masikini	TASAF III	2,049,750.00	2,049,750.00	-	Walengwa wote wamelipwa	
	Shule ya msingi Kashato na Katavi	Uendeshaji wa shughuli za taaluma (Captation)	Halmashauri ya manispaa	4,611,036.27	4,611,036.27	-	Taaluma imeboreka	
	Mwangaza Sekondari	Uendeshaji wa shughuli za taaluma (Captation)	Halmashauri ya Manispaa	2,650,098/=	2,650,098	-	Taaluma imeboreka	
	Mitaa 2 Kigoma na Mpadeco	Uzoaji taka ngumu	Michango ya Wananchi	1,392,000/=	1,392,000/=	-	Taka zinasombwa Trip 8	
	Mitaa 5	Kusomba kifusi Trip 4 Shule ya Msingi Katavi na Kashato	Mhisani	480,000/=	480,000/=	-	Umaliziji wa boma	
	Mitaa 5	Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 Mwangaza Sekondari	Msaada wa nchi ya Uholanzi	60,000,000/=	-	60,000,000/=	Usawa wa renta	
	Mitaa 5	Umaliziji wa maabara Mwangaza Sekondari	P4R	17,000,000/=	17,000,000/=	-	Umaliziji unaendelea	
		<b>JUMLA KUU</b>	<b>TSHS</b>		<b>88,182,884.27</b>	<b>28,182,884.27</b>	<b>60,000,000</b>	

## **1. MIRADI INAYOENDELEA KWA SASA**

- A. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Msingi Kashato  
Hatua za ujenzi michango inaendelea kukusanywa kwa wananchi na wahisani mbalimbali
- B. Umaliziaji wa madarasa 2 Shule ya msingi Katavi – Hatua iliyofikia Boma limekamilika.
- C. Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Mwangaza Sekondari na umaliziaji wa maabara.

## **CHANGAMOTO**

1. Ubovu wa barabara uliyosababishwa na mvua
2. Tishio la viboko wanaozurula ovyo mtaa wa Kachoma na Kigoma
3. Gari la Taka kutomudu kuondosha taka mtaani na kupelekea taka kuzagaa maeneo (Kaya) zinapohifadhiwa kabla ya kuondolewa.  
Naomba kuwasilisha

Mhe.Haidary Summry  
Diwani Kata ya Makanyagio

## **KATA YA MAJENGO**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KATIKA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI 2018 KATIKA KATA YA MAJENGO.

### **1. UTANGULIZI**

Kata ya Majengo ni miongoni mwa kata 15 zilizopo katika Manispaa ya Mpanda, mkoa wa Katavi . Kata hii imeundwa na mitaa 3 ambayo ni mtaa wa Paradise, maridadi na ji mwema.

### **2. UONGOZI WA KATA**

Kata ya Majengo inao uongozi kama ifuatavyo:-

- I. Ndugu Willy P. Mbogo –Mheshimiwa diwani wa kata –CCM
- II. Ndugu Caritas MAngwangwa –Mhe. Diwani viti maalum –CCM
- III. Ndugu Rhoda Mwakalenge –Mhe. Diwani viti maalum- CCM
- IV. Ndugu Stanslaus Lwambusha Mhe.Mwenyekiti wa Mtaa Mjimwema
- V. Ndugu Donatha Mpandangazi Mwenyekiti mtaa wa Mridadi
- VI. Ndugu Margreth A. Kisanga Kaimu Mwenyekiti mtaa wa Paradise

Aidha mtaa wa paradise hauna mwenyekiti kutokana na dosari za uchaguzi zilizo jitokeza wakati wa uchaguzi bali unakaimiwa na mjumbe wa serikali ya mtaa.

### **3. WATUMISHI WALIOPO KATIKA KATA:**

Kata inaowatumishi wapatao 83 ambapo kati yao 41 ni walimu wa shule zilizopo katika kata 36 ni wafanyakazi w kituo cha afya mwangaza 6 ni wataalamu katika ofisi ya kata.

### **4. MIPAKA YA KATA :**

- Kata ya Majengo inayo mipaka kama ifuatavyo:-
- Upande wa Maghaaaribi inapakana na kata ya Makanyagio
  - Upande wa Mashariki inapakana na kata ya Uwanja wa Ndege
  - Upande wa kaskazini inapakana na kata ya Kashaulili
  - Upande wa Kusini inapakana na kata ya Mpandahotel.

### **5. IDADI YA WATU KATIKA KATA:-**

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Kata ya majengo ina jumla ya kaya 1084 zenye idadi ya watu wapatao 5147 ambapo kati ya hao wanaume ni 2476 na wanawake 2671

### **6. HUDUMA ZA JAMII**

Kata ya Majengo inazo huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule ambazo ziko mbili,soko moja benki ya CRDB 1, Maduka ya rejareja, M-pesa, Sheli ya mafuta n.k

### **7. SHUGHULI ZA WAKAZI KATIKA KATA:**

Wakazi wa kata ya majengo hujishughulisha na shughuli mbalimbali zinazo wawezesha kuishi kama vile vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini , biashara, ufundi wa fani mabaalimbali , watumishi wa serikali , watumishi wa kampuni na Taasisi mbalimbali.

## **8. SEKTA YA MAEDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO.**

Kata ina mtaalam wa sekta ya maendeleo ya jamii anayeratibu shughuli hizo. Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2018 sekta ya maendeleo ya jamii imefanya shughuli zifuatazo :-

- I. Kuendelea kutoa elimu ya kujenga uwezo kwa vikundi vya wajasiliamali vilivyopo katika kata.
- II. Kuendelea kusimamia uundaji wa vikundi vipya vya wajasiliamali ambapo kikundi kimoja kimeundwa na kiko kwenye hatua ya kuandaa katiba.
- III. Kuendelea Kusimamia upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vilivyopo katika kata ambapo kikundi kimoja cha vijana kinachoitwa HAPA KAZI TU, wamepata mkopo wa Tsh milioni nne (4,000,000/=)
- IV. Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa vikundi vilivyopata mkopo.
- V. Kufuatilia marejesho kwa vikundi vilivyopata mikopo ambapo vikundi vifuatavyo vimerejesha:-kikundi cha Mbanga, Loveness na Makaruseje.

## **9. SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**

Ofisi ya Kata ya Majengo inasimamia pia sekta ya kilimo na mifugo ambapo katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2018 shughuli zifuatazo zimefanyika.

- I. Kufanya sensa ya wakulima na wafugaji kwaajili ya bajeti ya kilimo na mifugo ya mwaka **2018/2019**
- II. Kuendelea kutoa hamasa ya kilimo cha mazao ya bustani, juu ya matumizi sahihi ya mbegu bora zenye tija na matumizi sahihi ya viwatilifu na matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza kipato na kuboresha maisha.
- III. Kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa mifugo mbalimbali mfano wafugaji watano wa kuku wa kisasa wamepewa ushauri wa ufugaji wa kuku wa kisasa na kuzingatia chanjo kwa mifugo kama mbwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na kuku dhidi ya ugonjwa wa kideli.
- IV. Kutoa elimu ya utunzaji wa chakula kwa wananchi ili kujikinga na balaa la njaa. Pia katika kipindi hiki cha mwaka wakulima walinufaika na pembejeo za ruzuku ambazo zilipatikana kwa mfumo wa kununua kwa wakala mkuu ndugu E. Mbwilo.

## **10. SEKTA YA AFYA.**

### **1) AFYA KINGA**

Ofisi ya kata kwa kushirikiana na wataalamu na kamati za serikali za mitaa huratibu na kusimamia usafi wa mazingira kwa kudhibiti uchafu katika kata ambapo katika kipindi hiki cha Aprili hadi Juni 2018 kazi zifuatazo zimefanyika:-

1. Kutoa elimu ya afya kinga kwa kuishauri jamii juu ya usafi wa mazingira katika maeneo ya kuishi na biashara
2. Kusimamia vikundi kazi vya uzoaji wa taka ngumu mitaani na kuzipeleka Dampo kuu kwa kutumia lory la manisipaa.
3. Kufuatilia ulipaji tozo za taka
4. Kukagua mazingira mara kwa mara na kuhakikisha kuwa maeneo yote ya kata yanakuwa safi.

### **2) AFYA TIBA**

Kata ya majengo inayo bahati ya kuwa na kituo cha afya katika kata kinachoitwa Kituo cha afya Mwangaza au Town Clinic ambapo wakazi kata hupata huduma za afya katika kituo hicho na wengine hupata huduma za afya katika hospitali kubwa ya Manispaa na katika zahanati za watu binafsi.



Aidha kituo cha afya kina wodi ya wazazi ambayo inasaidia sana kwa huduma ya uzazi kwa akina mama wa kata hii pamoja na Manispaa kwa ujumla.

### CHANGAMOTO ZA SEKTA YA AFYA.

Sekta ya afya inakabirwa na changamoto kadhaa kama vile

- I. Baadhi ya wanachi kutofanya majukumu ya usafi wa mazingira yao kwa hiari.
- II. Baadhi ya wananchi kuendelea kukaidi kutoa tozo za taka
- III. Kata kuwa na maeneo mengi ya wazi ambapo baadhi ya wananchi wasiojua umuhimu wake hutumia vibaya maeneo hayo kwa kutupia taka.
- IV. Kata kuwa na viwanja na mapagala yasiyoendelezwa yaliondani ya kata ambayo husababisha uchafu.
- V. Upungufu wa malori ya kuzolea taka

### UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA SEKTA YA AFYA.

- I. Ofisi ya kata inafanya jukumu kubwa la kuendelea kuelimisha jamii umuhimu wa usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale wanaokaidi maelekezo na kutofanya usafi kwa hiari, pia wale wanaokaidi kutoa tozo la taka.
- II. Ofisi ya kata imeweka mkakati wa kupunguza kasi ya uchafu katika maeneo ya wazi kwa kuokota makopo au uchafu unaozagaa katika maeneo ya wazi hasa siku za jumamosi ya mwisho wa mwezi kwa kushirikiana na watumishi wa kata, viongozi wa mitaa na kata na viongozi wa chama wa kata.
- III. Upungufu wa malori ya taka ni changamoto ambayo tunaomba ofisi ya mkurugenzi isaidie kutatua.

## 11. SEKTA YA ELIMU

Kata ya Majengo ina shule mbili (2) za msingi ambazo ni shule ya msingi Majengo na shule ya msingi Azimio. Kata hii ina haina shule ya sekondari.

### I. IDADI YA WANAFUNZI

NA.	SHULE	WAV	WAS	JUMLA
1	Azimio	392	374	726
	(Azimio maalum)	11	10	21
2	majengo	605	983	1389

### II. IDADI YA WALIMU WALIOPO

NA	SHULE	KABLA YA UHAKIKI			BAADA YA UHAKIKI		
		ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
1	Azimio	11	17	28	9	15	24
2	Majengo	6	12	18	5	12	17
		17	29	46	14	27	41

### III. MATOKEO YA DARASA LA 1V 2017

	shule	waliandikishwa			waliosajiliwa			Walifanya mtihani			waliofaulu		
		WA V	WA S	JML	WA V	W AS	JML	WA V	WA S	JML	WA V	WA S	JML

1	Azimio	49	52	101	43	37	80	39	36	75	39	36	75
2	Majengo	20	46	66	39	34	73	36	34	80	36	34	70
	Jumla	69	98	167	82	71	153	75	70	155	75	70	145

#### IV. MATOKEO DARASA LA VII 2017

	shule	waliandikishwa			waliosajiliwa			Walifanya mtihani			waliofaulu		
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML
1	Azimio	36	47	83	45	51	96	44	49	93	43	42	85
2	Majengo	34	30	64	29	45	74	29	44	73	28	42	70
	Jumla	70	77	147	74	96	170	73	93	166	71	84	155

#### V. UANDIKISHAJI DARASA LA AWALI NA DARASA LA KWANZA

	SHULE	AWALI			DARASA LA I		
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML
1	Azimio	24	29	53	46	45	91
2	Majengo	10	10	20	16	33	49
	Jml Kikata	34	39	73	62	78	140

#### VI. MADAWATI, MADARASA OFISI NA VYOO NYUMBA ZA WALIMU

	SHULE	AZIMIO			MAJENGO		
		mahitaji	yaliyopo	pungufu	mahitaji	yaliyopo	pungufu
1	Madawati	245	250	-	214	240	-
2	madarasa	17	12	5	15	8	7
3	Ofisi	4	2	2	4	3	1
4	vyoo	29	6	23	30	4	26
5	Nyumba za walimu	24	2	22	17	1	16

**Aidha maudhurio ya wanafunzi ni mazuri na hatuna watoro wengi wala mimba za wanafunzi katika kipindi chote cha aprili hadi Juni 2018.**

#### CHANGAMOTO ZA SEKTA YA ELIMU

1. Uhaba wa matundu ya vyoo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi kwani yaliyopo ni 10, yanayohitajika ni 59 na pungufu 49
2. UPungufu wa nyumba za walimu kwani zilizopo ni 3 zinazojitajika ni 41 na pungufu 38
3. Upungufu wa vyumba vya madarasa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi waliopo kwani yaliyopo ni 20 yanayohitajika ni 32 na pungufu ni madarasa 12.

#### UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA SEKTA YA ELIMU

##### 1. MATUNDU YA VYOO:

Ofisi ya kata kwa kuona umuhimu wa vyoo kwa wanafunzi imechukua hatua ya kuanzisha mchakato wa ujenzi wa matundu 8 ya vyoo vya shule za kata. Vikao vilishafanyika kwa kupanga mkakati wakutatua changamoto hii ambapo wananchi walishashirikishwa na kuazimia kufanya ujenzi huo. Aidha tumefanikiwa kutafuta kibali cha uchangishaji wa mchango kwa wananchi na mpaka sasa tumechangisha kiasi cha Tsh. **1,195,000/=** na tuko katika hatua ya upauaji. Tuaeendelea kutoa shukrani zetu za dhiti kwa Mh: Diwani wa kata ambaye katika michango hiyo amechangia Tsh 100,000/= na tripu moja ya kokoto yenye thamani ya Tshs 250,000/= pia ofisi ya mkuu wa wilaya ambayo imechangia Tshs 200,000/= .

## **2. UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA**

Ofisi ya kata imeshaanza kutatua changamoto hii kwa kuanza na mkakati wa ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa mpaka sasa tumeshafanya baadhi ya vikao na mikakati ya maandalizi imeanza .

## **12. SEKTA YA MAJI**

Hali ya maji katika kata ya Majengo ni wastani. Kata inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa maji kwani wakazi ni wengi kuliko huduma ya maji inayopatikana. Wakazi wa kata hii hupata maji katika visima 3 vilivyopo katika kata ambapo katika visima hivyo 2 vyawatu binafsi na kimoja ndiyo cha serikali. Pia wakazi wa kata hii hutumia maji ya bomba maji ambapo hupatikana kwa mgawo kwa kufuata ratiba ya Idara ya Maji. Maji haya hupatikana kwa shida kwani mgawo wake hauzingatii ratiba ilivyopangwa na huleta usumbufu mkubwa kwa wananchi.

### **Changamoto:**

- a) Uhaba wa visima.
- b) Mgawo wa maji ya bomba kutofuata ratiba ilivyopangwa.

### **Utatuzi wa wa changamoto**

1. Changamoto ya uhaba wa visima iko nje ya uwezo wa ofisi ya kata hivyo tunaomba halmashauri ya manisipaa isaidie kutatua changamoto kwa kuongeza idadi ya visima na kuboresha huduma ya maji ya bomba.
2. Tumefuatilia ratiba ya mgawo wa maji katika ofisi ya idara ya maji lakini bado changamoto haijatatuliwa hivyo tunaomba ofisi ya mkurugenzi isaidie kufuatilia utatuzi wa changamoto hii.

## **13. SEKTA YA BARABARA**

Hali ya barabara katika kata ya majengo ni nzuri kwani sehemu kubwa ni barabara za lami.

Changamoto katika barabara za kata ni mitaro kwani baadhi ya barabara zilizoko si imara kwa sababu ya kukosa mitaro. Aidha ipo mitaro ambayo haipitishi maji kutoka na kalavati zake kuziba.

## **14. ULINZI NA USALAMA**

Hali ya ulinzi na usalama katika kata ya majengo ni ya wastani. Katika kipindi hiki cha kuanzia Aprili hadi Juni 2018 hakuna tukio hata moja lilijitokeza, hivyo kata imeendelea kujiimarisha kiulinzi.

## **15. HALI YA MAJANGA**

Katika kipindi cha mwaka 2018 kuanzia Aprili hadi Juni hakuna janga lolote lililotokea katika kata .

## **16. UZALENDO NA UTAIFA**

Katika kipindi cha mwaka 2017 Kata ya Majengo iliwapeleka vijana kadhaa kwenda kujiunga na jeshi la kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kuendeleza dhana ya ujenzi wa Taifa letu. Tunayo matumaini kuwa Kata ya Majengo inao uzalendo wa kutosha kwa Taifa lake.

## **17. UTAWALA BORA.**

Ofisi ya kata ya majengo inaendeshwa kwa kufuata kanuni za utawala bora. Wananchi wa kata hii hupata huduma bora kwa maafisa watendaji na wataalamu, wenyeviti na wajumbe wa mtaa pamoja na waheshimiwa madiwani waliopo. Kila jimbo linaendeshwa

kwa ufinisi ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi kusomwa katika vikao na mikutano ya hadhara. Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2018 vikao 3 vimefanyika katika kata ambapo kimoja ni cha kanuni na 2 ni vikao maalumu (dharula). Pia mikutano maalumu miwili (2) kwa sababu hakuna utaratibu wa mikutano ya kikanuni katika ngazi ya kata.

Aidha vikao na mikutano iliyofanyika katika mitaa ni kama ifuatavyo:-

- Mtaa wa paradise vikao 3 na mkutano 1.
- Mtaa wa Maridadi vikao 3 na mkutano 1.
- Mtaa wa mji mwema vikao 3 na mkutano 1.

## **18. UKIMWI NA MALARIA**

Kata ya majengo inapambana na kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na Malaria kwa kusaidiana na kamati ya kudhibiti UKIMWI ya kata na **NG'O** mbalimbali kama ile Shidepha<sup>+</sup>, Kizazi Kipya n.k. Kamati hii hufanya vikao na kuratibu namna ya kupambana na magonjwa haya hatari na kutoa elimu juu ya maambukizi ya VVU katika kata. Aidha kata inayo maeneo mengi hatarishi yanayo sababisha maambukizi.

## **19. MAPATO NA MATUMIZI**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Kata imehisia kukusanya kiasi cha **899,597,369.36** katika vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mabalimbali za maendeleo ambapo katika kipindi hiki cha Aprili hadi Juni **2018** Kata imekusanya kiasi cha **Tshs. 25,884,773.51** ambayo ni sawa na **2.8%** ya makadilio yake na kutumia kiasi cha Tsh. **15576311.87/=** na kubakiwa na **10,308,461.64** kwa mchanganuo uliopo katika jedwali lifuatalo:-

**MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI 2018 KATIKA KATA YA MAJENGO  
A: UENDESHAJI WA OFISI**

	MAHALI MRADI ULIPO		AINA YA MRADI	GHARAMA ZA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA ZA UTEKELEJAZI
	KATA	MTAA				MAPATO	MATUMIZI	SALIO	
1.	MAJENGO	Paradise Maridadi Mji mwema	Salio katika akaunti.			8,497,292.85	—	8,497,292.85	Ni salio katika akaunti.
2.	MAJENGO.		Uendeshaji wa ofisi	633684.20	Mapato ya ndani ya HM	319429.00	—	319429.00	Ni fedha ambazo hazikuingizwa katika akaunti mgawo wa awamu iliyopita
			<b>JUMLA NDOGO</b>					8816721.85	

**B: - UENDESHAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

1	MAJENGO.	Paradise. Maridadi. Mji mwema	Ujenzi wa matundu 8 ya vyoo S/M majengo.	12,000,000/=	-H/Manispaa Mapato ya ndani -Nguvu za wanao dai -Mfuko wa jimbo.	2,722,364/=	<b>5,568,000</b>	717364	Mradi upo hatua ya uezekaji
						1,195000/=			
						2,368,000			
						6,285,364			
2	MAJENGO.	S/msingi Azimio	Uendeshaji wa shule	—	Capitation	3401127.66	<b>2,818,475.40</b>	<b>582,652.26</b>	Fedha zimetumika kuendeshea shule kama ilivyo elekezwa.
3	MAJENGO.	S/M Majengo	Uendeshaji wa shule	—	Capitation	1,511,560/=	1,431,236.47	80,323.53	Fedha zimetumika kuendeshea shule kama ilivyo elekezwa
4	—	Paradise.	Usafi wa mazingira – Tozo za taka	—	Wananchi (jamii)	1,820,000/=	1,743,600/=	76400	Fedha zimetumika kulipa vibarua, posho za wajumbe, Stationary, 20% ya manispaa n.k

5	_____	Maridadi.	_____	_____	_____	1,895,000	1,895,000	_____	Fedha zimetumika kulipa vibarua, posho za wajumbe, Stationary, 20% ya manispaa n.k
6	_____	Mji mwema	_____	_____	_____	2155,000/=	2120,000/=	35,000/=	Fedha zimetumika kulipa vibarua, posho za wajumbe, Stationary, 20% ya manispaa n.k
	JUMLA NDOGO					17,068,051.66	15576311.87	1491739.79	
	JUMLA KUBWA					25884773.51	15576311.87	10308461.64	

Naomba kuwasilisha

MHE.WILLIAM P. MBOGO.  
DIWANI KATA YA MAJENGO

## **KATA YA MISUNKUMILO**

### **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA APRIL - MAY 2018 - KATA YA MISUNKUMILO**

#### **UTANGULIZI:-**

Kata ya Misunkumilo ni miongoni mwa Kata sita (6) zinazounda Tarafa ya Misunkumilo, Kata ya Misunkumilo kwa upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Makanyagio na Kata ya Mpanda Hotel, Magharibi imepakana na Kata ya Kabungu, Kaskazini imepakana na Kata ya Shanwe, Kusini imepakana na Kata ya Kakese.

#### **IDADI YA KAYA:-**

Kiutawala Kata ya Misunkumilo ina jumla ya Mitaa mitatu (3) na Kijiji kimoja (1) chenye Vitongoji kumi (10). Kata hii ina jumla ya Kaya **2026 na Wakazi wapatao 10,522 kati ya hao Wanaume ni 5154 Wanawake 5368.**

#### **MAPATO:-**

Katika mwaka wa fedha **2018/2019** Kata ya Misunkumilo imekisia kukusanya na kupokea **Tshs. 10,248,498.40** toka katika vyanzo vyake vya mapato kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Posho za Wenyeviti wa Mtaa 4 Tshs. 800,000.00
2. Posho za Wajumbe wa Mitaa na Vitongoji Tshs. 2,000,000.00
3. Fedha ya kuendeshea ofisi ya Kata 1 Tshs. 200,000.00
4. Fedha ya kuendeshea ofisi za Mitaa 4 Tshs. 712,982.40
5. Fedha ya Miradi ya Maendeleo ngazi ya Kata Tshs. 883,000.00
6. Malipo ya mradi wa simu AIRTEL Tshs.1,200,000.00
7. Michango ya Wananchi kwa shughuli za maendeleo Tshs. 1,800,000.00

**JUMLA TSHS. 10,248,498.40**

#### **MATUMIZI KWA KIPINDI CHA APRIL – JUNI 2018:-**

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 Kata imetumia kiasi cha **Tshs 589,260** kwa ajili ya posho ya wajumbe wa Serikali za Mitaa kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Wenyeviti wa Mitaa wanne (4) @Tshs 32,315/= = Tshs 129,260/=
2. Posho ya Wenyeviti wa Vitongoji 9@Tshs.20,000/= =Tshs. 180,000/=
3. Posho ya Wajumbe wa Serikali za Mitaa @ 20,000/= 280,000/=

**JUMLA TSHS.589,260/=**

#### **MICHANGO YA SHUGHULI ZA MAENDELEO:-**

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 jumla ya michango Tshs. 300,000/= zimekusanywa kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya Msingi Misunkumilo na trip 5 za mawe zimekusanywa , tofari 15,000 zilizochochomwa.

Aidha tofari 9,000, mawe trip 10, mchanga trip 5 zimekusanywa katika Shule ya Msingi Milala na fedha taslim 30,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

#### **CHANGAMOTO ZILIZOPO:-**

Ugumu wa Wananchi kuhudhuria mikutano ya hadhara. Ugumu wa Wananchi kuchangia michango ya shughuli za maendeleo uelewa ni mdogo.

**UFYATUAJI WA TOFARI NA ULIPAJI 7% YA MATOFARI:-**

Kwa kipindi cha May hadi Juni jumla ya **Tshs. 240,000/=** zimekusanywa kwa ajili ya kuomba vibari vya kufyatua tofari ambapo tutakusanya 7% ya tofari alizofyatua.

**TAARIFA MBALIMBALI KATIKA KATA:-**

**KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI:-**

Kamati hii imekifanya kikao kimoja ambacho kilijadiliwa taarifa ya hali maambukizi ya VVU katika Kata, mtoa huduma majumbani alieleza kuwa hali ya maambukizi katika Kata yapo lakini siyo kama hapo mwanzo.

Wagonjwa wapo lakini hawapo kitandani kama siku za nyuma kwa sasa wapo na wanafanya kazi zao kama kawaida kwa sababu wamepokea ushauri wa kunywa dawa. Kikao cha Kamati ya Ukimwi kimefanyika tarehe 17/07/2017.

Wajumbe wa Kamati ya maendeleo ya Kata wamepongeza sana watoa huduma majumbani na wameomba waendeleo kuhamasisha jamii katika mikutano ya hadhara na maeneo mengine.

**MATUKIO;** Kwa kipindi cha April – Juni lipo tukio la Mwananchi kujinyonga tukio ambalo lilitokea **tarehe 9/05/2018.**

**TASAF:-**

Kwa kipindi cha April hadi Juni 2018 Kaya masikini 138 wamelipwa posho jumla ya **Tshs. 2,500,000/=** Kata ya Misunkumilo.



**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA APRIL – JUNI 2018**

<b>KATA</b>	<b>KIJIJI/ MTAA</b>	<b>AINA YA MRADI</b>	<b>CHANZO CHA FEDHA</b>	<b>FEDHA ILIOPOKELE WA</b>	<b>FEDHA ILİYOTUMIKA</b>	<b>FEDHA ILİYOBAK I</b>	<b>HATUA YA UTEKELEZA JI</b>	<b>MAELEZO</b>
M/NKUMILO	KAMPUNI	UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 2, OFISI NA VYOO 2	MANISPA A MPANDA	60,564,000	58,260,300	2,303,700	UJENZI UMEFIKIA 95%	MRADI UPO HATUA ZA MWISHO
M/NKUMILO	M/NKUMI LO	UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA SEKONDAR I 2	MANISPA A MPANDA	40,000,000	37,108,000	2,892,000	UJENZI UMEFIKIA 100%	MRADI UMEKAMILIKA
	MIS/MIL O	UKAMILISH AJI WA MAABARA	MANISPA A MPANDA	9,000,000	8,738,800	261,200	SHUGHULI IMEKAMILIK A	BADO MADAWATI
<b>JUMLA</b>				<b>109,564,000</b>	<b>104,107,100</b>	<b>5,195,700</b>		<b>MATUMIZI YANAENDELEA</b>

**SEKTA YA KILIMO:-**

Jumla ya wakulima nane (8) walilima zao la pamba wanaendelea kuvuna zao hili ambalo linaendelea vizuri na wako tayari kuuza. Jumla ya ekari 11.5 zilizolimwa.

**ZAO LA KOROSHO:-**

Zao la korosho linaendelea kutunzwa licha, ya changamoto za mifugo wafugaji wanakumbushwa kuangalia mashamba ya korosho na wakulima waendeleo kufanya usafi mashamba yao. Jumla ya ekari 68 zilipandwa zao hilo.

**CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MIFUGO:-**

Hakuna maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya malisho na ndiyo maana migogoro ya wakulima na wafugaji ipo ya mara kwa mara.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO:-**

Viongozi tunaendelea kuelimisha wafugaji kupunguza idadi ya mifugo yao au kuhamia maeneo ambayo yana nafasi ili kuondoa au kupunguza migogoro.

**SEKTA YA MAJI:-**

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 jumla ya visima virefu vimechimbwa kati ya hivyo visima 2 vimefungwa pampu zinatumiwa.

**HALI YA ULINZI NA USALAMA:-**

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 vikao vya WDC, kimefanyika kikao kimoja kiko cha Kamati ya malalamiko kimoja, kikao cha mazingira kimoja, kikao cha Kamati ya kudhibiti Ukimwi kikao kimoja.

**MAJANGA:-**

Hakuna majanga yaliyolipotiwa katika Kata.

**MIKUTANO YA HADHARA:-**

Kwa kipindi cha April – Juni 2018 umefanyika mkutano mmoja ambao ulihusu hali ya usalama katika Kata.

**MWISHO:-**

Naomba kuwasilisha,

**MHE.MATONDO KANYEPO  
DIWANI KATA MISUNKUMILO**

## **KATA YA MPANDA HOTEL**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA KUENZIA APRILI HADI JUNI 2018 KWA KATA YA MPANDAHOTEL.

### **UTANGULIZI**

Kata ya Mpandahotel ni miongoni mwa kata kumi na tano (15) zinazounda manisipaa ya mpanda.

Kata hii inapakana na kata nne kama ifuatavyo:-

- (a) Kaskazini inapaka na kata ya makanyagio.
- (b) Mashariki inapakana na kata ya kashaulili
- (c) Kusini inapakana na kata ya Ilembo.
- (d) Magharibi inapakana na kata ya misunkumilo.

### **KIUTAWALA.**

Kata hii inaundwa na mitaa mitatu ambayo ni Msasani, Mpandahotel na Tambukarel, kata hii ina serikali tatu za mitaa ambazo zina wajumbe halali waliochaguliwa kwa taratibu za uchaguzi japo mtaa mmoja wa Tambukarel kwa mapenzi ya mungu mjumbe mmoja alishafariki kwa takribani ya miaka mitatu iliyopita.

Sambamba na hilo mitaa hii kwa sasa haina watendaji wa mitaa kama makatibu wa serikali hizo za mitaa, jambo ambalo kwa sasa linacherewesha uratibu na usimamizi wa shughuli za maendeleo.

### **IDADI YA WATU WA MAKAZI**

<b>KATA</b>	<b>MAKAZI KAYA</b>	<b>JML YA WATU</b>	<b>ME</b>	<b>KE</b>	<b>WENYE UWEZO</b>	<b>ME</b>	<b>KE</b>	<b>WATOTONA WASIO JIWEZA</b>	
								<b>ME</b>	<b>KE</b>
Mpandahoteli	1890	11,027	5513	5514	4074	1098	2976	1920	5933

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KWA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI 2018**

NA	KATA	KIJIJI/MTAA	AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEKEZO
					Iliyopokelewa	Iliyotumika	Iliyobaki		
01	<b>MPANDA HOTEL</b>	MPANDAHOTEL	SHUGHULI ZA UENDESHAJI OFS MITAA	HALMASHAURI	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	FEDHA HAZIJAWEKWA KWENYE AKAUNTI
		MSASANI	POSHO WAJUMBE KWA		HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA MJUMBE ALIOLIPWA	
		TAMBUKARELI			POSHO W/V/MITAA KWA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA PESA
		KATA	UENDESHAJI OFISI YA KATA		HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA PESA	
			UENDESHAJI SHUGHULI MAENDELEO KATA ZA	MFUKO WA JIMBO	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA	HAKUNA PESA	
			FAINI ZA BARAZA	WANANCHI	-	-	HAKUNA	HAKUNA PESA	
		<b>JUMLA KUU TSHS,</b>					<b>HAKUNA</b>	<b>HAKUNA</b>	<b>HAKUNA</b>

## ULINZI NA USALAMA

Kata ya Mpandahotel ina mitaa mitatu ambayo ina Selekali kamili hivyo kamati za ulinzi shirikishi zimeketi nakuunda vikundi vya ulinzi kila mtaa isipokuwa mtaa wa mpandahotel, na vikundi hivyo vimeanza Doria za nyumba kwa nyumba ili kupambana na wizi unaofanyika katika mitaa hii.

## AFYA

Kata	Mtaa	Kaya	Vyoo vilivyokaguliwa	
			Tayari	Bado
	Mpandahotel	650	450	200
	Msasani	610	305	305
	tambukaleli	630	507	123

## MAZINGIRA

Swala la mazingira katika kata hii lina shughulikiwa ipasavyo kwa ushirikiano wa wajumbe wa ngazi ya kata na walezi kutoka manispaa kwenye vikao vya kata ila utatuzi wake unakutwa na ugumu wa jiografia ya eneo la kata hii takribani ni asilimia 80 ya eneo ni viwanda hivyo ukabilianaji wa swala la mazingira kuwa gumu, japo jitihada zinaendelea.

## MAJI.

Katika swala hili la upatikanaji wa miundombinu ya maji mikakati inaendelea, na mpaka sasa mtaa wa mpandahotel unawasitani wa 70% huduma ya maji ipo na Tambukarel juhudi zinafanyika kupitia mradi wa Tasaf kusambaza maji kila eneo, na wataalamu wa maji walikwisha kufanya utafiti wa awali, pia kwa mtaa wa Msasani bado taratibu za serikali zinafanyiwa kazi kwa ajiri ya kuchimba kisima kirefu japo kata inamipango ya kuunganisha miundo mbinu hiyo na maji ya Ikorongo kupitia mtaa wa Mpandahotel.

## KAMATI ZA UKIMWI.

Kata hii imekuwa ikifanya vikao vya kamati za Ukimwi mara kwa mara nahali hii inalazimika kutokana na kata hii kuwa ndio mapokeo na matoleo ya jamii inayoingia mkoa wetu na jamii inayotoka hapa katavi pia kata hii kiuhalisi ina kila sababu ya kuweka kipaumbele swala la kujikinga na maambukizi ya Ukimwi na virusi vya Ukimwi hivyo kumekuwa haja ya vikundi mbalimbali vya kusimamia upimaji na utoaji elimu. Mashirika mbalimbali yameweka wawakilishi wa upimaji Ukimwi majumbani.

## ELIMU.

### TAARIFA YA ROBO MWAKA JAN- MARCH 2018.

#### 1. MIUNDOMBINU-: KATA YA MPANDAHOTEL

SHULE	AINA	MAHITAJI	YALIYOPO	%	PUNGUFU	%
MPANDA	MADARASA	VYUMBA 45	9	20	36	80
	VYOO WALIMU	2	1	50	1	50
	VYOO WANAFUNZI	81	10	12	71	88
	VYUMBA (W)	45	-	0	45	100
	OFISI	2	1	50	1	50
	STOO	2	1	50	1	50
MUJUNGANO	MADARASA	36	9	25	27	75
	VYOO WALIMU	2	1	50	1	50
	VYOO WANAFUNZI	65	10	15	55	85
	VYUMBA (W)	36	-	0	36	100
	OFISI	2	2	100	-	0

	STOO	2	-	0	2	100
KASHAULILI SEKONDARI	MADARASA	20	14	70	6	30
	VYOO WALIMU	3	3	100	-	0
	VYOO WANAFUNZI	30	17	57	13	43
	VYUMBA (W)	31	2	6	29	94
	OFISI	2	2	100	-	0
	STOO	2	-	0	2	100
	MAABARA	3	3	100	-	0

## 2. SAMANI

MPANDA	MADAWATI	602	602	100	-	0
	MEZA	30	19	63	11	37
	VITI	30	27	77	7	23
MUUNGANO	MADAWATI	488	488	100	-	0
	MEZA	24	19	79	5	21
	VITI	32	22	69	10	31
KASHAULILI SEKONDARI	MADAWATI	751	668	89	83	11
	MEZA	30	8	27	22	63
	VITI	30	5	17	25	83

## 3. IDADI YA WANAFUNZI

3. IDADI YA WANAFUNZI				MEMKWA – MPANDA		
SHULE	WV	WS	JML	ME	KE	JML
MPAND	891	914	1805	61	54	114
MUUNGANO	717	715	1432			
KASHAULILI SEC	386	365	751			

## 4. (i) IDADI YA WALIMU

## (ii) WASIO WALIMU

SHULE	ME	KE	JML	ME	KE	JML
MPANDA	8	11	19	1	-	1
MUUNGANO	4	12	16	1	-	1
KASHAULILI SEC 19	9	28	2	2	-	2

## 5. UANDIKISHAJI NA MATOKEO YA WANAFUNZI – 2018 MATOKEO

SHULE	WV	WS	JML
AWALI	101	119	220
MPANDA	147	149	296
DRS 1			
AWALI	71	80	151
MUUNGANO	67	66	133
DRS 1			
WALIO LETWA	113	120	233
KASHAULILI SEC			

## UANDIKISHAJI

SHULE		WV	WS	JML	%
MPANDA	AWALI	72	99	171	78
	I	157	133	290	99
MUUNGANO	AWALI	83	77	160	106
	I	104	101	205	154
KASHAULILI FORM I		116	99	215	92

6. FEDHA: RUZUKU YA SERIKALI			
SHULE	MAPATO	MATUMIZI	SALIO
MPANDA	2,763,880/=	1,201,200/=	1,562,680/=
MUUNGANO	1,723,580/=	1,612,000/=	111,580/=
KASHAULILI SEKONDARI	3,558,000/=	2,360,000/=	1,198,000/=

### 7. MIRADI INAYOENDELEA.

#### UJENZI WA VYOO VYA WANAFUNZI

#### MICHANGO YA WANANCHI NA WADAU ANUAI

SHULE	IDADI YA MATUNDU	MAKISIO	MAPATO	MATUMIZI	SALIO
MUUNGANO	20	12000,000/=	3807000/=	3431000/=	376000/=
MPANDA	20	12000,000/=	2640,000/=	2640,000/=	-

NB: (1) ILI KUKAMILISHA VYOO VYA WANAFUNZI SHULE YA MSINGI MPANDA WANAOMBA TSHS 9,360,000/=

(2). SHULE YA MSINGI MUUNGANO WANAOMBA TSHS 8,569,000/=

#### CHANGAMOTO.

1. Ni ukosefu wa kujenga kizimba
2. Ni wananchi kujua hatima yao kwa swala lililo wakuta la upishaji wa ujenzi wa reli kuwa watapata fidia au laa
3. Ni uelewa tofauti kwa wananchi juu ya kuchangia juhudi za maendeleo pale ambapo walisikia hatachaguliwa michango japo elimu inaendelea kuelimishwa.
4. Ugumu wa kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo kwa upungufu wa watendaji wa mitaa kuwa mtendaji wa kata ndio mtendaji wa mitaa yote mitatu.

Naomba kuwasilisha taarifa hii kwako mwenyekiti wa kikao hiki kitukufu kwa heshima kubwa na unyenyekevu thabiti kwa kupokea, masahihisho, maelekezo na pia ushauri wako kupitia baraza hili kuwa tayari kupokea kwa mikono yote.

Naomba Kuwasilisha

**Mhe. William Liwali**  
**DIWANI KATA YA MPANDA HOTEL**

## KATA YA MWAMKULU

KUWASILISHA TAARIFA ZA ROBO YA NNE YA MWAKA 2017/2018 YA APRIL HADI JUNE 2018 YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO NA TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI KATA YA MWAMKULU.

## UTANGULIZI

Kata ya Mwamkulu ni moja ya Kata zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Kata hii imeundwa na Mitaa mitano, hiyo ni **Kabwaga, Mkokwa, Mkwajuni, Nguvumali** na **Nseso** kwa mjibu wa sensa ya **mwaka 2012** Kata hii ina kaya **1544** zenye wakaazi **7277**, wakiwa wanaume **3576** na wanawake **3701**.

## HALI YA HEWA

Kwa kipindi hiki **April** hadi **June** hali ya hewa ni nzuri na wananchi wameweza kuvuna mazao yao vizuri na tayari wameweza mazao yao gharani.

## VIKAO VYA KISHERIA

Katika Kata ya Mwamkulu kuna vikao vya kisheria vilivyofanyika kwenye Mitaa yote mitano na Kata pamoja na vikao hivyo kumefanyika mikutano ya kisheria pamoja na mikutano ya dhahara kama inavyoonekana kwenye jedwali.

S/N	MIKUTANO YA HADHARA	MAHITAJI	VILIVYO FANYIKA	UPUNGUFU	MAELEZO
1	Kabwaga 1	3	3	0	-
2	Mkokwa 1	3	2	1	-
3	Mkwajuni 1	3	3	0	-
4	Nguvumali 1	3	1	2	-
5	Nseso 1	3	2	1	-

## MAENDELEO YA SHULE ZA MSINGI

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwamkulu na Shule shikizi za Kabwaga, Mkokwa, Mkwajuni na Nseso zinaendelea vizuri kama zinavyoonekana kwenye jedwali.

## IDADI YA WANAFUNZI

JINA LA SHULE	WAV	WAS	JUMLA
Mwamkulu	675	615	1290
Nseso	49	53	102
Kabwaga	382	353	735
Mkokwa	288	273	561
mkwajuni	103	90	193
<b>JUMLA KUU</b>	<b>1497</b>	<b>1386</b>	<b>2881</b>

## MADARASA

SHULE	LENGO	YALIOPO	PUNGUFU
Mwamkulu	15	7	8
Nseso	5	-	5
Kabwaga	10	7	3
Mkokwa	10	3	7
Mkwajuni	3	-	3



Pamoja na upungufu huo wa madarasa tayari kwa shule ya Msingi Mkwajuni madarasa mawili na Ofisi muda si mrefu yatakuwa yamekamili vilevile madarasa matatu mengine michango ya fedha kwa ajili ya umaliziaji/upauaji inaendelea ili kuenzeka/kupaua sambamba na shule hiyo shule ya Msingi Nseso nayo wananchi wa mtaa wa Nseso wanaendelea na michango kwa ajiri ya kumaliza madarasa hayo mawili na Ofisi moja hii ni pamoja na michango inayoendelea ya kukamilisha ujenzi wa darasa moja na ofisi Shule ya Msingi Mkokwa.

### NYUMBA ZA WAALIMU

S/N	SHULE	LENGO	ZILIZOPO	PUNGUFU	MAELEZO
1	KABWAGA	7	-	7	
2	MKOKWA	7	-	7	
3	MKWAJUNI	3	-	3	
4	MWAMKULU	19	2	17	
5	NSESO	2	-	2	

Juhudi za ufyatuzi wa tofari na michango ya fedha zinaendelea kwa ajili ya kupunguza upungufu huo.

### WAALIMU

S/N	SHULE YA MSINGI	LENGO	WALIOPO	PUNGUFU	MAELEZO
1	MWAMKULU	19	12	7	
2	KABWAGA	5	2	3	
3	MKOKWA	5	1	4	
4	MKWAJUNI	2	-	2	
5	NSESO	2	-	2	

- A. Pamoja na upungufu huu tunaishukuru Serikali kwani tayari wamelipoti walimu nane ambao watakuwa Kata ya Mwamkulu ambao watagawanywa kwa shule ya Msingi Mwamkulu na Shule shikizi hivyo kupunguza upungufu wa waalimu Katika shule za Kata ya Mwamkulu.
- B. Pamoja na kupata waalimu hao Kata bado inaendelea na kua na waalimu wa kujitolea ambao wanalipwa na wazazi mpaka hapo upungufu huo wa waalimu utakapo kwisha.

### MADAWATI

Katika Kata ya Mwamkulu hatuna upungufu wa madawati yapo ya kutosha changamoto ni vyumba vya madarasa.

### ELIMU YA SEKONDARI

Kata ya Mwamkulu inathamini elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari imejiwekea mikakati ya kujenga madarasa matano ya Sekondari kila Mtaa ujenge darasa moja la Sekondari na makubaliano hayo kwa kipindi hiki ni ujenzi wa madarasa hayo kwa kukamilisha maboma tayari eneo la hekali kumi na mbili zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo wa shule ya Sekondari na tayari kwa kila Mtaa michango ya tofari na michango ya fedha inaendelea vizuri ili kufanikisha zoezi hilo.

### IDADI YA MIFUGO KWA KATA YA MWAMKULU

NG'OM BE	MBU ZI	KOND OO	PUNDA	NGURU WE	MBWA	PAKA	KUKU	BATA	KANGA	NJIWA
7847	2017	357	35	39	701	260	1979 7	2291	43	1100

## **KILIMO**

Kwa kipindi hiki cha **April – June** wakulima wanaendelea kuvuna mazao waliokua wamelima kwa msimu huu hivyo mavuno ni mazuri na wanavuna na kujitunzia chakula kwa ajili ya matumizi yao pia ziada wanauza ili kujipatia kipato.

## **CHAMA CHA UMWAGIRIAJI**

Chama hicho cha umwagiliaji kinaendelea vizuri na shughuli za chama na kinaendelea kuwahamasisha wakulima wenye mbuga za mpunga ndani ya mpunga ya Mwamkulu waende kujisajili kwenye chama hiki ili wawe wanachama katika chama hicho.

## **BIASHARA**

Wakazi wa Kata hii wanaendelea na shughuli za biashara mbalimbali kama vile **vibanda, migahawa, maduka, biashara ndogondogo** vilevile kuna **mashine za kukoboa na kusaga nafaka mashine za kukoboa mpungua**, biashara nyingine ni mafundi baiskeli biashara za vinywaji, vinyozi na mafundi baiskeli biashara hizi kwa sasa zinakwenda vizuri kwa sababu ni wakati wa mavuno.

## **MAJI**

Kata hii ya Mwamkulu kwa kipindi hiki cha **April** hadi **Juni** Serikali inaendelea kuchimba visima virefu tayari kuna visima vitano vimechimbwa bado tu havijafungiwa Pampu ili vianze kutoa huduma kupitia kasi hii ya uchimbaji wa visima hatuna budi kuishukulu Serikali kwa kuliangalia tatizo la maji kwa macho mawili hivyo baada ya kufungwa Pampu tatizo la maji kwa Kata hii litapungua kwa asilimia **75** kutokana na mgao wa kuchimbiwa visiwa saba na kisima kimoja cha ahadi ya Mbunge wa Mpanda Mjini ambacho tayali kimechimbwa hivyo Kata hiyo kua na visima nane na tayali vimechimbwa visima vitano **(5)** bado **3** tunaiomba Serikali iendelee kuchimba visima hivyo vitatu vilivyobaki ili kuondoa kabisa tatizo hili la maji kwa Kata hii ya Mwamkulu.

## **HUDUMA YA AFYA**

Huduma ya Afya zinaendelea vizuri kwa zahanati ya Mwamkulu kuendelea kutoa huduma kikamilifu na kutokua na upungufu wa dawa kwa kipindi hiki cha April hadi Juni shughuli zinaendelea vizuri pamoja na zahanati hii ya mwamkulu kua inaendelea kufanyakazi kwa sasa muda wowote kuanzia sasa zahanati ya Mlima kipara ambayo ipo Kata ya Mwamkulu itaanza kufanya kazi hatua zinazo endelea ni kutafuta vyumba vya kukaa waganga kwa kua mganga Mkuu tayari amelea waganga kwa ajili ya kuanza huduma hapo zahanati ya Mlima Kipala.

## **TASAF**

Kwa kipindi hiki cha robo ya nne ya mwaka walengwa wa TASAF wameweza kufanya mkutano na vikao kwa ajili ya kuibua miradi itakayotekelezwa kwa miezi minne kuanzia Julai hadi **Oktoba 2018**. Miradi iliyoibuliwa ni uchimbaji wa visima, upandaji wa miti ya matunda na uchimbaji wa mabwawa.

## **ULINZI NA USALAMA**

Katika Kata ya Mwamkulu tumekua tukipanga vikao vya kamati ya ulinzi na usalama ya mitaa na kata pamoja na mikutano ya hadhara kwa polisi Kata na Polisi mita kuja kutoa elimu juu ya ulinzi shilikishi na tumekua tunamuunganiko mkubwa kati ya serikali sungusungu na Polisi kwa matukio yote yaliyojitokeza ndani ya robo ya nne ya mwaka.

## MAPATO NA MATUMIZI

NA	KATA	MTAA	AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	LENGO	ZILIZOKUSAN YWA	PUNGUFU	MAELEZO
1		MKWAJUNI	Ujenzi wa madarasa mawili ofisi na vyoo	Fedha toka serikalini	Tshs 60,000,000/=	Tshs 60,000,000/=		Kazi ipo kwenye hatua ya umaliziaji
2		MKWAJUNI	Ujenzi wa sekondari na umaliziaji wa madarasa S/ya msingi	Michango nguvu za wananchi	Tshs 8,00,000/=	Tshs 200,000/=	Tshs 7,800,000/=	Michango inaendelea
3		MKWAJUNI	Ujenzi wa sekondari na shule ya msingi	Nguvu za wananchi	Tshs 9,000,000/=	Tshs 2,000,000/=	Tshs 7,000,000/=	Michango inaendelea
4		KABWAGA	Ujenzi wa darasa 1 la sekondari	Nguvu za wananchi	Tshs 3,400,000/=	Tshs 280,000/=	Tshs 3,120,000/=	Michango inaendelea
5		NGUVU MALI	Ujenzi wa darasa la sekondari	Nguvu za wananchi	Tshs 4,000,000/=	Tshs 1,800,000/=	Tshs 2,200,000/=	Michango inaendelea
6		NSESO	Ujenzi wa darasa la sekondari na upauaji wa madarasa S/ msingi Nseso	Nguvu za wananchi	Tshs 8,500,000/=	Tshs 524,000/=	Tshs 7,976,000/=	Michango inaendelea
7	MWA MWA MKULU	-	Kaya masikinmi	Serikali Tasaf	Tshs 28,000,000/=	Tshs 28,000,000/=		Fedha zimelipwa
		-	Ujenzi wa nyumba ya Afisa Ugani Kata	H/masha uri ya Manispaa	Tshs 57,000,000/=	Tshs 17,000,000/=	Tshs 60,000,000/=	Nyumba inaendelea kujegwa kwa kasi
		-	Fedha ya posho ya wasimamizi wa vitambulisho ya Taifa (NIDA)	Michango ya wananchi	Tshs 2,000,000/=	Tshs 1,600,000/=	Tshs 400,000/=	Fedha Tshs 900,000/= zilitukima na 700,000/= zipo Benk

### UKIMWI

Kata ya Mwamkulu kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka imefanya kikao kimoja (1) na kikao hiki kilikuwa na maazimio

1. Kuboresha kamati za Ukimwi za mitaa.
2. Kutoa hamasa kwa wananchi kupima kwa hiali maambukizi ya VVU
3. Kuweka mkakati wa kupambana na maambukizi mapya pamoja na kutoa hamasa kwa hale walioambukizwa kutumia dawa kwa usahihi

### MIRADI INAYOTEKELEZWA KWA KUPINDI HIKI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA

NA	KATA	MRADI	HATUA YA UTEKELEZA	MTAA
1	MWAMKULU	Ujenzi wa nyumba ya Afisa Ugani	Nyumba ipo kwenye lenta na kazi inaendelea vizuri	Mkwajuni
2	-	Ujenzi wa madarasa mawili ofisi na matundu ya vyoo	Madarasa yapo kwenye hatu ya umaliziaji sababa na ofisi pamoja na vyoo	Mkwajuni
3	-	Ukamilishaji/umaliziaji wa	Madarasa mawili na ofisi	Nguvumali

		madarasa	moja yapo kwenye hatua ya umaliziaji	
4	-	Uchimbaji wa visima vilefu	Kazi za uchimbaji zinaendelea	- Mkokwa visima viwili -kambwaga kisima kimoja -nguvumali kisima kimoja Mkwajuni kisima kimoja

### **HIFADHI YA BONDE LA MTO KATUMA MITA SITINI**

Katika kipindi hiki cha robo ya nne ya mwaka kazi ya ulinzi wa hifazi ya mazingira ndani ya bonde la mto Katuma mita sitini zinaendelea vizuri kwa kufanya doria ndani ya mita sitini

### **MIUNDOMBINU**

Kata ya Mwamkulu haina miundo mbinu hususani barabarea hazipitiki hasa wakati wa masikia hii inasababisha Kata hii kutofikiwa kwa wakati

### **CHANGAMOTO**

1. Wakulima kutokuwa na uelewa juu ya kujiunga na chama cha uwagiliaji
2. Miundombinu ya barabra kutopitika wakati wa masika.
3. Upungufu wa Maafisa Ugani/Watendaji mitaa.
4. Mifereji wa sikimu ya umwagiliaji kutokamilika kwa wakati

### **MWISHO.**

Nawashukuru wale wote waliotoa mchango wao wa mawazo ili kufanikisha uandaaji wa taarifa hii ya robo ya nne ya mwaka April hadi June **2018**

.....  
**MH:KALIPI S. KATANI**  
**DIWANI KATA YA MWAMKULU**

## KATA YA NSEMULWA

TAARIFA FUPI YA UTEKELELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATA YA NSEMULWA KWA KIPINDI CHA KUENZIA APRILI – JUNI 2017-2018 ROBO YA NNE

### 1. UTANGULIZI

#### Mh mstahiki meya

- Kata ya Nsemulwa ni miongoni mwa kata **15** zinazounganisha Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na ipo umbali wa Km **4** kutoka makao makuu ya manispaa

#### MIPAKA

1. Kwa upande wa kusini kata hii imepakana na kata ya uwanja wa ndege
2. Kwa upande wa kaskazini kata hii imepakana na kata ya Kazima
3. Kwa upande wa mashariki kata hii imepakana na kata ya Mtapenda iliyoko halmashauri ya Nsimbo
4. Upande wa magharibi kata hii imepakana na kata ya Kashaulili.

**UTAWALA (UONGOZI)** - Mheshimiwa diwani wa kata yupo aliyepita kwa tiketi ya chama cha mapinduzi (**CCM**)

- Kata hii ina mitaa **5** na kijiji **1**
- Uongozi ndani ya mitaa na kijiji upo kama ifuatavyo
  - (i) Mtaa wa Nsemulwa mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wake wapo **4** na **1** huwa hafiki kwenye kikao
  - (ii) Mtaa wa Tulieni mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wapo **4** na **1** alishahama.
  - (iii) Mtaa wa Kichangani mwenyekiti wa mtaa yupo wajumbe **3** wapo, mjumbe **1** alifariki na mjumbe **1** ameshajiachisha ujumbe kwa kutohudhuria vikao vya kisheria vya Serikali ya mtaa zaidi ya mwaka **1**.
  - (iv) Mtaa wa kilimani mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wake wote wapo
  - (v) Mtaa wa Migazini mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wanaofanya kazi wapo **2**
  - (vi) Kijiji cha Shankala mwenyekiti wa kijiji yupo pamoja na wenyeviti **3** wa vitongoji wapo .

### IDADI YA WATU NA MAKAZI

IDADI YA KAYA	KAYA ZENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI	KAYA ZISIZO NA UWEZO	IDADI YA WATU		WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI		WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI		WATOTO YATIMA		WALEMAVU WA VIUNGO		WATOTO WENGI NE	
			ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE
2343	1734	509												
			4912	5781	2203	2539	430	642	2480	2664	1619	1231	2196	2402

### SHUGHULI ZA KIUCHUMI WAZIFANYAZO WANANCHI WA KATA YA NSEMULWA

1. Kilimo cha kutumia jembe la mkono, kilimo cha kutumia matrekta pamoja na kilimo cha kutumia wanyama kazi ambapo wakulima walio wengi hufanya shughuli zao hizo za kilimo nje ya kata hii ya Nsemulwa.

## HUDUMA ZA KIJAMII ZINAPATIKANA NDANI YA KATA HII

1. Ipo shule ya msingi **1** inayotoa huduma kwa mitaa yote **5**
2. Misikiti **4** na makanisa **12**
3. Lipo genge **1** litumikalo kama soko maarufu kwa jina la soko la Kwarakwacha ambalo lina maelekezo ya kuhamishwa na kupelekwa eneo lililopimwa kisheria wakati wowote kuanzia sasa.

## WATUMISHI WALIOPO NGAZI YA KATA

Na	IDARA	JINSIA		JUMLA
		ME	KE	
1	UTAWALA	1	0	1
2	AFISA ELIMU KATA	0	1	1
3	AFYA	0	1	1
4	KILIMO, USHIRIKA NA MIFUGO	1	0	1
5	M/JAMII	0	1	1
6	ELIMU MSINGI	12	12	24

## VIKAO NA MIKUTANO YA KATA VYA KISHERIA NA DHARULA

TAREHE YA KIKAO	MKUTANO	WDC KAWAIDA	WDC DHARULA
03/07/2017		1	
08/04/2018			1
05/06/2018	1		
Jumla ya vikao vilivyofanyika	3		

<b>MKUTANO</b>	<b>1</b>
<b>VIKAO</b>	<b>2</b>

## MIRADI YA MAENDELEO

- Katika Kata hii kuna miradi iliyoibuliwa na wananchi na kuanza kutekelezwa na wananchi pamoja na ofisi ya Mkurugenzi kama ifuatavyo :-
  - (a) Ujenzi wa ofisi ya Kata ambayo inajengwa mtaa wa Kichangani na ujenzi huo ulianza mwaka **2003** hadi mwaka **2014** uliposimama kwa ukosefu wa fedha.

AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
		ILIYOPOKELEWA	ILİYOTUMIKA	ILİYOB AKI		
Ujenzi wa ofisi ya Mtendaji kata ya Nsemulwa mwaka	Halmashauri	21,221,969.50	21,221,969.50	-	Jengo lote limepauliwa na kuwekwa fremu za madirisha na milango ya nje , fedha pungufu ni	Fedha Tshs. 22,380,682.69 zilizotumika kumlipa mkandarasi kwa kuzingatia mkataba pia

2013/2014					Tshs 9,442,686.50/= kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi bado umesimama kwa kukosa fedha	kununua vifaa vya nguvu za wananchi
-----------	--	--	--	--	--	---

AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
		ILIOPOKELEWA	ILİYOTUMIK A	ILİYOBAKI		
Ujenzi wa ofisi 1 ya Kijiji cha Shankala	Halmashauri Wananchi	<b>15,000,000/=</b> <b>3,000,000/=</b> <b>18,000,000/=</b>	<b>18,000,000/=</b>	-	Jengo lote limepauliwa na kuwekwa fremu za madirisha na milango ya nje , fedha pungufu ni Tshs 7,000,000/= kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi bado umesimama kwa kukosa fedha	Fedha Tshs. 7,000,000/=  Jengo limepauliwa lote milango na fremu za madirisha vimewekwa kasoro dilisha moja halijawekwa fremu  Jumla 7,000,0000/=  zinatakiwa ili kumalizia jengo
Ujenzi wa kituo cha afya mtaa wa Kilimani	Halmashauri na wananchi	<b>1,650,000/=</b>	<b>1,650,000/=</b>	-	Tripu 9 za mawe na tripu 5 za mchanga ambazo ni nguvu za wananchi na halmashauri zipo eneo la ujenzi	Uhamasishaji juu ya uchangiaji na nguvu za wananchi unaendelea

<b>Jumla kuu</b>		<b>1,650,000/=</b>	<b>1,650,000/=</b>			
------------------	--	--------------------	--------------------	--	--	--

**UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA YA SHULE YA MSINGI NSEMULWA**

AINA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA			HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
		ILIOPOKELEWA	ILİYOTUMIKA	ILİYOBAKI		
Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ya shule ya msingi Nsemulwa mwaka 2017/2018. Tshs. 25,000,000/=	PAR FUND	2,000,000/=	2,000,000/=	-	Jengo lote limepauliwa fedha pungufu ni Tsh.3,000,000/= ujenzi unaendelea vizuri	Fedha Tshs. 11,540,000/= zilizotumika kwa malipo ya fundi ujenzi, ununuzi wa vifaa vya ujenzi
	Halmashauri	11,540,000/=	11,540,000/=	-		
	M, Jimbo	4,566,000/=	4,566,000/=	363,000/=		
	Ofisi DC	200,000/=	200,000/=			
	Wananchi	350,000/=	350,000/=			
	Nguvu kazi	Nguvu kazi				
Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa pamoja na ofisi 1 ya walimu	Mfuko wa Jimbo	3,000,000/=		500,000/=	Msingi unaelekea kukamilika	Baada ya kukamilika kwa msingi wa jengo hilo hatua za ujenzi wa kuinua boma utaanza maramoja kwani tofari zipo eneo la mradi
Ujenzi wa shule shikizi mtaa wa Tulieni	Wananchi	Nguvu kazi Kukata miti pamoja na kujenga jengo hilo la shule shikizi la muda Tsh.230,000/=	Fedha iliyotumika kukata miti pamoja na ujenzi pia thamani ya ardhi Inakadiliwa Tsh.2,300,000/=	-	Jengo limejengwa kwa kiwango cha miti na limefikia hatua ya upauaji	Hatua za kuanza ujenzi wa jengo la kudumu la shule hiyo shikizi zinaendelea



	Kamati ya maendeleo ya kata WDC	250,000/=	250,000/=			

Pia ipo ofisi **1** ambayo haijakamilika ingawa inatumika Kijiji cha Shankala ambapo inakadiliwa kutengewa kiasi cha Tsh. **25,000,000/=** ili kukamilisha ujenzi. Sambamba na miradi hiyo ambayo imeshaanza kutekelezwa upo mradi mwingine ulioibuliwa na wananchi wa ujenzi wa kituo cha afya ambapo tayari tripu **9** za mawe za nguvu za wananchi zimeshafika eneo la mradi.

#### MAPATO

NA	JINA LA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	MAPATO	JUMLA
1	SALIO ANZIA	HALMASHAURI WANANCHI	3,154,567.37	3,154,567.37
2	RUZUKU KUTOKA MMC	HALMASHAURI	701,495	701,495
3	MFUKO WA MASALIA MALI KATA YA NSEMULWA	MH. MBUNGE MPANDA MJINI	552,000	554,000
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>4,408,062.37</b>	<b>4,408,062.37</b>

#### MATUMIZI

NA	JINA LA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA TENGWA	FEDHA TOLEWA	TUMIKA	BAKI	MAELEZO
1	SALIO ANZIA	HALMASHAURI WANANCHI	3,54,567.37	3,154,567.37	1,209,712	1,944,855.37	i)Ubebaji mawe tripu 3 shule ya msingi Nsemulwa ii)posho ya uendeshaji ofisi ya kata Nsemulwa iii) Uendeshaji akaunti ya kata iv)Ulipaji fidia mradi wa maji mtaa wa Tulieni chanzo ni fedha Ni mradi wa ukopesaji

							vikundi vya wajasiriamali
2	RUZUKU KUTOKA MMC	HALMASHAURI	701,495	701,495	-	701,495	
3	MFUKO WA WAJASILIAM ALI KATA YA NSEMULWA	MH. MBUNGE MPANDA MJINI	554000	55400	-	554000	
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>4,408,062.37</b>	<b>4,408,062.37</b>	<b>1,209,712</b>	<b>3,198,350.37</b>	

### SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

- Kushiriki katika siku ya usafi kiwanja cha ndege kwa ajili ya maandalizi ya mwenge
- Kushiriki katika siku ya Mwenge na watumishi wengine wa halmashauri ya Manispaa ya Mpanda. Mwenge ulikimbizwa na kuzindua miradi mbalimbali katika halmashauri.
- Kushirikiana na wataalamu na watendaji katika kutatua kesi mbalimbali za kijamii zilizowasilishwa ofisini
- Kutembelea kikundi cha chaki, kilichopewa mkopo wakati wa Mwenge ili kuona maendeleo ya kikundi.
- Kushirikiana na mtendaji wa mtaa Tulieni katika kuhamasisha wananchi kuchangia hela ya ujenzi wa kisima ambapo kila kaya ilikuwa inachangia **Tsh. 2,500/=**

### MAFANIKIO

Katika robo hii kata ya Nsemulwa, vikundi viwili kimoja cha vijana na kingine cha wanawake kilipatiwa mkopo wakati wa Mwenge.

JINA LA KIKUNDI	MTAA KILIPO	BIASHARA WANAZOFANYA	MKOPO WALIOPEWA KIASI	
MWIZA GROUP	NSEMULWA	Kutengenezwa wine na unga wa lishe	<b>5,000,000/=</b>	Halmashauri ya Manispaa
COOPERATION GROUP	MIGAZINI	Kutengeneza chaki	<b>10,000,000/=</b>	Mfuko wa wizara wa vijana

Vilevile kata ya Nsemulwa ina vikundi viwili ambavyo vipewa mkopo na halmashauri na vinaendelea vizuri na marejesho. Jedwali lifuatalo linaonyesha hali ya urejeshaji

JINA LA KIKUNDI	MTAA KILIPO	BIASHARA WANAZOFANYA	MKOPO WALIOPEWA KIASI	KIASI KILICHOREJESHWA	DENI LILILOBAKI
FEVAM GROUP	NSEMULWA	Kusindika wine Kutengenezwa shanga n.k	<b>3,000,000, /=</b>	<b>1,100,000/=</b>	<b>2,200,000/=</b>
TWIJUMILE	MIGAZINI	Kutengeneza chaki	<b>10,000,000/=</b>	<b>1,600,000/=</b>	<b>600,000/=</b>

### CHANGAMOTO

- Umbali wa mitaa hadi mitaa hivyo kufuatilia wananchi wachache kutokana na kutokuwana usafi
- Uelewe mdogo wa wananchi na kutokujua umuhimu wa kuunda vikundi.

**IDADI YA VISIMA NA MABOMBA KWA KILA MTA A PAMOJA NA MAPUNGUFU YAKE.**

NA	JINA LA MTA A	MAHITAJI	VILIVYOPO	PUNGUFU
1	NSEMULWA	5	1	4
2	MIGAZINI	5	0	5
3	KILIMANI	5	0	5
4	KICHANGANI	5	0	5
5	TULIENI	8	1- Vimekamilika	6
6	SHANKALA	8	0	8

**MAGATI YA MAJI YALIYOPO NA UPUNGUFU WAKE**

NA	JINA LA MTA A	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
1	<b>NSEMULWA</b>	<b>15</b>	<b>0</b>	<b>15</b>
2	<b>MIGAZINI</b>	<b>15</b>	<b>0</b>	<b>15</b>
3	<b>KILIMANI</b>	<b>15</b>	<b>2</b>	<b>13</b>
4	<b>KICHANGANI</b>	<b>7</b>	<b>0</b>	<b>7</b>
5	<b>TULIENI</b>	<b>15</b>	<b>0</b>	<b>15</b>
6	<b>SHANKALA</b>	<b>15</b>	<b>4</b>	<b>11</b>

**ILI KUKABILIANA NA UPUNGUFU WA HUDUMA YA MAJI PAMOJA NA HUDUMA NYINGINE YAFUATAYO YANASHAURIWA KUFANYIKA:-**

- Wananchi wanahamasishwa kuvuta maji kutoka chanzo cha mto Ikorongo kutumia mtandao wa bomba lililopita katikati ya kata hii ya Nsemulwa. Pia wamehamasishwa kuchimba visima
- Idara ya maji imeshafunga pampu kwenye visima vyote viwili mtaa wa Tulieni Ofisi ya mkurugenzi kupitia idara ya ardhi tayari wameshatenga eneo la soko
- Ombi kwa Mkurugenzi tunaomba fedha itolewe kwa ajili ya umaliziaji miradi viporo.
- Ombi kwa Mkurugenzi kupitia wataalamu wa Idara ya Ardhi waanze kugawa viwanja vya soko haraka iwezekanavyo ili kukabiliana na uibukaji wa magenge holela.
- Wajumbe wa WDC wameishukuru ya Ofisi ya Mkurugenzi kwa kutoa thamani za ofisi Kata ya Nsemulwa ambapo Kata imepokea viti 16 na meza 8.

**SEKTA YA ELIMU: ELIMU YA MSINGI**

Mpaka kukamilika kwa taarifa hii mwalimu mkuu S/M Nsemulwa alikuwa hajaleta taarifa yake ingawa aliombwa kuwasilisha taarifa hiyo.

### TAARIFA YA MAPATO FEDHA ZA RUZUKU

S/N	JINA LA WIZARA	CHANZO CHA FEDHA	MAPATO	JUMLA
1	Ruzuku kutoka MMC kwa ajili ya miradi	HALMASHAURI	1,614,419	1,614,419
2	Ruzuku kutoka MMC kwa ajili ya Utawala	HALMASHAURI	1,076,280	1,076,280
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>2,690,699</b>	<b>2,690,699</b>

### TAARIFA YA MATUMIZI FEDHA ZA RUZUKU

S/N	JINA LA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA TENGWA	FEDHA TOLEWA	TUMIKA	BAKI	MAELEZO
1	Ruzuku toka MMC kwa ajili ya mradi	HALMASHAURI	1,614,419.5	1,614,419	-	1,614,419	-Hakuna matumizi
2	Ruzuku kutoka MMC kwa ajili ya utawala	HALMASHAURI	1,076,280	1,076,280	956260	1200020	-Posho ya wenyeviti sita 6x50000. -Posho ya wajumbe Serikali za mitaa 440,000 -Matumizi ya ofisi ya mitaa na Kata.
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>2,690,699</b>	<b>2,690,699</b>	<b>956,260</b>	<b>1,734,439</b>	

### UJENZI WA NYUMBA BORA

- Katika kukabiliana na ujenzi holela wa makazi ofisi ya Mkurugenzi imeshatuma timu ya wataalam wa ardhi kwa ajili ya upimaji wa mradi wa viwanja awamu ya pili mtaa wa Tulieni ambapo zoezi hilo linaendelea mpaka sasa.
- Pia katika kudhibiti ujenzi holela wa nyumba wananchi wameshaukiwa kutonunua viwanja visivyopimwa maarufu kwa jina la (vishamba vidogo vidogo).

### ONYAKA

Katika kukabiliana na ujenzi wa nyumba bora wananchi wameelimishwa wanapojenga nyumba watumie tofali za kuchoma na wapaue kwa kutumia bati na sio nyasi.

### ULINZI NA USALAMA

Kwa kipindi cha kuanzia Aprily mpaka Juni **2017 – 2018** katika kata hii kumetokea vitendo vya uharifu ikiwemo wizi na taarifa hizo zilifikishwa kituo cha polisi na hatua zilichukuliwa pia wananchi wameelimishwa juu ya umuhimu wa kujitokeza katika ulinzi shirikishi (polisi jamii). Wenyeviti wa mitaa pamoja na watendaji wa mitaa wamefanya agenda hiyo ya ulinzi na usalama kuwa ya kudumu kila wanapoitisha mikutano ya hadhara kuizungumzia

Wananchi walipata fursa ya kuelimishwa juu ya umuhimu wa kujilinda na kulinda mali zao kupitia mkutano wa hadhara uliofanywa na jeshi la polisi tarehe **05.06.2018** katika viwanja vya S/M Nsemulwa.

### HALI YA MAJANGA

Kwa kipindi cha Aprily – Juni **2018** hakuna janga lolote lililojitokeza katika kata hii.

### TAARIFA YA IDARA YA AFYA KINGA KWA KAZI ZILIZOFANYIKA ROBO YA NNE 2017/2018 KWA KATA YA NSEMULWA.

NA	SHUGHULI	HALI YA UTEKELEZAJI	CHANGAMOTO	MIPANGO MIKAKATI
1	Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira	i)Nimesimamia kaya <b>9</b> zisizo na vyoo kuchimba, kujenga na kutumia choo bora, kaya <b>353</b> zenye vyoo vya asili kuboresha ii)Kusimamia ukusanyaji wa takwimu kutoka katika mitaa <b>5</b> ya kata na kijiji <b>1</b>	-Upungufu kwa mafuta ya kusafiri -Takwimu za kwenye daftari kutopatikana kwa wakati kutokana na viongozi wa mitaa kuchelewesha	Mkazo wa ujenzi na utumiaji wa vyoo bora unaendelea
2	Ukaguzi kwenye majengo ya biashara na kuongeza uelewa na kutafsiri sheria za mamlaka ya chakula, dawa na vipodozi ( <b>TFDA 2003, 2006</b> ) na matumizi yake na kukagua ubora usalama na ufanisi wa vyakula na bidhaa zitikanazo na vyakula.	Nimefanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya biashara ya vileo – <b>8</b> mamalish/baba lishe <b>-15</b> , bucha <b>-9</b> , kinyozi na saluni <b>14</b> maduka ya jumla na rejareja <b>-31</b> mashine za nafaka <b>-4</b> jumla ya majengo <b>3</b> yamekaguliwa <b>16</b> yamepewa notisi <b>5</b> ya mefungwa.	Kukosekana kwa vitendea kazi, karatasi za limu, pesa za kuchapa na kurudufu notisi na barua	Zoezi ni endelevu linaendelea ili kuwabaini wale wote waliokiuka sheria na kanuni za afya na kuwachukulia hatua.
3	Kudhibiti uchafu na uchafuzi wa mazingira ili kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mlipuko	Vipaumbele ni kufyeka na kupalilia majani, kudhibiti mlundikano wa uchafu kwenye maeneo ya makazi, biashara, taasisi na maeneo ya mikusanyiko	Upungufu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara kutokana na kuwa siku chache nahudumia kata mbili	Kuboresha usimamizi ili wananchi waepukane na uchafu na uchafuzi wa mazingira
4	Kusimamia na kutafsiri matumizi ya sheria ya <b>2009</b> , sheria ya hifadhi ya mazingira ya mwaka <b>2004</b> , sheria ndogo ya manispaa ya mwaka <b>2011</b> kifungu cha <b>96</b> uzuiaji magonjwa ya kuambukiza	Jumla ya watu <b>2</b> wametozwa faini ya uxhafu wa mazingira	Uelewa mdogo wa jamii kuhusu matumizi ya sheria kuu kutokana na kutohudhuria mikutano ya hadhara	Kutokuwepo kwa magonjwa ya mlipuko kwenye kata yangu
5	Kushiriki na kusimamia shughuli za usafi kila siku za jumamosi ya mwisho wa mwezi	Jumla ya siku za jumamosi za mwisho wa mwezi zimehudhuriwa	Baadhi ya wafanya biashara kutokuwepo maeneo yao ya biashara	Kuboresha usimamizi ili wananchi/umma wanasafisha mazingira

### MIUNDOMBINU ILIYOPO HAPA KATANI

#### (I) BARABARA

- Katika kata hii zipo barabara chache zilizochongwa na mitambo na baadhi ya mitaa hakuna kabisa barabara zilizochongwa
- Mh. Diwani wa kata hii ya Nsemulwa amewasiliana na watalamu wa **TARURA** kwa ajili ya kupunguza kero hiyo, na wataalamu wameahidi kutengeneza barabara za

mtaa wa Kichangani zenye urefu wa **Km 3** kazi hiyo itaanza wakati wowote kuanzia sasa mwaka **2018** kwani tayari msimu wa mvua umekwisha

- Barabara ndani ya kata hii wananchi wanatumia umeme wa **TANESCO** ingawa bado zoezi la usambazaji wa nguzo pamoja na nyaya zinaendelea
- Pia wananchi walio wengi ndani ya kata hii wanatumia umeme wa **SOLA**
- Upande wa mawasiliano ya simu wananchi ndani ya kata hii wanatumia mawasiliano ya simu za mkononi kwa kutumia mitandao ifuatayo :-  
**VODACOM, TIGO, AIRTEL** na **HALOTEL**.

## **CHANGAMOTO NA UFUMBUZI**

### **MAFANIKIO YANAYOPATIKANA KWENYE KATA**

1. Kata kukubaliwa mradi wa ujenzi wa kituo cha afya
2. Mkurugenzi kupima viwanja awamu ya pili

### **CHANGAMOTO ZILIZOMO NDANI YA KATA**

1. Elimu ya msingi
  - Upungufu wa miundombinu shule ya msingi Nsemulwa kama vile madarasa, ofisi za walimu pamoja na matundu ya vyoo
2. Shule kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi
3. Miundombinu ya barabara ni mibovu
2. Idadi ya visima na magati ya maji havitoshi
3. Kata haina kituo cha afya
4. Kata haina soko la uhakika
5. Kukosekana kwa fedha ya kumalizia miradi viporo

## **UFUMBUZI WA CHANGAMOTO**

### **1. Elimu ya msingi**

- Tayari wananchi wamechangia nguvu zao kwa kukusanya tofari na kupeleka eneo la shule kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa pia ofisi ya Mkurugenzi umekwisha ingiza kiasi cha milioni 10 kwenye A/C ya shule kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa.

## **HITIMISHO**

Uongozi wa Kata pamoja na uongozi wa mitaa utaendelea kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchangia nguvu zao katika miradi ya maendeleo pia ofisi ya Mkurugenzi inaombwa kuleta fedha kwa wakati mara tu wananchi wanapokuwa wameibua miradi hiyo na kuanza kutekeleza kwa kusogeza nguvu zao eneo la mradi.

## SEKTA YA KILIMO

NA	SHUGHULI ZILIZOFANYIKA	MAHALI	WAHUSIKA
1	Wakulima <b>710</b> wa ndani ya kata katika mitaa <b>3</b> mitatu wameingizwa kwenye daftari la wakulima	-Mtaa wa Tulieni -Mtaa wa Nsemulwa -Mtaa wa Kilimani	-A. kilimo -Wakulima wote
2	Kufanya tathimini ya uhalibifu wa mazao shambbani yalipo haribiwa na mifugo (ng'ombe na mbuzi) na kutafuta suluhu ya jambo hilo	-Mkulima -Mfugaji	-A. Kilimo -Kamati ya malalamiko
3	Kubaini maeneo yanayolimwa kwa msimu wa kilimo <b>2018/2019</b> sambamba na wakulima wanaolima mazao mbalimbali	-A. kilimo -Wenyeviti wa mitaa	-A. Kilimo -Wenyeviti wa mitaa
4	Kuhamasisha kilimo cha pamba na korosho kwa wakulima wote kata ya Nsemulwa kupitia mikutano ya hadhara.	-Kata na mitaa yote	-A. Kilimo -Watendaji wa mitaa yote
5	Kuandaa taarifa za kazi za robo, mwezi na mwaka za Kata ya Nsemulwa	-Kata	-A. Kilimo

### MAFANIKIO

Katika robo hii kata ya Nsemulwa, vikundi viwili kimoja cha vijana na kingine cha wanawake kilipatiwa mkopo wakati wa Mwenge.

JINA LA KIKUNDI	MTAA KILIPO	BIASHARA WANAZOFANYA	MKOPO WALIOPEWA KIASI	
MWIZA GROUP	NSEMULWA	Kutengenezwa wine na unga wa lishe	<b>5,000,000/=</b>	Halmashauri ya Manispaa
COOPERATION GROUP	MIGAZINI	Kutengeneza chaki	<b>10,000,000/=</b>	Mfuko wa wizara wa vijana

Vilevile kata ya Nsemulwa ina vikundi viwili ambavyo vlipewa mkopo na halmashauri na vinaendelea vizuri na marejesho. Jedwali lifuatalo linaonyesha hali ya urejeshaji

JINA LA KIKUNDI	MTAA KILIPO	BIASHARA WANAZOFANYA	MKOPO WALIOPEWA KIASI	KIASI KILICHOREJESHWA	DENI LILIOBAKI
FEVAM	NSEMULWA	Kusindika wine	<b>3,000,000, /=</b>	<b>1,100,000/=</b>	<b>2,200,000/=</b>

GROUP		Kutengenezwa shanga n.k			
TWIJUMILE	MIGAZINI	Kutengeneza chaki	<b>10,000,000/=</b>	<b>1,600,000/=</b>	<b>600,000/=</b>

### CHANGAMOTO

- Umbali wa mitaa hadi mitaa hivyo kufuatilia wananchi wachache kutokana na kutokuwana usafi
- Uelewe mdogo wa wananchi na kutokujua umuhimu wa kuunda vikundi.

### SEKTA YA KILIMO

NA	SHUGHULI ZILIZOFANYIKA	MAHALI	WAHUSIKA
1	Wakulima <b>710</b> wa ndani ya kata katika mitaa <b>3</b> mitatu wameingizwa kwenye daftari la wakulima	-Mtaa wa Tuliene -Mtaa wa Nsemulwa -Mtaa wa Kilimani	-A. kilimo -Wakulima wote
2	Kufanya tathimini ya uhalibifu wa mazao shambbani yalipo haribiwa na mifugo (ng'ombe na mbuzi) na kutafuta suluhu ya jambo hilo	-Mkulima -Mfugaji	-A.Kilimo -Kamati ya malalamiko
3	Kubaini maeneo yanayolimwa kwa msimu wa kilimo <b>2018/2019</b> sambamba na wakulima wanaolima mazao mbalimbali	-A. kilimo -Wenyeviti wa mitaa	-A.Kilimo -Wenyeviti wa mitaa
4	Kuhamasisha kilimo cha pamba na korosho kwa wakulima wote kata ya Nsemulwa kupitia mikutano ya hadhara.	-Kata na mitaa yote	-A. Kilimo -Watendaji wa mitaa yote
5	Kuandaa taarifa za kazi za robo, mwezi na mwaka za Kata ya Nsemulwa	-Kata	-A. Kilimo

**BAKARI KAPONA**

DIWANI KATA YA NSEMULWA



## **KATA YA SHANWE**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA SHANWE YA ROBO YA NNE YA APRIL –JUNE 2018.

### **1. UTANGULIZI**

Kata hii ya Shanswe ni miongoni mwa kata kumi na tano (**15**) zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na iko kaskazini magharibi mwa Manispaa ndani ya Tarafa ya Kashaulili na ina mitaa minne (**4**) ambayo ni Shanwe, Kigamboni, Kivukoni na Kilimahewa. Kwa mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka **2012** Kata hii ina jumla ya wakazi.

<b>Na.</b>	<b>MTAA</b>	<b>KAYA</b>	<b>WATU</b>	<b>ME</b>	<b>KE</b>
1	KIGAMBONI	1000	5100	2300	2800
2	SHANWE	270	900	430	470
3	KIVUKONI	950	4788	2245	2543
4	KILIMAHEWA	238	602	290	321
	<b>JUMLA</b>	<b>2462</b>	<b>11590</b>	<b>5265</b>	<b>6125</b>

### **2. SHUGHURI ZA WAKAZI**

1. Wakulima
2. Watumishi wa serikali na kwenye mashirika mbalimbali
3. Wafanyabiashara ndogondogo
4. Wafugaji wadogowadogo

### **3. VIKAO VYA KISHERIA**

- I. Ngazi ya Kata  
Imefanyika **WDC** moja ya tarehe **3/7/2018** ya robo ya nne (**4**) ambayo kaziwake ni kupitia na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Kata na pia kujadili na kupitisha taarifa mbalimbali za vikao vya mitaa na mikutano mikuu ya mita
- II. Ngazi ya mitaa  
Vimefanyika vikao vya ndani (**3**) kwa kila mtaa, pia imefanyika mikutano ya hadhara minne (**4**) kwa mitaa yote

### **4. MAPATO NA MATUMIZI**

- (a) Ngazi ya Kata
  1. Salio Tshs **61,000/=**
  2. Mapato 0
  3. Matumizi 0

Kwa kipindi cha miezi mitatu (**3**) hatujafanikiwa kupata fedha kutoka Halmashauri na pia kwa wadau

(b) Ngazi ya mitaa

1. Mtaa wa Kilimahewa wana **Tshs 802,000/=** za ujenzi wa Zahanati fedha hizi ni kati ya matarajio ya kukusanya **Tshs 8,000,000/=** kwa kaya **1600** kila kaya itachangia **Tshs 5,000/=** na fedha hizi hajizaanza kutumika
2. Mtaa wa Kigamboni - hakuna mapato
3. Mtaa wa Shanwe - hakuna mapato
4. Mtaa wa Kivukoni - hakuna mapato

## 5. MAMBO YALIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU

1. Tumefanikiwa kusimamia ukusanyaji wa fedha kiasi cha **Tshs 802,000/=** katika mtaa wa kilimahewa kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ambapo matarajio ni kukusanya **Tshs 8,000,000/=** kwa kaya **1600** na kila kaya imetegemea kutoa **Tshs 5,000/=**

## 6. HUDUMA ZA JAMII

### (a).ELIMU Y SEKONDARI NA MSINGI: MIUNDOMBINU

NA	SHULE	MADARASA			MADAWATI			VYOO					
		Mah	Yal	Pung	Mah	Yal	Pung	Mah		Yal		Pung	
								Me	Ke	Me	Ke	ME	ke
1	S/S SHANWE	24	12	12	821	561	260	12	12	6	6	6	6
2	S/M SHANWE	30	5	25	490	290	200	12	12	4	4	6	6
3	S/S KIVUKONI	27	5	22	489	148	141	12	12	3	3	9	9
4	S/S MAKANYAGIO	32	8	24	435	274	161	12	12	6	6	6	6

### MAELEZO.

Kwa msimu wa mwaka **2018- 2019** kila mtaa umewekewa malengo ya kujenga madarasa mawili kwa kila shule husika ambapo tayari wameshakusanya.

### (b). WALIMU NA WANAFUNZI

NA	SHULE	WALIMU			WANAFUNZI		
		ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
1	S/S Shanwe	18	19	27	406	473	880
2	S/M Sahnwe	7	10	18	552	623	1175
3	S/M Kivukoni	7	7	14	517	532	1049
4	S/M Makanyagio	5	9	14	664	697	1361

## 7. MAJI

NA	MTAA	VISIMA VILEFU			MAGATI		
		Vizima	Vibovu	Jumla	Mazima	Mabovu	Jumla
1	SHANWE	1	0	1	3	0	3
2	KIVUKONI	1	1	1	4	0	4
3	KIGAMBONI	1	0	1	5	0	5
4	KILIMAHWEA	0	0	0	4	0	4

Swala la maji siyo tatizo sana kw kata ya Shanwe na mitaa yake yote minne kwa sababu pipe zote za maji toka Ikolongo na Manga na Bwawani zimepitia hapa Shanwe, kwahiyo ni suala la kuunganisha mabomba kwa gharama za wananchi wenyewe.

## **8. AFYA**

### **(a) AFYA TIBA**

Kwa sasa wananchi wa kata hii ya Shanwe wanaendelea kupata huduma za Afya tiba pamoja na huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya na Hospitali ya Mwangaza lakini maandalizi ya ujenzi wa zahanati yamesha anza na kwa sasa tuko kwenye hatua ya michango na tumekusanya **Tshs 802,000/=** kati ya Tshs **8,000,000/=** zinazohitajika.

### **(b) AFYA KINGA**

Wananchi wanaendelea kuelimishwa juu ya usafi wa mazingir yao hususani kuwa na vyoo na kuvitumia ikiwa ni pamoja na kufyeka nyasi

## **9. UTAWALA BORA**

(a) Utawala wa Demokrasia unaendelea kutumika kupitia vikao vya WDC ambapo wajumbe wake ni wenyeviti wa serikali za mitaa, wataalamu wote ngazi ya kata. Viongozi wa chama Tawala na viongozi wa dini kadhalika katika mitaa utawala wa Demokrasia unatumika kupitia vikao vya ndani na mikutano ya hadhara

### **(b) UTAWALA WA KISHERIA**

Unatumika kupitia baraza la kata ambapo watu wote huelekezwa kupeleka malalamiko yao na kusikilizwa na maamuzi kutolewa kwa kufuata sheria.

## **10. ULINZI NA USALAMA**

Swala la ulinzi na usalama linaendelea kufanyiwa kazi kwa usimamizi wa kamati ya ulinzi na usalama wa kata pamoja na Polisi wa kata na viongozi wote wa chama na serikali pamoja na viongozi wa dini

## **11. KILIMO/MIFUGO/UVUVI**

Yamelimwa mashamba darasa heka tatu **(3)** pia zinatarajiwa kulimwa heka **19** za zao la korosho zimelimwa hekali **125** za mahidni, zimelimwa hekali **12** za karanga , zimelimwa heklai **25** za mihogo, zimelimwa hekali **12** za viazi

Imetolewa chanjo ya ng'ombe **133** idadi ya ng'ombe **13**, mbuzi **80** mbwa **68**,kuku **1778**

## **12. BIASHARA NA MASOKO**

Wananchi wa kata ya Shanwe wanaendelea kufanya shughuli zao za biashara ndogondogo kwente maeneo yao na kwenye maneo ya wazi ya mtaa wa Kilimahewa na kigamboni wakati wanasubiri kibari cha kubadilisha maeneo ya wazi kuwa maeneo soko

## **13. ARIDHI**

Tayari maeneo ya Kilimahewa yameshapimwa kuwa viwanja na wahusika wanasubiri kugawiwa viwanja hivyo.

## 14. MAENDELEO YA JAMII

### i. IKUNDI

a. **V**Katika sekta hii kikundi kimoja cha wanawake cha **UWT** Shanwe kilichokopeshwa fedha kinaendelea na mkopo huo vizuri na karibu wamalize mkopo huo

ii. **TASAF** vilevile Nyanja hii ya maendeleo ya jamii kaya 49 za mtaa wa kivukoni zinaendelea kunufaika na malipo ya **CCT** pamoja na malipo yanayotokana na ajira za muda wanazofanya kazi walengwa

### iii. UKIMWI

Kupitia kamati ya UKIMWI ya kata iliendelea kutoa hamasa juu ya kupunguza maambukizi mpya ya VVU/UKIMWI kupitia vikao na mikutano ya hadhara.

## 15. MIGOGORO

Ipo migogoro miwili kama ifuatavyo:-

a. Mgogoro wa zahani – huo ni mgogoro wa kuvamiwa kwa eneo la shule ya msingi Shanwe na familia ya Mzee MWANAMELI bado unaendelea pamoja na kwamba Mzee huo ameshafaliki na kwamba bado shauli liko kwenye Mahakama ya rufaa lakini bado familia yake wanaendelea kumenga maeneo ya shule na kuunza kwa kisiingizio cha kwamba Baba yao ndiye aliyeuza kabla hajafaliki.

b. Mgogoro mpya ni ule wa wananchi kuvamia maeneo ya serikali ya kachoma mjinga na kujimilikisha na hii imeshafanyika kwa

i. SKORASTIKA SADARA

ii. SAIDI SHAGILOMO

Jitihada za kuwaondoa wavamizi hawa zilifanywa na uongozi wa kata pamoja na baraza la kata kwa kuwaondoa wa vamizi hawa lakini wavamizi hawa walikwenda kukata rufaa kwenye baraza la ardhi na nyumba la Wilaya na huko wakapewa haki bila kushirikisha uongozi wa kata na baraza la kata kwahiyo mpaka sasa takribani kiasi cha heka 4 kimechukuliwa na wavamizi hao lakini taarifa ya uvamizi huo imeshatolewa kwa mkurugenzi.

## 16. MAJANGA NA MATUKIO.

1. Tarehe **31/5/2018**, Majira ya saa **5.00** Asubuhi mtoto **SEPHANIA KASTORY**, umri wa miaka **6** kabila msukuma mwanafunzi wa darasa la awali S/Msingi makanyagio jinsi(me) mkazi wa mtaa wa shanwe akiwa anachota maji na dada yake kwenye shimo aliteleza na kutumbukia kwenye shimo hilo la maji na alifariki dunia.

2. Tarehe **5/6/2018** Majira ya saa **8.00** Mchana kijana **EMMENUELI MAIKO** mwenye umri wa miaka 20 kabila mpimbwe mkazi wa mtaa wa shanwe jinsi (me) alijirushia kwenye dimbwi la maji alipokuwa anafyatua tofali na wenzake na kufariki dunia na alikuwa amefanya kazi ya kufyatua tofali hapo kwa muda wa mwezi mzima wote wa 5. katika matukio hayo yote mawili taarifa zilizotolewa polisi. Na kwa tukio la pili kikosi cha zima moto kilisaidia kuopoa mwili wa marehemu kwenye maji. Pamoja na matukio hayo yote tayari uongozi wa kata umewaagiza kampuni ya KASCO ambao ndiyo waliyo chimba kifusi wayafuie mashimo hayo.

## **17. CHANGAMOTO**

1. Ucheleweshaji wa kibali cha kubadili matumizi ya Ardhi kwa ajiri ya masoko kwa mitaa ya Kivukoni na Kigamboni.
2. Kwa muda mrefu hatujapokea fedha za ruzuku kwa ajiri ya miradi ya maendeleo na uendeshaji Ofisi na za wenye viti wa seriakali za mitaa
3. Ofisi ya kata ya shanwe kutokuwa na chombo cha usafiri (pikipiki) kwa sababu kata ya shanwe iko mbali na makao makuu zaidi ya kilometa **7**.

Naomba kuwasilisha,

**KANONI LUCAS**  
**MHE.DIWANI KATA YA SHANWE.**

## KATA YA UWANJA WA NDEGE

TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI ZA SERIKALI ROBO YA NNE KATA YA UWANJA WA NDEGE  
APRILI -JUNI 2018

### UTANGULIZI:

#### MAHARI KATA ILIPO

- Kata ya Uwanja wa ndege ni miongoni mwa Kata kumi na tano zilizopo katika Manispaa ya Mpanda Kata hii ina mitaa ambayo ni Mtaa wa Airtel, Mtaa wa Msufini na Mtaa wa mnazi mmoja.

#### MIPAKA YA KATA

- Upande wa Kaskazini imepakana Kata ya Nsemulwa, Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Ilembo, Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Kashaulili na Mpanda Hoteli, Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Mtapenda Halmashauri ya Nsimbo.

### IDADI YA WATU NA MAKAZI

- Kata ya Uwanja wa Ndege ina jumla ya Kaya **1545** na Idadi ya watu ni **3386** , Wanaume **449** na Wanawake ni **3887** watoto **2890** Jumla ya wasio na uwezo wa Kufanya kazi wanaume ni 1435 wanawake 1453 Wazee ni 445, wanawake 171, wanaume ni 274 na Yatima ni 126 na wanawake ni 90.

### SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA WAKAZI

Wakazi wa Kata ya Uwanja wa Ndege wanajishughulisha na shughuli zifuatazo;

- Uchimbaji mdogo mdogo wa madini.
- Wafanyakazi wa Taasisi mbalimbali za Serikali, Makampuni ya ulinzi.
- Kilimo cha Jembe la Mkono ( Bustani za mbogamboga na Ujasiliamali)
- Biashara ndogondogo za Ujasiliamali
- Ufugaji mdogo wa ndani na nje ya mabanda Mfano. Kuku, Bata, Ng'ombe, Mbuzi n.k

### UONGOZI NA UTAWALA;

- MH. DIWANI WA KATA
- WENYEVITI 3 WA MITAA WA KUCHAGULIWA
- WAJUMBE 15 ( KUMI NA TANO) WA SERIKALI
- WATENDAJI MTAA WAWILI (2) WA KUJAJILIWA
- AFISA KILIMO 1
- AFISA MAENDELEO YA JAMII 1
- AFISA UVUVI WA KATA 1
- AFISA AFYA 1

### VIKAO NA MIKUTANO

JINA LA MTAA	KATA	AINA KIKAO YA	TAREHE YA KIKAO	MAHALI	MAELEZO
AIRTEL	UWANJA WA NDEGE	CHA SERIKALI YA MTAA	27/04/2018 31/05/2018 29/06/2018	OFISI YA KATA	Kikao cha kawaida dhalula
MSUFINI	-	-	-	-	Mtaa hauna Mtendaji
MNAZI MMOJA 2	UWANJA WA NDEGE	MKUTANO WA HADHARA WA KATA	-	-	
KATA UWANJA WA NDEGE	UWANJA WA NDEGE	KIKAO CHA DHARULA (WDC)	26/04/2018	OFISI YA KATA	Tarehe iliyopangwa kufanya WDC kulikuwa zoel la nida

## MAPATO NA MATUMIZI

S/N	JINA MTA	CHANZO CHA MAPATO	KIASI	SALIO TUMIKA	BAKI
1	AIRTEL	TOZO VIBARI S/MTAA AIRTEL	100,000/=	30,000/=	70,000/=
2	MSUFINI	-	-	-	-
3	MHAZINI MMOJA	HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA.  TOZO VIBARI VYA TOFALI	190,000  20,000/=	160,000 Kutengeneza thamani za ofisi ya mtaa  10,000/= kusomba tofali	30,000  10,000/=
4	KATA UWANJA WA NDEGE	FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO TOKA HALMASHAURI YA MANISPAA	433,000/=	Ukarabati bomba la maji 271 mahitaji ya stationary za uandaaji wa taarifa na matumizi ya ofisi 62,000/=	
5	UWANJA WA NDEGE	UFADHILI WA MBUNGE WA JIMBO LA MPANDA MJINI	1000,0000/=	1000,000/= kukopesha vikundi	

### SEKTA YA MAJI

- Gati moja la maji katika mtaa wa mnazimmoja za kisima kimoja kirefu
- Magati manne ya maji toka chanzo cha ikorongo. Bomba lililofadhiliwa na mbunge limekamiliika ila halitoi maji kutokana na hujuma ya kukataa bomba.

### CHANGAMOTO

- Uharibifu wa miundombinu ya maji kukata mabomba ya maji.

### MAENDELEO YA UJENZI MIRADI YA 2017/2018

NA	AINA YA MRADI	MTAA	CHANZO CHA FEDHA		GHARAMA ZA MRADI
1	<b>SEKTA YA HUDUMA YA JAMII</b> UJENZI WA OFISI YA KATA UWANJA WA NDEGE NA OFISI ZA MITAA	AIRTEL	HALMASHAURI  296,000,000	NGUVU ZA WANANCHI  7400000	37,000,000/=
2	<b>UJENZI WA SOKO LA KATA</b> UWANJA WA NDEGE NA MASOKO YA MITAA MAWILI	AIRTEL	37,600,000	9,400,000	47,000,000/=
3	<b>SEKTA YA ELIMU</b> UJENZI WA MADARAJA (2) MAWILI SHULE YA MSINGI KASIMBA	AIRTEL	12,200,000	1,800,000	14,000,000/=
	UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU NSEMULWA SEKONDARI	AIRTEL	20,000,000	5,000,000	25000,000/=
	UJENZI WA MATUNDU 4 YA CHOO, NSEMULWA	AIRTEL	4,800,000	1,200,000	6,000,000/=

	SEKONDARI				
	<b><u>SEKTA YA AFYA NA MAJI</u></b> UJENZI WA ZAHANATI 2 KATIKA MITAA	- AIRTEL -MNAZI MMOJA - MSUFINI	48,000,000	12,000,000	60,000,000/=
	KUJENGA MAGATI YA MAJI 9 KWA KILA MTAA KATIKA 3	A) AIRTEL B) MNAZI MMOJA C) MSUFINI	14,700,000	3,000,000	15,000,000/=

### HUDUMA ZA JAMII

- Kila katika mtaa kuna mashine za kusaga nafaka hasa mahindi
- Kuna barabara kuu nne zinazolingia na kutoka katika Kata na Mitaa.
- Kuna kiwanja cha ndege.
- Kuna viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza thamani.
- Kuna mashine za kumenya karanga.
- Huduma ya nishati ya umeme inapatika katika Mitaa yote mitatu.

### CHANGAMOTO ZA KUTOA HUDUMA ZA JAMII.

- Mashine zimekaa jirani na makazi ya watu, hivyo kuhatarisha Afya.
- Barabara hizi hazipitiki kwa muda wote kwani madaraja hujaa mchanga na hivyo maji kupita juu ya madaraja na kukatika barabara na madaraja kama daraja la Nsemulwa Mnazi Mmoja, na Airtel Kilimahewa.
- Kukosekana eneo la barabara ya kuunganisha Mitaa yote mitatu hivyo kufanya shughuli za kimzunguko za kawaida kwenye Mitaa hii kuwa zenye usumbufu.
- Kukosekana kwa ofisi katika Kata na Mitaa. (Majengo ya Serikali).

### UTATUZI.

Kuitisha nguvu kazi kufukua madaraja mawili na kulima barabara kwa mkono baada ya barabara hizo kukatika.

Kuendelea kukusanya nguvu kazi mpaka sasa tofali 15,000 zimekusanywa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Kata.

Michango mpaka sasa kaya zimechangia Tsh.82,000/= ambazo ni kwa ajili ya asilimia 20% ya nguvu za jamii. Michango inaendelea.

### MAENDELEO YA UJENZI MIRADI YA 2017/2018

NA	AINA YA MRADI	MTAA	CHANZO CHA FEDHA		GHARAMA ZA MRADI
1	<b><u>SEKTA YA HUDUMA YA JAMII</u></b> UJENZI WA OFISI YA KATA UWANJA WA NDEGE NA OFISI ZA MITAA	AIRTEL	HALMASHAUR I 29,600,000	NGUVU ZA WANANCHI 7,400,000	37,000,000/=
2	<b><u>UJENZI WA SOKO LA KATA</u></b> UWANJA WA NDEGE NA MASOKO YA MITAA MAWILI	AIRTEL	37,600,000	9,400,000	47,000,000/=
3	<b><u>SEKTA YA ELIMU</u></b> UJENZI WA MADARAJA (2) MAWILI SHULE YA MSINGI KASIMBA	AIRTEL	12,200,000	1,800,000	14,000,000/=
	UJENZI WA NYUMBA YA	AIRTEL			



	WALIMU NSEMULWA SEKONDARI		20,000,000	5,000,000	25000,000/=
	UJENZI WA MATUNDU 4 YA CHOO, NSEMULWA SEKONDARI	AIRTEL	4,800,000	1,200,000	6,000,000/=
	<b>SEKTA YA AFYA NA MAJI</b> UJENZI WA ZAHANATI 2 1) KATA NA 2) KATIKA MTAU MMOJA WA KATA YA UWANJA WA NDEGE	- AIRTEL - MNAZI MMOJA - MSUFINI	48,000,000	12,000,000	60,000,000/=
	KUJENGA MAGATI YA MAJI 9 KWA KILA MTAU KATIKA 3	D) AIRTEL E) MNAZI MMOJA F) MSUFINI	14,700,000	3,000,000	15,000,000/=

### UTEKELEZAJI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA MWAKA 2018

S/N	SHUGHULI ZILIZOFANYIKA	MAHALI	WAHUSIKA
1	Wakulima 1203 wameandikishwa na kuuisha daftari la wakulima	- Kata na Mitaa yake yote	- A. Kilimo - Wenyeviti wa Mitaa yote. - Wajumbe Serikali za Mitaa wote
2	Kubaini eneo sahihi la kilimo ambapo Ekari 2145 zimebainika zikilimwa mazao mbalimbali	- kata na Mitaa yake yote	- A. Kilimo - Wakulima
3	Kukusanya taarifa za mifugo mbalimbali inayofugwa ambapo jumla ya mifugo 324 imehesabika	-Mitaa wa Msufini	- A. Kilimo - Mkwenyekeziti wa Mtaa
4	Kutembelea vikundi 3 vya kilimo na kikundi kimoja cha ufugaji	- Mtaa wa Airtel - Mtaa wa Mnazi mmoja	- A. Kilimo - A. Maendeleo ya jamii Kata
5	Kuhudhuria mikutano ya hadhara na vikao vya ndani vya kila Mtaa jumla ya vikao 3 vya ndani na mikutano 4 ya hadhara.	- WDC - Mtaa wa Msufini - Mtaa wa Airtel - Mtaa wa Mnazi mmoja	- A. Kilimo
6	Kushiriki katika zoezi la uandikishaji vitambulisho vya Uraia (NIDA)	- Kata ya Uwanja wandege	- A. Kilimo

## 7. CHANGAMOTO ZA KILIMO

Ukosefu wa usafiri kwa Afya Kilimo.

### UTEKELEZAJI WA MIFUGO NA UVUVI SHUGHULI ZILIZOFANYIKA

- Kuhakikisha wafugaji wa samaki kuongeza idadi ya mabwawa ambapo imeweza kuleta ongezeko la mabwawa 5 mapya ambapo kwa jumla ni mabwawa 10.
- Kuongeza idadi ya wafugaji wa samaki na kufikia wafugaji wa samaki 1 na jumla wafugaji wa samaki 3.

- Kufanyia marekebisho ya mabwawa 2 ambapo yalikauka kwa kipindi cha jua kali na bwawa moja liliathirika na mvua kwa kubomoka kuta za bwawa na baadhi ya samaki kupotea kwa maji.
- Kuhamasisha wafanyabiashara kukata leseni za kuuza samaki ambapo wameweza kukata leseni wafanyabiashara 2.
- Watu 2 wamehamasika kwa huitaji wa kufuga samaki na wana maeneo ya kufugia.

### CHANGAMOTO

- Mabadiliko ya hali ya hewa ambapo ilipelekea kubomoka kwa kingo za mabwawa ya samaki na kupotea kwa samaki.
- Ukosefu wa usafiri.
- Ukosefu wa zana nzuri za shughuli za ufugaji wa samaki na chakula.

### UTEKELEZAJI WA MAENDELEO YA JAMII

SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAFANIKIO	CHANGAMOTO
- Kushiriki katika zoezi la uandikishaji na upigaji picha vitambulisho vya Kitaifa kwa wananchi Uwanja wa Ndege	-Zoezi la uandikishaji wananchi lilifanyika kwa kuwashirikisha wenyeviti wa Mtaa na wajumbe wa Serikali za Mtaa.	-Wananchi walihudhuria kwa wingi katika kujiandikisha na kupiga picha. -Wananchi walichangia kwa hiari chakula ili kufanikisha zoezi hilo.	-Kutokujua kusoma na kuandika kwa wananchi wengi na hivyo kufanya zoezi kuwa gumu na kuchukua muda mrefu.
-Kushiriki katika malipo ya Tasafu Kata ya Misunkumilo	-Malipo yalifanyika kwa walengwa wote	-Walengwa wote walilipwa ruzuku zao	-
-Kuhudhuria kikao kazi na Anglikana kizazi -Kipya	- kikao kilifanyika	-CCW na wasimamizi walihudhuria kikao kwa pamoja na kuelezea kazi tunazofanya kwa pamoja	- Baadhi ya CCW, wamekuwa wakitoa taarifa za uongo
-Kushiriki katika kikao cha WDC (Maendeleo ya Kata) Kata ya Uwanja wa Ndege.	-kikao kilifanyika	- ajumbe wote wa kikao walihudhuria	-
-Kushiriki katika usafi siku ya Muungano, ikiwa ni maandalizi ya kuupokea mwenge katika kiwanja cha Ndege Mpanda	-Usafi ulifanyika kwa kushirikiana na wanafunzi wa shule ya Sekondari Nsemulwa na wanafunzi wa shule ya Msingi Kasimba.	-Sehemu kubwa ya uwanja iliweza kufanyiwa usafi	- Vitendea kazi vichache. - Baadhi ya wajumbe hawakushiriki katika zoezi hili
-Kutembelea kikundi cha wanawake Tumaini	-Kuwahimiza kumalizia kufanya marekebisho ya mkopo wao	-Kikundi kinajitahidi katika kufanya marejesho	-
-Kutatua kesi mbalimbali zilizofika ofisi za Kijamii	-Kesi hizi zilisikilizwa katika ofisi ya Kata kwa kushirikiana na wataalamu wengine	-Tuliweza kutatua kesi mbalimbali zilizowasilishwa kwa kutoa ushauri	-
-Kushiriki katika zoezi la kutembelea na kutambua kaya	-Wajumbe husika tulitembelea kaya baadhi ili kupata uhakiki wa kaya hizo	- Tulifanikiwa kutembelea baadhi ya kaya (walengwa) wanaohudumiwa na kizazi kipya	- Baadhi ya walengwa kutotoa ushirikiano pindi wanapotembelewa.
-kuhudhuria mkutano wa	-Mkutano ulifanyika wananchi	-Wananchi	-

hadhara na wananchi Kata ya Uwanja wa Ndege.	walihudhuria mkutano huo uliohusu uandikiashaji wa vitambulisho vya kitaifa na uchangiaji wa ujenzi wa ofisi ya Kata	walikubali kuchangia zoezi la nida pia walikubali kuchangia ujenzi wa ofisi na kila kaya ilipaswa kuchangia Tsh.2,000/=	
--	--	---	--

#### TAARIFA YA MAREJESHO KWA VIKUNDI VINAVYODAIWA

JINA LA KIKUNDI	RIBA NA KIASI CHA MKOPO	MTAA WANAFANYIA SHUGHULI ZAO	SHUGHULI WANAZOFANYA	MAREJESHO YA MKOPO	DENI LILIOBAKI
ROGERS GROUP	1,650,000/=	MNAZI MMOJA	BIASHARA	1,100,000	550,000/=
TUJINASUE GROUP	2,200,000/=	MNAZI MMOJA	KILIMO CHA BUSTANI NA B. NDOGONDOGO	780,000	1,420,000
MAARIFA GROUP	1,100,000/=	AIRTEL	KUUZA MAZAO NA MGAHAWA	1,100,000	WAMEMALIZA
HATANGIMANA GROUP	2,200,000/=	AIRTEL	KILIMO CHA BUSTANI	65,000	2,135,000
FIKIRIA GROUP	2,750,000/=	MSUFINI	KUUZA ASALI	446,000	2,304,000
TUJIVUNE GROUP	2,200,000/=	MSUFINI	KILIMO CHA BUSTANI	85,000	2,115,000
TUMAINI GROUP	1,100,000/=	MSUFINI	BIASHARA NDOGO NDOGO	1000,000	100,000

#### MAFANIKIO:-

Katika robo hii kikundi kimoja cha vijana MAARIFA kilipewa mkojo wakati wa mwenge.

#### TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHURI ZA AFYA KINGA KATA YA UWANJA WA NDEGE

NA	SHUGHULI	HALI YA UTEKELEZAJI	CHANGAMOTO	MIPANGO MIKAKATI
1.	Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira.	i)Nimesimamia kaya 9 zisizo na vyoo kuchimba, kujenga na kutumia choo bora, kaya 58 zenye vyoo vya asili kuboresha ii)Kusimamia kukusanyaji wa takwimu kutoka katika mitaa 3	-Upungufu kwa mafuta ya usafiri. -Takwimu za kwenye daftari kutopatikana kwa wakati kutokana na viongozi wa mitaa kuchelewesha	Mkazo wa ujenzi na utumiaji wa vyoo bora unaendelea.
2.	Ukaguzi kwenye majengo ya biashara na kuogeza uelea na kustafsiri sheria za mamlaka ya chakula, dawa na vipodozi (TFDA) 2003, 2006) na matumizi yake na kukagua ubora usalama na ufanisi wa vyakula na bidhaa zitokanazo na vyakula.	Nimefanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya vileo3 mama/ baba lishe-9, bucha 5, kinyozi na saluni 4 maduka ya jumla na rejereje 24, mashine za nafaka 8, Jumla ya	Kukosekana kwa vitendea kazi, karatasi za rimu, pesa za kudurufu notisi na barua	Zoezi ni endelevu linaendelea ili kuwabaini wale wote waliokiuka sheria na kanuni za afya na kuwachukulia hatua.

		majengo .....yamekaguliwa, .....yamepewa notisi .....yamefungiwa.		
3.	Kudhibiti uchafu na uchafuzi wa mazingira ili kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mlipuko	Vipaumbele ni kufyeka na kupalilia majani, kudhibiti mlundikano wa uchafu kwenye maeneo ya makazi, biashara, taasisi na maeneo ya mikusanyiko.	Upungufu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara kutokana na kuwa siku chache nahudumia kata mbili	Kuboresha usimamizi ili wananchi waepukane na uchafu na uchafuzi wa mazingira.
4.	Kusimamia na kutafsiri matumizi ya sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009, sheria ya hifadhi ya mazingira ya mwaka 2004, sheria ndogo ya 2011 kifungu cha 96 uzuiaji magonjwa ya kuambukiza.	Jumla ya Mtu 1 ametozwa faini ya uchafu wa mazingira	Uelewa mdogo wa Jamii kuhusu matumizi ya sheria kuu kutokana na kutohudhuria mikutano ya hadhara	Kutokuwepo kwa magonjwa ya mlipuko kwenye kata yangu
5.	Kushiriki na kusimamia shughuli za usafi kila siku za jumamosi za mwisho wa mwezi.	Nimehudhuria usafi jumamosi za mwisho wa mwezi	Baadhi ya wafanya biashara kutokuwepo maeneo yao biashara	Kuboresha usimamizi ili wananchi / umma wanasafishe mazingira.

#### UTEKELEZAJI WA ELIMU.

#### SHULE YA MSINGI KASIMBA JULAI - 2018

##### (i) TAKWIMU ZA WANAFUNZI

DARASA	WAVULANA	WASICHANA	JUMLA	MIKONDO
AWALI	164	172	336	13
I	208	243	451	11
II	279	300	579	14
III	182	185	367	9
IV	173	146	319	8
V	101	104	205	5
VI	72	88	160	4
VII	54	87	141	4
<b>JUMLA</b>	<b>1233</b>	<b>1325</b>	<b>2558</b>	<b>68</b>

##### (ii) SAMANI ZA SHULE

NA.	AINA YA SAMANI	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
01.	MADAWATI	852	300	552
02.	MEZA	136	12	124
03.	VITI	136	12	124
04.	KABATI	140	01	139

**(iii) MIUNDO MBINU YA SHULE**

NA.	AINA YA SAMANI	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
01.	VYUMBA VYA MADARSA	68	08	60
02.	OFISI	04	02	02
03.	STOO	04	01	03
04.	MATUNDU YA VYOO	115	10	105
05.	WALIMU	68	24	44

**(iv) SHUGHULI ZA MAENDELEO**

**a) TAALUMA**

Shule hii imeendelea kufanya vizuri katika suala la Elimu, kwa kuwaandaa vizuri wanafunzi wote na hasa wanaotegemea kufanya mtihani wa Taifa kwa Darasa la IV na VII. Hata hivyo mwezi huu wa tatu Shule imefanya mtihani wa **MOCKO KATA** ambao umefanyika Kiwilaya na kusimamiwa na Walimu kutoka Shule jirani na kusahihishwa na Walimu wa hapa Shuleni.

Kwa ufupi waliofanya mtihani walikuwa ni 134 kati ya wanafunzi 141 na kati ya hao wanafunzi 75 wamepata alama za ujumla yaani alama 100. Hivyo kwa ishara hii na pate kueleza kuwa suala la Elimu linakwenda vizuri.

**b) UJENZI**

Kutokana na suala la upungufu wa vyumba vya Madarasa, Kamati ya Shule iliazimia kujenga vyumba hivyo vya madarasa kwa kiwango cha Maboma.

Hata hivyo kwa kushirikiana na wadau wa Shule hii Shule imefanikiwa kujenga vyumba viwili vya madarasa kwa hatua ya maboma. Hata hivyo vyanzo vya pesa hiyo ni kama ifuatavyo:-

- Nguvu za wananchi ambao walichangia pesa pamoja na tofali za vyumba vyote.
- Pesa jumla ya **Tsh.1, 000,000/= (milioni moja)** ambayo ilitolewa na ofisi ya Kata.
- Pia tumepata **jumla ya Tsh.4, 000,000/=(milioni nne)** kutoka mfuko wa Jimbo.

Hivyo kutokana na michango hiyo yote tumefanikiwa kunyanyua na kumaliza maboma yote mawili na ipo pesa **Tsh.1,750,000/=** ambayo tunakusudia tuanze kunyanyua na kujenga boma lingine ili kukabiliana na upungufu uliopo wa vyumba vya madarasa.

**(v)CHANGAMOTO ZILIZOPO.**

Zipo changamoto nyingi ambazo kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikipunguza ufanisi wa Shule yetu na hizo tunaendelea kukabiliana nazo ili ikiwezekana tuzimalize tukishirikiana na wadau wa Elimu hapa Airtel na Mpanda kwa ujumla. Nazo ni:-

- a. Upungufu mkubwa wa Walimu. Hii ni changamoto kubwa sana; Shule ina walimu 20 mpaka sasa. Na kwa ukubwa wa Shule tulipaswa tuwe na walimu 68. Hivyo tunaupungufu wa walimu 48.Hata hivyo tumekuwa tunaendelea kuomba walimu ili kukidhi haja ya Shule yetu.
- b. Upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa. Shule hii inaupungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, kiasi cha kufanya wanafunzi zaidi ya mia mbili (200) wakae chumba kimoja ambayo ni hatari sana.  
Hata hivyo tunaendelea na jamii kuona tunatatua kwa kujenga maboma hayo nab ado jitihada zinaendelea ili kuongeza zaidi.
- c. Utoro wa wanafunzi na hasa ule wa rejareja ambao unakuwamisha ufanisi katika masomo. Hivyo endapo wangehudhuria wote; Mafanikio ya kitaaluma yangepatikana na ufaulu ungekuwa mkubwa sana.  
Tunaendelea kutoa elimu na kukaa na wazazi wa watoto watoro ili waache tabia hiyo na kuona elimu ni zaidi kwa mafanikio yao baadae.

- d. Upungufu wa nyumba za walimu. Shule haina nyumba za watumishi, hivyo wameishi kwenye jamii na wakati mwingine ni mbali na Shule. Hivyo wakati mwingine wanachelewa au kutokamilisha majukumu kikamilifu kwa kuwa wanapaswa kushiriki katika masuala ya kijamii pia. Hata hivyo tunaendelea kuhimiza na kufafanua kila mara Kanuni na Sheria za utumishi ili kuendana na kukabiliana na changamoto hizo.

## ELIMU SEKONDARI

### I. IDARA YA WALIMU.

<b>MASOMO</b>		<b>SANAA – 01</b>
<b>SANAA</b>	<b>16</b>	
<b>SANYANSI</b>	<b>03</b>	
<b>HISABATI</b>	<b>02</b>	
<b>JUMLA</b>	<b>21</b>	
		<b>UPUNGUFU: SAYANSI - 02</b>
		<b>HISABATI 02</b>
		<b>JUMLA 05</b>

### II. IDADI YA WANAFUNZI.

KIDATO I			KIDATO II			KIDATO III			KIDATO IV		
WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA
72	76	148	72	78	150	57	50	107	42	30	72
<b>JUMLA KUU</b>			<b>WAVULANA</b>			<b>WASICHANA</b>			<b>JUMLA</b>		
			<b>243</b>			<b>234</b>			<b>477</b>		

### III. MAJENGO NA SAMANI.

	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU
<b>MADARASA</b>	12	08	04
<b>OFISI</b>	02	02	-
<b>MAABARA</b>	03	03	-
<b>MATUNDU YA VYOO</b>	18	12	06
<b>MEZA ZA WALIMU</b>	20	16	04
<b>VITI VYA WALIMU</b>	20	12	08
<b>MEZA ZA WANAFUNZI</b>	477	313	164

#### 1. HALI YA UFAULU -2017

KIDATO II									KIDATO IV								
WALIOANDIKISH WA			WALIOFANYA			WALIOFAULU			WALIOANDIKI SHWA			WALIOFANYA			WALIOFAULU		
ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML
64	61	125	64	61	125	60	51	111	37	22	59	37	22	59	19	14	33

Katika robo hii ya tatu kuna janga la kukatika barabara na madaraja kunakosababishwa na mvua zilizonyesha mfululizo hivyo kumekuwa na hofu na usumbufu kwa wanajamii wa Kata ya Uwanja wa Ndege ambao wengi wao hufanya shughuli zao za kiuchumi nje ya Kata. Barabara hizo ni inayotoka kasimba darajani kuelekea Airtel na kivuko cha Airtel kwenda kilimahewa pia kufurika daraja la Nsemulwa – Mnazimmoja.

## **UTATUZI:**

Wananchi kushirikiana na Mweshimiwa Diwani wa Kata ya Uwanja wa Ndege pamoja na watumishi wamejitolea kurekebisha kasoro hizo Jumamosi ya mwisho wa mwezi 3 walifukua daraja Nsemulwa 16/04/2018 kuweka mbao kwenye kivuko cha Airtel –Kilimahewa ili waweze kupita kwa muda.Mipango inaendelea kuwekwa ili kushughulikia barabara ya Airtel – Kasimba darajani.

## **ULINZI NA USALAMA**

- Shughuli za Ulinzi na Usalama zinaendelea kwa mwendelezo wa vikao vya kamati kuweka mikakati ya Ulinzi na usalama hasa katika Kiwanja cha ndege ambapo Dora zinaendelea kubaini waharifu wanaotumia mazingira ya Uwanja wa ndege kama maficho.
- Wizi mwingine mdogomdogo ambao tunaendelea kuuthibiti kwa kuunda vikundi vya Ulinzi shirikishi Jamii
- Matukio ya vikundi vya uharifu vilivyojiunda na kujipa majina mfano; Mtaa wa Mnazi mmoja kuna kikundi cha watu watano (5) wanajiita ninja.
- Ulinzi na usalama kikao cha tarehe 16/03/2018 kilibaini kuwa kunatatizo la uingiaji wa wahamiaji haramu na kwa kukosa haki ya kisheria ya kumiliki Ardhi wamekuwa wakinunua Ardhi isiyopimwa na kujenga. Pia kuvamia maeneo yaliyotengwa . kutoshiriki kwenye shughuli za maendeleo.

## **CHANGAMOTO ZILIZOPO**

- Kukosekana kwa Ofisi ya Kata na za Mitaa hivyo kukosa mahali salama pa kutolea huduma.
- Uhaba wa Watumishi hasa kukosekana kwa Mtendaji wa Mtaa mmoja na Afisa Afya tulienae kwa sasa ana hudumia Kata mbili , Afisa kilimo anahudumia Kata mbili, hivyo hulemewa na ukubwa wa maeneo
- Kukosekana kwa maji hasa eneo la mtaa wa Msufini hakuna gati hata moja la maji
- Kutopimwa Viwanja hasa eneo la mnazi mmoja kunapelekea wananchi kujenga kiholela na wahamiaji haramu kuvamia.
- Ongezeko kubwa la Watoto walioandikishwa darasa la kwanza ni tatizo hasa yanapokosekana madarasa ya kufundishia.

## **UTATUZI/MAFANIKIO**

- Kukusanya tofari zilizotumika kujenga darasa 2 shule ya Msingi Kasimba ili kuondoa tatizo la upungufu wa Madarasa
- Kuchangia kiasi cha shilingi **1,000,000/=**kwa ajili ya kuingiza umeme shule ya Sekondari Nsemulwa
- Kukusanya tofari Eflu ishirini na tatu ( **15,000/=**) kwaajili ya Ujenzi wa Ofisi ya Kata
- Kuchangia Shilingi **1,000,000/=** za Ujenzi wa darasa shule ya Msingi Kasimba ambalo limefikia hatua ya ukamilishaji ili kuendelea kupunguza tatizo la upungufu wa madarasa pesa hizi ni kutokana na pesa ya Ruzuku inayoletwa kwenye WDC,wafadhili,Equipt.

- Kuendelea kufanya Vikao na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kupata michango kwa ajili ya kuongeza Magati ya Maji ambapo tumepata **Tsh. 1000000/=** kutoka kwa Mh. Mbunge ambazo zimetumika kujenga Gati moja la maji Mitaa wa Airtel C.

**MWISHO**

Utatuzi /mafanikio/changamoto vimebainishwa kwenye kila kurasa katika kila sekta.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,  
Naomba kuwasilisha.**

**STEPHANO A. MWAKABAFU  
DIWANI KATA YA UWANJA WA NDEGE**